# Nipashe

Jumatano Desemba 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581152

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Uhamiaji** wamnasa mtuhumiwa uhalifu wa kimataifa

UKURASA 4




siasa

JUMATANO DESEMBA 7, 2022 Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Heche awashukia vijana, awakumbusha mabadiliko duniani huletwa na kundi hilo

Viwanda simu za mkononi vinavyoleta kiama DRC

Ruto, Gachagua watoa somo sera za kuwafikia vijana

MIAKA 61 YA UHURU

Tanzania bado inabanwa utegemezi kiteknolojia, unazidi kufifisha maendeleo

UKURASA 13

# VIKUMBO

## • Vigogo CCM wachuana kuwania u-NEC, wamo mawaziri, wakubwa ndani ya chama... *Ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama hicho, Daniel Chongolo, wakati akikagua maandalizi mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa 10 wa CCM jijini Dodoma jana, unaotarajiwa kufanyika kesho na kesho kutwa. Kushoto ni Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka. **PICHA: IKULUMAALUM**


## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### WAZIRI ATAKA KUUNGWA MKONO KUKABILI UKATILI



WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wanasheria nchini kuunga mkono juhudi za serikali kukabili...

**UKURASA WA 4**

### ZUMARIDI NA WENZAKE 80 WAACHIWA HURU

MCHUNGAJI Diana Bundala, maarufu mfalme Zumaridi mungu chini ya jua na wafuasi wake 80, wameachiwa huru...

**UKURASA WA 10**

### MUHIMBILI YASAIDIWA VIFAA TIBA MIL. 50/-

KAMPUNI ya Letshego Holdings imesaidia vifaa tiba kwa kitengo cha wagonjwa watoto wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili...


## DC kikaangoni madai kumpiga makofi msichana

UKURASA 3



## Wanasheria wasema Assad anastahili kulipwa hadi 2026

UKURASA 3

MICHEZO YANGA, NAMUNGO PATACHIMBIKA LEO UK.32 KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA




Kamishna wa Uhamiaji, Usimamizi na Udhibiti wa Mipaka nchini, Samweli Mahirane, akiongea na waandishi wa habari jana. Habari Uk. 4. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ORODHA YA WAGOMBEA NEC

1. ABASI Tarimba Gulam Dr. ABEID
2. Rija Rajab
3. Dr. ABUBAKARI Abubakari Ally
4. ACHIKUO Mtamila Abdul
5. ALLY Hamisi Abdallah
6. AMBILIKILE George Fabian
7. AZZAN Idd Mohamed
8. BAKARI Athumani Said
9. BASHANZI Anaclet Mbeikya
10. BASHE Hussein Mohamed
11. BASHUNGWA Innocent Lugha
12. Dkt. BATINOLUHO Ladislaus Bushoberwa
13. BAYYO Festa Banga
14. BIGAMBO Emmanuel Japhet
15. BINTO Binto Mawazo
16. BUMBULI Hassan Maulid
17. CHACHA Emmanuel Ndege
18. Dr. CHALi Frederick Henri
19. CHARLES Richard Bundala
20. CHAWAKA Gabriel Joseph
21. CHITIN KA Joseph Meshack
22. CHONJO Steven David
23. DAM BAYA Hamis Hassan
24. DAU DA Shafih Kajuna
25. Dr. FOCUS Erasto
26. GEHERI Joseph Laurent
27. Bishop GWAJIMA Josephat Mathias
28. HASUNGA Japhety Ngailonga
29. Dr. HIN DI Hindi Mastai
30. HOZA Francis Heri
31. Prof. IRIRA Samwel Michael
32. JAZZAA Salim Almasi Seif
33. JOSEPH George mabula
34. KALINJU NA Eumachius Wendalin
35. KAMINYOG E Joel George
36. KANGA Frederick Furaha
37. KANGOYE Jackson Ryoba
38. KAPIGA Harris Newman
39. KASA Mashaka Fadhili
40. KASALAMA Justus Athanas
41. KASESELA Richard Atufigwege
42. KASH EKU Msukuma Joseph
43. Dr. KASIGA Gervas Andrew (P.H.D)
44. KAYOM BO Burkard Gallus
45. KENGIA Josamu Anael
46. Dr. KHADU DU Chisuligwe Salum
47. Dr. KIBACHA Peter Eliji
48. KIBONA Joseph Etson
49. Eng. KIHAKA Burton
50. KILAJA Christopher Jacob
51. KILUVIA Swalehe Sadiki
52. KIMWAGA Yusufu Mohamed
53. KIOBYA Ashiraph Sadru
54. Dr. KOM BA George John
55. KOM BA Andrew Francis (KUCHONJOMA)
56. KYASI Mugwagi Samweli S.
57. KYESH E Sospeter Rugemarila
58. LAIZERIbrahimu Sendui
59. Eng. LEMILIA David Saiquran
60. LENGANASA Lenana Soipey
61. LINYAMA Hassan Ally
62. LORRY John Msuri
63. LUBANGO Martine Shigongo
64. LUBINGA Nqemela Eslom
65. LUFUNG ULO Jonas Francis
66. LUKUVI William Vangimembe
67. LUMATO Omari Bahati
68. LUSANGIJA Dama samora
69. MABELELE Buluba Luteia
70. MACHA Anamringi ssay
71. MACHAGE Yohana Mwema
72. MACHAI Masanja John
73. Dkt. MADELU Mwigulu Lameck Nchemba
74. MAGEM BE Lewa Safari
75. MAGOTI Kamese Bernard
76. MAHANDE Mabula Michael
77. MAH EN DA Leonard gaga (QWIHAYA)
78. MAH UNDI Yusuf Hussen
79. MAKAM BA January Yusuf
80. MAKAN DA Lusinqi Sita
81. MALELA Mohamed Chibwana
82. MALISA Beno Morris
83. MALYETA Yela Ligemba
84. MANARA Haji Sunday
85. MANGUNGU Murtaza Ally
86. MASELE Stephen Julius
87. Dr. MASON DA Yohana Paul
88. MASUKA Tumaini Benjamnin
89. MATAMBO Mohamed Hassan
90. MAYO Wilhelmon Wilbroard
91. MBILINYI Jotham Daima
92. Dkt. M OEDE Geofred Leonard
93. MDEM E Said Rajab
94. MGAWE Galus Paschal
95. MGUMIA Fadhili Hamza
96. MHONGOLE Stanslaus Thomas
97. MIRUM BA Bernad brahimu
98. MISIGALO Josephat Kanatali
99. MKODYA Clemence Salehe
100. MKOTYA Khamis Suleman
101. MOLLEL Simon K.
102. MOSHI Goodluck Wilson
103. MROSSO Severini Bernardi
104. Dr. MSENGI brahim. H.
105. MSOM E Jackson Wlliam
106. MTITU Evaristo Andreas
107. MTULIA Maulid Saidi
108. MUDHIHIR Mudhihir Mohamed
109. MUH UZA Baruan Abdallah
110. MULONGO David Mayala
111. MUSTAPHA Hamidu brahim
112. MUYOM BYA Johnson Fredrick
113. MWACHA Emmanuel Raymond
114. MWAIFWANI Cosmas Aron
115. MWAKIBETE Charles Fredy
116. MWAKIPESILE Charles Michael
117. MWAKISU Noah Edson
118. MWAMBE Wilson Elias
119. MWANYIKA Deodatus Philip
120. Dr. MWEM BEZI Gaspar Petro
121. MWIJ UKI Habas Chrizant
122. MWING E Mussa Pendes
123. MWITA Charles N.
124. NANAI Francis Majige
125. NANAU KA Joel Arthur
126. NANGORO Alais Taleck
127. NCHIM BI Alexander John
128. NDEJEM BI Deo John
129. NDILITO Netho Ndiiima
130. NDOSI Kennedy Elimereck
131. NGAJIRO Fred Fabian (VUNJABEI)
132. NGEM ELA Edmund Rweyemamu
133. NGEWE Gilliard Wilson
134. NGODA Hamisi Ayob
135. NGONYANI Edwin Amandus
136. NGULI Faraji Taratibu
137. NNAUYE Nape Moses
138. NSANZUGWANKO Daniel Nicodemu
139. NSEKELA Khalid Mussa
140. NYABAKARI James Rudonya
141. NYAGAWA Reuben Reuben
142. NYAM BELWA Anold Gosbert
143. NYANGWINE Nyambari C.
144. NYAWENGA Mohamed Omari
145. NYERERE Manyerere Jackton
146. NZOTA Mganwa
147. NZOWA George Yangison
148. NZYUGU Hassan Juma
149. PARESO Pantaleo Victory
150. PINDA Gephrey Privatus Mizengo
151. RAG E Aden smail
152. RU HULA Mohamed Moshi
153. RUTTA Deogratias Mgeni
154. SAGINI Jumanne Abdallah
155. SAIDI Mussa Mansour
156. SALU Falila Fabian
157. SALUM Yasini Musa
158. SANGA Haran Nyakisa
159. SARAKIKYA William Ndeoya
160. SHAURI Alex Stanford
161. SHEMAHONGE Baraka Ramadhan
162. SHENDA Charles Samson
163. SHIRIMA Mursal Musa
164. SILAA Jerry William
165. SIMBACHAWENE George Boniface
166. SULAIMANI Olise Rashidi
167. SULEIMANIsmail Abdulnuru
168. TEM BA Alphonce Boniface
169. TIBANYEN DERA Julius Kakuru
170. WAMBU RA Chacha Mwita
171. WASIRA Stephen Masato
172. ZAMBI Thadeo Daimon

**WANAWAKE BARA**

1. AISHA Wally Ally
2. AM INA Hoza Salehe
3. AM INA Selehe Mollel
4. ANGEL Andrew Akilimali
5. ANGELLAH Jasmine Kairuki
6. ANNA Agatha Msuya
7. ASHA Ramadhani Baraka
8. ASH MA Muhai Hakim
9. ASHURA Rashidi Mshumba
10. ASIA Miyasi Rajabu
11. ASSUM PTER Nshunju Mshama
12. ASU MPTA marcel Muna
13. CHRISTINA Solomon Mndeme
14. Dkt. ASHATU Kijaji
15. Dkt. BIBIANA Ambrose Massawe
16. Dkt. TUMAINI Juma Sanga
17. Dkt. VERONICA Francis Shao
18. DOREEN Peter Noni
19. Dr. ANG ELINA William Samike
20. Dr. ANG ELIN E Sylvester Mabula
21. Dr. JOYCE Nimrod Sigala
22. Dr. SHAMAA Mohamed Nawar
23. EDINA Ernest Kalambo
24. ELLEN Makungu Bogohe
25. FARIDA Salum Mgomi
26. FENELA Ephraim Mukangara
27. FLORENCE Sastory Masunga
28. GETRUDE Jerome Haule
29. GETRUDE Senni Kassara
30. GRACE George Kahama
31. HADIJA Shabani Taya (Keisha)
32. HALIMA Ramadhan Abdallah
33. HALIMA Yahaya Mpinge
34. HAPPIN ESS William Mgongo
35. HILDA Augustine Bwimba
36. HILDA Benjamini Kapinga

## Vikumbo vigogo kinyang'anyiro NEC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NI VIKUMBO. Ndivyo inavyoonekana au kuelezewa kutokana na vigogo wa serikali na chama wanavyochuana kuwania kugombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wanachama hao na makada wanatarajiwa kujinadi mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 10 wa Taifa utakaoanza leo katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC), jijini hapo.

Wakati macho na masikio ya Watanzania yakielekezwa Dodoma kwenye mkutano huo, joto la kinyang'anyiro hicho lilianza kupamba moto jana baada ya wagombea wa nafasi hizo, wakiwamo mawaziri na waliowahi kushika nyadhifa za juu ndani ya chama na serikali wakijaribu kutumia mbinu mbalimbali kuomba kura.

Vigogo hao wanawania nafasi za ujumbe wa NEC kutoka makundi ya Wanaume Tanzania Bara, Wanawake Tanzania Bara, Wanaume Zanzibar na Wanawake Zanzibar.

Miongoni mwa wanachama mashuhuri wanaotifuana katika kinyang'anyiro cha kundi la wanaume Tanzania Bara ni Tarimba Abbas, Japhet Hasunga, Richard Kasesela, Joseph Musukuma, William Lukuvi, Dk. Mwigulu Nchemba, January Makamba, Deo Mwanyika, Deo Ndejembi, Nape Nnauye, Geoffrey Pinda, Jumanne Sagini, Jerry Silaa, George Simbachawene ma Stephen Wassira.

Katika kundi la wanawake Tanzania Bara, miongoni mwa watu maarufu ni Angellah Kairuki, Christina Mndeme, Dk. Angeline Mabula, Dk. Fenela Mukangara, Namelok Sokoine, Queen Mlozi, Ritha Mlaki na Sophia Simba.

Baadhi ya wagombea wanaowania nafasi za wanaume Zanzibar ni Abdallah Sadala Mabodi, Shaka Hamdu Shaka, Mudric Ramadhan Soraga wakati waliopitishwa katika kundi la wanawake Zanzibar ni Yasmin Yusufal Aloo, Moudline Castico, Najma Murtaza Giga na Dk. Saada Mkuya Salum.

**SHAKA ANENA**

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo baada ya kumalizika kikao cha NEC, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema kikao hicho kimefanya uchambuzi na kuteua majina ya wanachama wa kuwania nafasi hiyo.

"Halmashauri Kuu imeteua wanachama 251 kuwa wagombea wa nafasi za ujumbe wa NEC. Hawa watapigiwa kwenye mkutano mkuu, kwa Zanzibar wameteuliwa wanachama 123, watakaochaguliwa ni 15 bara na 15 Zanzibar," alisema. Alifafanua kuwa wanachama waliojitokeza kuomba kuteuliwa kuwania nafasi hizo ni 2,703 na haijawahi kutokea tangu CCM imezaliwa.

"Chama chetu kwa mara ya kwanza wanaCCM wamehamasika vya kutosha kujitokeza kuomba nafasi mbalimbali, kwa upande wa Tanzania bara wamejitokeza 2,149 na Zanzibar wamejitokeza 554,"alisema.

Kadhalika, alisema kikao hicho kimependekeza jina la Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea uenyekiti na Abdulrahman Kinana kuwa Mgombea Makamu Mwenyekiti Tanzania bara na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi kugombea Makamu Mwenyekiti upande wa Zanzibar.

"Pia kazi itakayofanyika kwenye mkutano mkuu ni kupokea taarifa ya utekelezaji wa kipindi cha miaka tano ya CCM, kuanzia 2017-2022, pia kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM kutoka serikali zote mbili," alisema.

## HABARI KITAIFA




Waendesha pikipiki, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa kwenye msururu mrefu wa kusubiri kununua petroli katika kituo cha kuuzia mafuta cha TOP Oil, jirani na stendi kuu ya mabasi ya wilaya hiyo jana, baada ya kutokea uhaba wa bidhaa hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanasheria wasema Assad anastahili kulipwa hadi 2026

**Na Kulwa Mzee**

WANASHERIA wa kujitegemea wamesema aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, anapaswa kulipwa mishahara yake yote na malipo mengine kwa kipindi chote alichokuwa hayuko kazini hadi mwaka 2026 kwa sababu aliondolewa kinyume cha Katiba.

Wanasheria hao kwa nyakati tofauti, waliyasema hayo jana ikiwa ni siku moja baada ya hukumu kutolewa na Mahakama Kuu Masijala Kuu, mbele ya majaji Dk. Benhaji Masoud, Juliana Masabo na Edwin Kakolaki.

Akizungumzia hilo, Wakili Frank Chacha alisema, Prof. Assad ana haki ya kudai mishahara yake yote, kiinua mgongo kama mtumishi mwingine ambaye aliondolewa kazini kinyume cha utaratibu.

Wakili Majura Magafu, akizungumzia uamuzi huo alisema Prof. Assad anaweza kuzipata haki zake kwanza, kwa kuangalia barua yake ya uteuzi ilivyoeleza kuhusu haki zake endapo ataachishwa kazi.

"Suala la kwanza la kuangalia ni ile barua yake ya uteuzi inaeleza nini. Je, atapata haki zipi endapo ataachishwa kazi na suala la pili, Prof. Assad ana haki ya kudai haki zake kwa sababu nafasi yake ni ya kikatiba na kuondolewa kwake Katiba ilitakiwa kufuatwa," alisema Magafu.

Wakili Edson Kilatu akichangia hoja alisema alipokea vizuri uamuzi wa Mahakama Kuu kwa sababu unaanza kuwakumbusha misingi ya Katiba ambayo inatakiwa kuzingatiwa na kutiiwa pasipokuwa na shaka.

"CAG ni nafasi nyeti haitofautiani na majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani kwa sababu ya nafasi aliyo nayo ndiyo maana Katiba imemwekea kinga kwamba ukitaka kumtoa lazima kufuata taratibu ambazo Katiba inataka zifuatwe.

"Kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Ukaguzi kinaruhusu mkaguzi kupewa mkataba wa miaka kama mitano baada ya hapo inawezekana akaongezewa au asiongezewe wakati Katiba inataka akishika nafasi hiyo atumikie mpaka atakapofikia umri wa kustaafu, ndiyo maana kwenye uamuzi wa mahakama imesema, kwanza imetengua hicho Kifungu.

"Lakini cha pili ikasema kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ilitakiwa Assad aendelee kubaki kwenye nafasi yake mpaka anapofikisha umri wa kustaafu. Sasa aliondolewa kabla ndiyo maana mahakama imesema uamuzi wa kumtoa ulikuwa kinyume cha Katiba ya nchi.

"Suala ambalo limezua mjadala ni lile la kwamba baada ya kuwa mahakama imeona aliondolewa kimakosa pamoja na kwamba imekataa kusema na huyu aliyepo sasa kwamba yupo kinyume cha Katiba na imesema kwamba uteuzi wake ulifuata misingi inayotakiwa na vigezo vyote ambavyo alitakiwa awe navyo, alikuwa navyo. Kwa hiyo mahakama imeishia kusema Assad alitolewa kimakosa lakini imekataa kusema huyu aliyeingia aliingia kimakosa.

"Changamoto inakuja sasa unafuu upi ambao Profesa Assad anatakiwa aupate. Bahati mbaya wakati wa kesi inafunguliwa msingi uliokuwapo ni wa kutamka tu kwamba alitolewa kimakosa. Hawakwenda mbali kwamba kama mahakama itaona hapana sababu za kumrudisha kwenye nafasi yake labda alipwe fidia, mishahara yake aliyotumikia, sasa bahati mbaya kesi ya kikatiba haiendi huko.

"Mahakama haiwezi kutoa uamuzi zaidi ya kile ambacho hakipo mbele ya mahakama. Sasa hiyo hoja haikuwapo ndiyo maana mahakama iliishia pale," alisema Kilatu.

Alisema changamoto iliyopo ni kwamba alitakiwa aunganishe na maombi ya fidia lakini pia kwa sababu ni shauri la kikatiba, maombi kwenye mashauri ya kikatiba yana mipaka yake kwa hiyo mara nyingi haiwezi kwenda kwenye kiwango cha fidia labda kama angefungua kesi ya aina nyingine.

Prof. Assad aliyeteuliwa mwaka 2014, aliondolewa katika nafasi yake Novemba, 2019 na alitakiwa kuendelea kuwepo kwa mujibu wa Katiba hadi 2026 atakapokuwa amefikisha umri wa kustaafu wa miaka 65.

# Mkuu wa Wilaya matatani kwa madai kupiga msichana makofi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI maadhimisho ya siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili yakiendelea, Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga, anadaiwa kumpiga makofi msichana Frolencia Crispin (20), mkazi wa kijiji cha Mbangala na kumjeruhi jicho la kulia.

Kutokana na madai hayo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, ameshatuma kikosi kazi cha wataalamu wa ustawi wa jamii kufuatilia sakata hilo na kubaini kama lina ukweli.

Waziri Gwajima alisema jana kuwa ametuma kikosi kazi hicho kiende nyumbani kwa msichana huyo ili kumpa ushauri wakati shauri hilo likiendelea.

Akizungumza na Nipashe juzi, msichana huyo ambaye anaishi na mama yake baada ya baba yake kufariki dunia, alisema tukio hilo lilitokea Alhamisi iliyopita baada ya kukaa pembezoni mwa ukuta wa jukwaani ulioko kata ya Mkwajuni, Makao Makuu ya Wilaya ambako inadaiwa hairuhusiwi.

Wakati wakiwa jukwaani wakiangalia mpira, alisema Simalenga alifika na kuwaita, wenzake walikimbia na yeye alitii na kumsogelea na ndipo alipopigwa makofi na kumuumiza jicho la kulia.

Alisema baada ya kurudi nyumbani, walezi wake ambao wakati huo walikuwa hawapo, walirejea aliwaeleza kilichotokea ndipo walipokwenda polisi.

"Polisi mwenye namba WP 13294 alimpatia hati namba MKW/IR/2022 kwa ajili ya kwenda kutibiwa Hospitali ya Mwambani, baada ya kuangaliwa nimepewa rufani kwenda Hospitali ya Mkoa, jicho lilikuwa linavuja maji.

**MAMA ANENA**

Mama mzazi wa msichana huyo, Costancia Dulla, alisema kutokana na kutokuwa na uwezo amekuwa akisaidiwa matibabu ya mtoto wake na kaka zake (wajomba wa msichana huyo).

Mama huyo alisema amesikitishwa na kitendo cha kiongozi huyo alichokiita cha mabavu kwa kumpiga na kumjeruhi mtoto wake. Aliwaomba viongozi na wadau wamsaidie kupata fedha ili mtoto wake aende hospitali ya Mkoa kama alivyoshauriwa na daktari wa Mwambani.

Mjomba wa msichana huyo, Joseph Dulla, alisema alipigiwa simu na dada yake (mama wa msichana) akimweleza kuhusu tukio hilo na alipokwenda walikwenda polisi na baadaye hospitalini ambako daktari aliwataka waende Hospitali ya Mkoa kwa kuwa jicho linatoa maji.

**MTUHUMIWA AFUNGUKA**

Simalenga alipotafutwa na gazeti hili jana alisema kuwa hawezi kulizungumzia kwa kuwa limeingiliana na mambo ya siasa.

"Ninaomba suala hili la msichana anayedai kupigwa na mimi nisilizungumze kwa sasa, samahani sana maana kuna mambo ya kisiasa, kuna wanasiasa wapo nyuma yake katika jambo hili,"alisema na kukata simu.


KNAUF

## PUBLIC TENDER NOTICE

### TENDER NO: MKURANGA II 3652 CONSTRUCTION SERVICE IN DESIGN AND BUILD (EXTENSION) OF EXISTING PLASTERBOARD PRODUCTION LINE.

**Knauf international** is one of the world's leading manufacturers of modern insulation materials, drylining systems, plasters, thermal insulation composite systems, paints, floor screed, floor systems, construction equipment, tools, and other accessories. Knauf has more than 300 production facilities, with sales organizations in over 90 countries, 40,000 employees worldwide.

**Knauf Gypsum Tanzania Limited** being a part of Knauf international produces German quality drywall products using locally sourced materials. **Knauf Tanzania** is going to extend its plasterboard production line, located at Kisemvule, Mkuranga, Tanzania, from the manufacturing capacity of **15 million square to 40.5 million square.**

**The Company do hereby** invite competitive, reliable, well performing, experienced and eligible **Local Contractors** to tender for the construction service in **Design and Build** of its plasterboard production line based on the description and pre – qualification criteria provided in the table below.

**Description and pre – qualification criteria**

| No | Reference number | Description of work | Pre-qualification criteria |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkuranga II 3652 | • Extension of current plant building' <br>• New raw material stock area <br>• New parking area including internal roads. <br>• New social building | Civil and Building works Contractor Class 1 |

If your company meets the pre – qualification criteria you may obtain information from the Procurement & Logistics department at Knauf HQ offices, **Plot 17 Block 186030 14110 • Off Kinondoni Road • Mwindu Lane street, Dar es salaam** from 10:00AM to 16:00PM weekdays only.

A complete set of Tender Documents in English which include tender rules, terms and conditions will be available for physical collection at a fee of Tshs. 100,000/=. Funds must be deposited to the below bank details; (ensure your company details are clearly indicated on the deposit slip when collecting the tender documents for record and reference)

| BANK DETAILS | |
|---|---|
| Bank Name: | CRDB Bank Tanzania Ltd |
| Account Name: | **KNAUF GYPSUM TANZANIA LTD** |
| Account Number | **0150440243800** |
| Branch | Oysterbay Branch |

Submission deadline is **14th December 2022,** Late tenders, partial submission will not be considered.
**ENQUIRIES:** Magretha.VanDerMerwe@knauf.com
**NB: This tender advert does not entail any commitment on the part of Knauf to any applicant. Knauf reserves the right to accept or reject any or all applications without incurring any obligation to inform the applicant (s) of the grounds.**

217172602

HABARI KITAIFA

# Zumaridi, wenzake 80 waachiwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MCHUNGAJI Diana Bundala, maarufu mfalme Zumaridi mungu chini ya jua na wafuasi wake 80, wameachiwa huru huku wenzao watatu wakikutwa na kesi ya kujibu katika kesi ya kufanya mkusanyiko usio halali.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, imefikia uamuzi huo jana baada ya kusikiliza ushahidi na vielelezo vilivyofikishwa mahakamani kuhusu shauri hilo na waendesha mashtaka wa Jamhuri kupitia vipengele vyote huku wakiwakuta washtakiwa hao 81 bila kesi ya kujibu.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Clescensia Mushi, alieleza kutoa uamuzi huo baada ya kujiridhisha kuwa washtakiwa hao 81 walioachiwa huru hawakuguswa na vipengele muhimu vinavyotakiwa katika kuthibitisha makosa ya jinai kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Clescensia aliwataja washtakiwa waliokutwa na kesi ya kujibu kuwa ni Juma Hamis, Meshak Joseph na Daud Manyanda kwa kupatikana na kesi ya kujibu na kuendelea na kesi hiyo katika hatua ya utetezi.

Bundala anaendelea kubaki kizuizini kutokana na kesi ya jinai inayomkabili ya shtaka la usafirishaji haramu wa binadamu kinyume cha sheria huku Jamhuri ikiendelea na shughuli za kutafuta ushahidi wa shtaka hilo.

Katika hatua nyingine mahakama hiyo jana iliendelea kusikiliza kesi ya kuwazuia maofisa wa serikali kutekeleza majukumu yao inayomkabili Zumaridi na wenzake wanane kwa kusikiliza mashahidi wawili kutoka upande wa utetezi na kesi iliahirishwa mpaka Desemba 7, mwaka huu, mahakama ikitarajia kuendelea kusikiliza mashahidi upande wa utetezi kwa kusalia mashahidi wawili pekee.

Hakimu Clescensia aliwataja washtakiwa waliokutwa na kesi ya kujibu katika shauri hilo kuwa ni Juma Hamis, Meshak Joseph na Daud Manyanda.

Alisema washtakiwa hao walikutwa na kesi ya kujibu kwa kuwa ni pekee waliotajwa na mashahidi wa upande wa Jamhuri kuwa walisababisha majeraha na maumivu dhidi ya askari waliokwenda nyumbani kwa Zumaridi, Februari 23, 2022 kwa ajili ya kuwakamata.

"Uamuzi wa kuwaachia washtakiwa 81 umetokana na upande wa Jamhuri kushindwa kujenga kesi yao yaani 'Prima facie' kwa kuwa mashahidi wake walishindwa kutambua washtakiwa kuwa walitenda makosa au la," alisema Mushi.

Baada ya uamuzi huo, Hakimu Mushi aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 20, mwaka huu, itakapoitwa ili washtakiwa watatu waliokutwa na kesi ya kujibu waanze kujitetea.

Akizungumza nje ya mahakama baada ya uamuzi huo, Wakili wa Utetezi, Erick Mutta, alisema mahakama imetenda haki kwenye shauri hilo na kudai kuwa yeye pamoja mawakili wenzake wa utetezi wanajipanga kuhakikisha washtakiwa watatu waliokutwa na kosa la kujibu wanaachiwa huru.

"Tumeridhika na uamuzi uliyotolewa leo (jana) sasa hivi tunajipanga kwa ajili ya kuanza utetezi wetu dhidi ya hawa waliokutwa na kesi ya kujibu ikiwa ni jukumu letu kuhakikisha wateja wetu wanapata haki katika kesi hii," alisema.

Katika kesi hiyo upande wa utetezi unaongozwa na mawakili, Erick Mutta, Steven Kitale, Amri Linus na Merckzedeck Gunda, huku upande wa Jamhuri ukiongozwa na mwendesha mashtaka, Dorcas Akyoo, Mwanahawa Changale na Degratius Rumanyika.

Zumaridi anaendelea kubaki kizuizini kutokana na kesi ya jinai inayomkabili ya shtaka la usafirishaji haramu wa binadamu kinyume cha sheria huku Jamhuri ikiendelea na shughuli za kutafuta ushahidi juu ya shtaka hilo ili kuendelee kusikilizwa.



Rais wa Taasisi ya Umoja wa Amani Kwanza, inayotoa elimu ya utunzaji wa amani kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, George Wilson, akizungumza katika mkutano wa wanachama kutoka mikoa mbalimbali, mkoani Dar es Salaam juzi, kuhusu kuwa wazalendo ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani nchini. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Taasisi hiyo Taifa, Andrew Kayombo na Mwenyekiti wa Mkoa huo, Pendo Emmanuel. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Uhamiaji wamnasa mtuhumiwa uhalifu wa kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIA kutoka nchini Iran, Hamidreza Mohammad Ab Raheh, mwenye hati ya kusafiria namba H46000576 amekamatwa na kurejeshwa nchini kwake jana kwa makosa ya kuishi kinyume na sheria na tuhuma za kupanga mipango ya uhalifu wa kimataifa kwa kushirikiana na wengine.

Akizungumza na wanahabari jana, Kamishna wa Uhamiaji, Usimamizi na Udhibiti wa Mipaka nchini, Samweli Mahirane, aliwaasa Watanzania kushiriki kikamilifu katika kulinda usalama wa nchi yao ikiwa pamoja na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika kutoa taarifa dhidi ya wahalifu.

Kamishna Mahirane, alizungumzia mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa nchini katika kutoa huduma bora kwa wageni, kukabiliana na wahalifu wa kitaifa na kimataifa, wahamiaji haramu na kipekee katika kushirikiana na Taasisi za kimataifa likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wahamiaji (IOM) kuwarejesha wahamiaji haramu makwao.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu, kumekuwa na ongezeko kubwa la wageni nchini.

Aidha, alisema jumla ya wageni 1,172,205 waliingia nchini kihalali kwa kufuata taratibu na sheria na wageni 983,183 waliondoka nchini.

Watanzania 220,423 walirudi nchini wakitokea nchi za nje na 250,540 walitoka nchini kuelekea mataifa mengine.

# Waziri ataka wadau kuunga mkono jitihada kukabili ukatili

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wanasheria nchini kuunga mkono juhudi za serikali kukabili unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Kiongozi huyo alitoa wito huo juzi jijini Dar es Salaam, katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyoandaliwa na wizara yake kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Ujerumani ya GIZ.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo wanafunzi kutoka chuo cha sheria, wasanii pamoja na wawakilishi kutoka asasi za kiraia.

Waziri Ndumbaro alisema ili kuishinda vita dhidi ya ukatili uliokithiri, wanasheria, serikali na wadau wa maendeleo hawana budi kuungana kuwa kitu kimoja kumaliza matukio hayo.

"Tuna siku 16 za kupinga ukatili ukiziangalia unaona ni chache sana, lakini ukizitumia vizuri ni nyingi sana katika kutoa elimu na kusaidia jamii kujiepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema na kuongeza:

"Safari hii ilianza 1991 kule nchini Marekani, wanawake wa viongozi wakubwa waliungana mpaka kufikia hii leo jumla ya nchi 187, zimeungana na katika nchi hizo Tanzania ni miongoni."

"Lengo la mradi huo ndio agenda ya hizi siku 16 za kupinga ukatili tunataka kutekeleza kwa miaka mitatu ijayo tutatoa mafunzo kwa wataalamu, asasi, polisi, TAKUKURU na muhimili wa mahakama, ili waweze kulitambua kwa kina tuweze kuwa kitu kimoja katika kupambana na janga hili," alisema Ndumbaro ambaye pia ni Mbunge wa Songea Mjini.

Alisema elimu itajikita zaidi katika kutambua viashiria vya ukatili wa kijinsia, kwa sababu wapo wengine wanafanya ukatili lakini hawajui.

Pia alisema kwa sasa wanaume nao wanafanyiwa ukatili na kwamba tafiti zinaonesha wanakufa mapema kuliko wanawake kwa sababu wapo wanaume wanaonyanyaswa na kukatiliwa.

"Lakini tunampango wa kuanzisha 'Online Registration' (kujiandikisha mtandaoni), ukifanya unyanyasaji tunakuweka kwenye mfumo kwa hiyo tutakuwa tunaangalia ukienda kuomba ajira kama uliwahi kufanya ukatili hupewi, ukienda benki kuomba mkopo unaangaliwa ukikutwa na hatia hupewi mkopo hii ndio maana halisi ya kutumia teknolojia kupambana na ukatili.

Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Khamisi, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuongeza nguvu kushwawishi, kuhamasisha na kuchukua hatua katika kukabiliana na ukatili huo.

Kaulimbiu ya mwaka huu inasema 'Kila uhai una thamani tokomeza mauaji na ukatili dhidi ya watoto' kwa hiyo serikali inaendelea na kampeni ya kupinga ukatili kupitia Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii SUMAUJATA.

"Wizara hii inaendelea kufanya mambo mengi katika kutokomeza vitendo vya ukatili ikiwamo kutekeza mpangokazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watototo," alisema na kuongeza:

"Kuongeza madawati ya jinsia kwenye vituo vya polisi, kuanzishwa kwa vituo vya mkono kwa mkono ambavyo vinatoa huduma, kuanzisha madawati 22 katika vyuo vya elimu ya juu."

Mwakilishi wa Wanafunzi wa Chuo cha Sheria, Hashimu Mashiku, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kupinga ukatili wa kijisia kwa kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wahanga.

SIKU YA USAFIRI WA ANGA DUNIANI 2022

# MAADHIMISHO YA SIKU YA USAFIRI WA ANGA DUNIANI 2022




*Wajumbe wa Baraza (TCAA CCC) walipotembelea Kiwanja cha Dodoma ili kubaini Changamoto mbalimbali wanazokutana nazo Watumiaji wa Usafiri wa Anga katika Kiwanja hicho.*




*Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) wakiwa katika moja ya Mikutano ya Wadau wa Sekta ya Usafiri wa Anga*

Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga huazimishwa kila Desemba 7, kwa lengo la kuelimisha na kuongeza ufahama juu ya umuhimu wa usafiri wa anga katika kukuza na kuchochea maendeleo katika nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN).

Kila baada ya miaka minne (4) Shirika la kimataifa la usafiri wa anga (ICAO) huratibu maadhimisho hayo na hutoa kauli mbiu inayobeba dhima ya maadhimisho hayo.

Kauli mbiu ya mwaka huu 2022 ni Kukuza Ubunifu kwa maendeleo ya Usafiri wa Anga Duniani (Advancing Innovation for Global Aviation Development). Kauli mbiu hii ni muendelezo wa kauli mbiu iliyotolewa mwaka 2019 katika maadhimisho ya miaka 75 ya Shirika la kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO).

Katika siku hii wadau wote wa usafiri wa anga hufanya tafakari ya kina juu utendaji wa sekta ya usafiri wa anga pamoja changamoto zake na kutafuta njia sahihi ya kukabiliana nazo. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) linaungana na wadau wa sekta ya usafiri wa anga duniani kote katika kuadhimisha siku hii muhimu.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga hutumia siku hii kupaza sauti zao kuzitaka mamlaka zinazodhibiti usafiri anga kuongeza udhibiti husani matumizi sahihi ya teknolojia na kuongeza ushindani kwa ajili kupata usafiri salama na bora.

Baraza ni kiungo muhimu kati ya watumiaji na wadau wengine katika sekta na hivyo tunatumia siku hii kuyataka mashirika mbalimbali ya usafiri wa anga kuboresha huduma za usafiri wa anga.

Katika siku hii tunapaza sauti ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kuhusu maslahi ya watumiaji pamoja na upatikanaji wa huduma bora, salama na nafuu kwa wakati.

Baraza linafanya kazi hii kupitia mfumo wa kiuthibiti kwa kujenga hoja mahususi wakati wa mijadala ya kiuthibiti hususani kupitia utungaji wa kanuni na taratibu za udhibiti wa soko la usafiri wa anga.

Majukumu ya Baraza ni pamoja Ushauri, Uwakilishi, Utetezi na Uelimishaji kwa watumiaji wa huduma za Usafiri wa Anga, juu ya haki, wajibu na maslahi yao.

Tunaendelea kupongeza juhudi za Serikali katika kuendeleza na kusimamia sekta ya Usafiri wa Anga nchini kwetu, sekta ambayo katika miaka ya karibuni imekua kwa kasi na kuchochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi katika Nchi yetu.

Katika mwaka wa fedha 2022/23 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya Shilingi milioni 86,102.522. Fedha hizo zitagharamia ujenzi, upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na maungio yake, maegesho ya ndege, majengo ya abiria, majengo ya kuongozea ndege, majengo ya uchunguzi wa hali ya hewa, barabara za kuingia viwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa katika Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mwanza, Arusha, Mtwara Sumbawanga, Shinyanga, Msalato, Bukoba

Hatua hizi zimeonesha dhamira ya dhati ya kuboresha viwanja vya ndege ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora za usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga.Katika kufanikisha hilo, ujenzi pamoja na uboreshaji wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali nchini umeendelea kutekelezwa.

Pamoja na ujenzi wa miundombinu, Serikali imeendelea kuhuisha mikataba ya kimataifa kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na teknolojia na jumuiya ya Kimataifa kwenye sekta ya usafiri wa anga.ili kufungua soko la usafiri wa anga kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuvutia mashirika mengine kutoa huduma nchini na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

Serikali imeingia mikataba mipya ya usafiri wa Anga (BASA) kati yake na nchi za Cape Verde na Ugiriki. Aidha, BASA kati ya Tanzania na nchi za Oman, Uingereza, DRC, Nigeria, Qatar, Rwanda na Kenya imepitiwa upya.

Pamoja na mafanikio hayo, sekta hii bado inachangamoto nyingi hapa nchini. Baraza kwa kushirikiana na wadau wengine tumeendelea kushughulikia ucheleweshwaji wa safari za abiria na mizigo, changamoto ambayo imeongezeka kujitokeza katika kipindi cha hivi karibuni.

Aidha, tumebaini kuongezeka kwa mahitaji ya huduma ya usafiri wa anga inayotokana na kukua kwa uchumi na kipato cha Watanzania. Katika kipindi kinachoishia Julai 2021 watumiaji wa huduma ya usafiri wa anga waliongezeka kwa asilimia 73 kutoka watumiaji 2,964,471 mwaka 2020/21 hadi watumiaji 5,112,742 mwaka 2021/22.

Ni mapendezo ya Baraza kwa mamlaka zote kujenga na kuendesha sekta hii kwa misingi ya uchumi wa soko iliyojengwa kwenye misingi thabiti ya ushindani kwa watoa huduma na Mamlaka husika ili watumiaji wapate huduma bora kwa bei nafuu

Sambamba na hilo, Baraza linapendekeza kuendelea na uboreshwaji wa viwanja vya ndege nchini ikiwa ni pamoja na kufunga taa za kuruka na kutua ndege, minara ya kuongoza ndege kwa lengo la kuongeza usalama na matumizi sahihi ya viwanja hivyo. Hii iendane na juhudi za kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje kwenye sekta hii muhimu kwa ajili ya kuongeza huduma na fursa nyingi kwa vijana katika sekta hii muhimu sana.

Siku ya kimataifa ya usafiri wa anga ni nguzo muhimu kwa sekta ya usafiri wa anga kwa huwaleta pamoja wadau wa sekta ya usafiri wa anga kwa lengo la kujadili mafanikio na changamoto za usafiri wa anga. Siku hii hutumika kuwaelimisha wadau wa sekta hasa watumiaji ambao huitumia kutoa taarifa sahihi kwa umma juu mambo yanayowahusu watumiaji duniani kote.



*Katibu Mtendaji wa Baraza Bw. Innocent Kyara akipeana mkono na Dr. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu (Uchukuzi) wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi alipomtembelea Ofisini kwake Mji wa Serikali, Dodoma*




**Imetolewa na,**
**Katibu Mtendaji,**
**Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA CCC),**
**Jengo la TBA Na. L1, Kiwanja Na. 6/2,**
**Kinondoni, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,**
**S. L. P 12242,**
**14110 DAR ES SALAAM.**
**07/12/2022**

217179802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watu wenye ulemavu wasigeuzwe vitega uchumi

**KUIBUKA** kwa wimbi la watu wenye ulemavu wanaoomba mitaani kunaleta taswira mbaya kwa nchi pia kuna hatarisha maisha ya watu hao.

Wageni wanapoingia nchini na kukuta kundi kubwa la watu wenye ulemavu likiomba mitaani, wanaweza kufikiri jamii inayoishi nayo haiwajali.

Lakini kwa mujibu wa utafiti wa kihabari imegundulika kuwapo kwa watu wanaowatumia ndugu hao wenye ulemavu kama kitega uchumi chao cha kujipatia kipato.

Uchunguzi wa kihabari ulibaini kuwapo kwa watu wanaowahifadhi watu hao wenye ulemavu kwenye vyumba walivyo vipangisha na kisha kuwafanyisha kazi ya kuombaomba mitaani kwa mkataba wa malipo waliyokubaliana.

Kwa wanaofanya biashara hiyo, imegundulika kuwa mtu mwenye ulemavu anayesukumwa kwenye baiskeli, hupewa mtu wa kumsindikiza kwa ajili ya kumsukuma mitaani kuomba pesa na tajiri aliyewahifadhi hupanga kiwango cha kati ya Sh. 3,000 mpaka 5,000 kwa siku kutoka kwa kila mtu aliyemuhifadhi.

Kiwango hicho hupewa bosi huyo na pesa nyingine itakayopatikana ya ziada hugawana anayefanyakazi ya kumsukuma na mwenye ulemavu, huo ndio ujira wao.

Watu hao hushinda kwenye jua kutwa nzima na inakuwa kipindi cha mvua pia hupata adha ya kuloa kwa lengo la kufikisha kiwango walichopangiwa na bosi wao aliyewahifadhi.

Vitendo hivi vya kuwageuza watu wenye ulemavu kama vitega uchumi vimeenea maeneo mengi nchini na kwa hakika hali hii isipokemewa itaitia doa nchi.

Katika kupinga vitendo hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Josephath Maganga, amezitaka jamii zinazoishi na watu wenye ulemavu kuacha tabia ya kuwatumia kama vitega uchumi kwa kuwaweka barabarani kwa ajili ya kuomba misaada.

Alikemea tabia hiyo na kusema inawadhalilisha na kuwaondolea utu wao huku akiitaka jamii kuwajibika kwa kuwasaidia kiuchumi, kimaisha na kuwalinda muda wote.

Watu wenye ulemavu wanatakiwa kusaidiwa kiuchumi na kijamii badala ya kuwafanya kitega uchumi kwa kuwaweka barabarani kuomba katika maeneo mbalimbali.

Tabia hiyo kwa kweli inawadhalilisha utu wao kwa kuwafanya kama hawastahili mbele ya jamii na kuwaagiza tabia hiyo iachwe ya kuwafanya vitega uchumi kwa kuwaweka juani kutwa nzima ili wapewe misaada kutoka kwa wapita njia.

Kadhalika, aliwataka watu wenye ulemavu kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri zote nchini ili kujisimamia wenyewe kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi. Aliwakumbusha kuwa mikopo hiyo ipo kwa ajili yao kinachotakiwa ni kuunda vikundi pamoja na kutimiza vigezo vya kuwawezesha kupata ili wajiendeleza na kutatua kero zao.


Hata hivyo, Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Mkoa wa Dodoma, Justast Ng'antalima, aliiomba serikali kuwapunguzia makali kwenye mikopo inayotolewa na halmashauri nchini.

Walilalamika kuwa bado kwa upande wao kuna ugumu wa kupata mikopo hiyo ya asilimia 10, kutokana na serikali kuwawekea vigezo vinavyosababisha kutopata kwa haraka kama ilivyo kwa makundi mengine ya wanawake na vijana.

"Kwa wenzetu mikopo hiyo wanaipata kwa urahisi zaidi, ila kwetu sisi watu wenye ulemavu bado kuna changamoto nyingi ambazo zinazotukwamisha kuipata mikopo hiyo kwa haraka kama ilivyo kwa wanawake na vijana."

Bila shaka kilio hicho cha watu wenye ulemavu katika kupata mikopo kitasikika ili nao waweze kuondokana na adha ya kutumiwa kama vitegauchumi vya watu wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Chonde fedha miaka 61 ya Uhuru zisichakachuliwe

**MAADHIMISHO** ya miaka 61 ya Uhuru, yanafikia kilele chake kesho kutwa Desemba 9, siku ambayo Tanganyika ilipata Uhuru kutoka kwa mkoloni Mwingereza.

Kwa kawaida Desemba 9 huwa kuna shughuli mbalimbali ikiwamo ya maonyesho yanayoelezea mafanikio ambayo nchi imepata tangu uhuru hadi sasa.

Aidha, kunakuwa na shamrashamra nyingi zikiambatana na gwaride rasmi, safari za viongozi mbalimbali kutoka mikoani, wilayani lakini Rais akiwaalika wakuu wengine wa nchi kujumuika kusherehekea au kuadhimisha mafanikio ya taifa huru.

Hata hivyo, kwa mara ya kwanza mwaka 2015 akiwa Rais John Magufuli, aliagiza kusiwe na sherehe badala yake maadhimisho yatumike kufanya usafi kitaifa na fedha zitumike kujenga kipande cha barabara kati ya Morocco na Mwenge jijini Dar es Salaam.

Kadhalika mwaka huu sherehe hizo hazitakuwapo, badala yake, Rais Samia Suluhu Hassan, anaelekeza fedha za kugharamia sherehe hizo Shilingi milioni 960 zitumiwe kujenga mabweni kwenye shule nane za msingi wanakosoma watoto wenye mahitaji maalumu.

Shilingi milioni 960, zilizotengwa na wizara na taasisi, sasa zinapelekwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika shule nane za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Ninaunga mkono uamuzi huo wa Rais, kwani zinaweza kupunguza vikwazo ambazo wanafunzi wamekuwa wakikumbana navyo kutokana na kuwa na uhitaji maalumu.

Kwa mfano, wapo baadhi yao ambao wamekuwa wakipanga nyumba uraiani na hawana mwangalizi, kitendo hicho kinaweza kuwaingiza katika matatizo na kujikuta wakikatishwa ndoto zao katika elimu.

Wanafunzi wa kiume kupanga vyumba uraiani, wanaweza kujiingiza katika makundi ya kihuni, lakini kwa wasichana wanaweza kujikuta wamejiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi na kupata mimba licha ya kuwa na uhitaji.

Lakini wakipata mabweni, wanakuwa na watu wa kuwalinda, hivyo uamuzi alioufanya Rais, unapaswa kuungwa mkono na kuheshimiwa, ili ulete matokeo chanya.

Pamoja na hayo, viongozi wenye dhamana ya kusimamia fedha hizo, ni vyema wakahakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa bila kuwapo uchakachuaji wa aina yoyote.

Ninagusia hilo, kwa sababu kumekuwapo na malalamiko kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule kama madarasa, vyoo na milango

Wapo baadhi ya viongozi ambao hudaiwa kupaua majengo hayo kwa mabanzi, kuweka sakafu chini ya kiwango ili mradi nao wapate cha juu.

Ninaamini kwamba, kile ambacho Rais amekikusudia katika fedha hizo kinaweza kutimia iwapo watakaokabidhiwa fedha watakuwa waaminifu na waadilifu na wenye hofu ya Mungu.

Hivyo, wakati huu ambao maadhimisho yanafanyika kwa njia mbalimbali ikiwamo midahalo, makongamano mbalimbali, ni muhimu kuwakumbusha watakaokabidhiwa fedha hizo, kwamba wasizisimamie ili zitumike kwa usahihi bila kuwapo uchakachuaji mahitaji maalum.

Ikumbukwe kuwa uchakachuaji unachangia kukwamisha maendeleo, hivyo ni muhimu mabweni yatakayojengwa yalingane na thamani ya fedha iliyotumika, ili kile ambacho Rais amekikusudia hadi kuahirisha sherehe kionekane.

Rais ameonyesha nia ya kuhakikisha nchi inapiga hatua za kimaendeleo kupitia nyanja zote, hivyo njia mojawapo ya kumuunga mkono katika hilo, ni watendaji kusimamia fedha umma zisitumike vibaya.

Ninachoamini ni kwamba, serikali imedhamiria kuimarisha uchumi hasa ule ambao unajikita katika maendeleo ya watu, inavyoelekeza fedha zipelekwe mahali fulani, inakusudia zitumike kulingana na malengo bila kuwapo kwa ujanja wa aina yoyote.

Kwa usimamizi imara wa fedha za umma, ni wazi kutakuwa na mabadiliko katika sekta zote za kiuchumi na kijamii na hivyo kufikia maendeleo yaliyokusudiwa.

# Wanafunzi vyuo vikuu kupatiwa salio la simu kila mwezi

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa vyuo vikuu sasa watapatiwa salio la Sh. 1,500 kila mwezi kwa wanaotumia laini za simu za Halotel ili waweze kujifunza kupitia mtandao.

Kampuni ya simu za mkononi ya Halotel, imetangaza huduma hiyo inayolenga kuchochea usomaji kwa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia mitandao.

"Tungependa kuwa sehemu ya maendeleo ya sekta hii muhimu. Tunaelewa kuwa elimu huwezesha watu kuendeleza vipaji vyao na kuwa watu wenye mafanikio katika jamii," alisema Mkurugenzi wa Biashara Halotel, Abdallah Salum.

"Kwa kuchangia sekta hii kupitia mradi wa maendeleo ya kijamii, tunaamini kuwa tutasaidia kupunguza hali ya kutokuwapo kwa usawa na hivyo kufanya maendeleo jumuishi ya rasilimali watu kwa kuwawezesha wanafunzi kupata na kufurahi fursa wezeshi na zenye tija kidijitali katika masomo na maisha kwa ujumla."

Alisema kuwa huduma hiyo ni endelevu kwa vile kampuni inalenga kukuza na kusaidia wanafunzi wote wa elimu ya juu kwa kuwapa salio hilo kuanzia wanapoanza masomo chuoni hadi watakapomaliza. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2022 kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), kwa makadirio kwa sasa kuna jumla ya wanafunzi 900,000 katika taasisi za elimu ya juu nchini.

Jumla ya vyuo vikuu vipatavyo 280 na zaidi vimejumuishwa katika programu hiyo ya Halotel. Pia, kampuni imepanga kuandaa tamasha kubwa Desemba 10, mwaka huu.

"Kuhakikisha kuwa wanafunzi wa vyuo wanafaidi huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia Halopesa, Halotel kupitia HaloPesa inaanzisha kampeni ya kutuma na kupokea pesa bila tozo za serikali kwa wateja wake ambao ni wanafunzi wa vyuo vikuu. Huduma hii itapatikana kupitia laini za mwananchuo za Halotel maalumu kwa wanafunzi ziitwazo 'Edu SIMs'," alisema Ofisa Masoko wa Halopesa, Roxana Kadio.

Alisema kampeni hiyo itaendeshwa kwa miezi sita kuanzia Desemba, kwa wanafunzi wa vyuo wanaotumia huduma ya HaloPesa kufanya miamala yenye thamani isiyozidi Sh. 30,000. Kila mwanafunzi wa chuo atakayekuwa mteja wa HaloPesa atapata promosheni hiyo kwa kufanya miamala yoyote ya Halopesa.

Hivi karibuni Speedtest Global Index ilitoa ripoti yake na kuonesha kuwa kampuni hiyo imeongoza kwa kuwa na mtandao wenye kasi zaidi katika kipindi cha robo tatu zote kwa mwaka huu zilizoishia mwezi Septemba.

Ripoti hiyo inaonesha kuwa kwa mwezi Septemba Halotel imeongoza kwa kuwa na intaneti yenye kasi ya 17.63.

**Ripoti hiyo inaonesha kuwa kwa mwezi Septemba Halotel imeongoza kwa kuwa na intaneti yenye kasi ya 17.63.**




Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum (katikati), akiongea na waandishi wa habari kuhusu huduma ya kuwapatia wanachuo salio. Kulia ni Meneja Masoko, Sakina Makabu na Ofisa Masoko, Roxana Kadio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi 39 uchumi wa buluu yasajiliwa ZIPA

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MIRADI 39 inayohusu uchumi wa buluu imesajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji Vitega Uchumi (ZIPA) katika miaka miwili ya kwanza ya awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Huduma Mamlaka ya Vitenga Uchumi Zanzibar (ZIPA) Shida Makame, alisema kati ya hiyo, miradi ya hoteli ni 30 yenye mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 213.16, kilimo na uvuvi miradi tisa (Dola milioni 18.26) pamoja na uwekezaji kwenye visiwa 17 Unguja na Pemba (Dola milioni 414.50).

Alisema Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kupata uwekezaji katika visiwa saba, akivitaja pamoja na viwango vya mtaji kwenye mabano kwa thamani ya Dola za Kimarekani kuwa ni kisiwa cha Bawe (Dola 30,000,000), Changuu (26,000,000), Kibandiko/Snake (10,000,000) na Kwale (68,000,000).

Visiwa vingine katika mkoa huo ni Pamunda 'A' (15,000,000), Pamunda 'B' (15,000,000) pamoja na Chapwani (20,000,000).

Mkoa wa Kusini Pemba unafuatia kwa kupata uwekezaji katika visiwa vitano ambavyo ni Misali (Dola 83,000,000), Mtangani (15,000,000), Kwata (15,000,000), Kashani (8,000,000) na Matumbini (15,000,000).

Shida alisema hadi sasa visiwa vitatu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja vimepata uwekezaji ambavyo ni Miwi (Dola 25,000,000), Niamembe (7,000,000) na Mnemba (17,000,000).

Visiwa vingine ni Pungume, Mkoa wa Kusini Unguja (Dola 10,500,000) pamoja na Njao Kaskazini Pemba ambacho mtaji wa uwekezaji wake ni Dola za Kimarekani 15,000,000.

Naye Halima Wagao, Mkurugenzi Uhamasishaji, Uenezi na Masoko mamlaka hiyo alisema wawekezaji waliojitokeza kuendesha miradi katika visiwa hivyo, wanaendelea na maandalizi ikiwamo kusafisha maeneo na kukamilisha michoro kabla ya ujenzi kuanza kufanyika mwakani.

Alisema serikali iko makini kuhakikisha ujenzi katika visiwa hivyo unazingatia uhifadhi wa mazingira ili kuibakisha Zanzibar na uoto asili ambao pia ni miongoni mwa vivutio vya watalii.

"Kwa sababu hiyo, mchakato wa ukodishwaji wa visiwa hivyo umeshirikisha pia Mamlaka ya Mazingira ambao ni miongoni mwa wadau wakubwa wa miradi ya uwekezaji nchini na tumewaelekeza wawekezaji juu ya umuhimu wa jambo hilo," alieleza Wagao.

Wagao alisema ZIPA kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali, inasimamia uimarishaji miundombinu katika eneo la uwekezaji Micheweni ikiwamo ujenzi wa barabara na kufikisha huduma za maji na umeme.

Alisema lengo ni kuhakikisha wawekezaji wanapojitokeza katika maeneo hayo, huduma hizo ziwe tayari ili kurahisisha shughuli zao zinazotarajiwa kusaidia kukuza uchumi kwa kuongeza pato la serikali.

Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Hassan Mbamba, ambaye pamoja na maendeleo yaliyopatikana, alisema changamoto kadhaa ziliathiri sekta ya utalii katika kipindi cha miaka miwili iliyopita ikiwamo UVIKO-19.

Hata hivyo, alisema hali kwa sasa ni nzuri, mwaka 2021 wageni 394,185 walifika nchini, na kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu tayari watalii 322,748 wametua, akieleza matumaini yake ifikapo mwisho wa mwaka idadi itaongezeka maradufu.

Mbamba alisema lengo la Kamisheni ni kupokea wageni 800,000 ifikapo mwaka 2025, hasa watalii wa hadhi ya juu kwa kubuni matukio mbalimbali kama vile matamasha na kukuza utalii wa michezo mbalimbali kwa kushirikiana na wizara husika.

Katika azma ya kukuza utalii wa michezo, Mbamba alisema Kamisheni kwa kushirikiana na Shirikisho la Utalii Tanzania (TTB), wamefungua banda la maonesho nchini Qatar kutangaza vivutio vya Tanzania.

Mpango mwingine alisema, ni kushajiisha utalii wa mikutano kwa kujenga kumbi kubwa za kisasa zinazoweza kuchukua watu wengi hata zaidi ya 1000, utalii wa tamaduni za asili badala ya kutegemea fukwe pekee ambazo watalii wamezizoea na hawavutiki kurudi tena.

Zanzibar imeanza kufunguka kiuchumi kutokana na kujitokeza miradi mingi kwa muda mfupi tangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuanzisha mapango wa uchumi wa buluu kwa kuongeza uzalishaji kupitia rasilimali za baharini kama nishati, uvuvi, kilimo cha mwani na utalii.

## KABWELA



# Jela miaka 15 mauaji ya bodaboda

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Mtanga, Nachingwea mkoani Lindi, Saidi Afia, maarufu Shomboro (20) na Hussein Juma (22), wamehukumiwa kifungo cha miaka 15 jela kila mmoja baada ya kukutwa na hatia ya kumuua dereva wa pikipiki, Hussein Athumani Juma.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, Dk. Eliamini Laitaika, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na wenyewe kukiri kosa hilo bila ya kulazimishwa.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Wakili Happiness Sabatho aliyekuwa anawatetea washtakiwa, aliiomba Mahakama kuwapa wateja wake adhabu iliyo nafuu kwa madai wamekaa mahabusu kwa muda mrefu, hivyo wanajutia makosa waliyoyafanya.

Kutokana na utetezi huo, wanasheria wa serikali, Yahya Gumbo na Godfrey Mramba, walipoulizwa kama wana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa, walidai kuwa hawana.

Hata hivyo, waliiomba mahakama kuwapa adhabu kali ili iwe fundisho kwao na wengine wenye tabia ya kutumia nguvu kunyang'anya mali za wengine.

"Mheshimiwa Jaji hatuna kumbukumbu zao lakini tunaiomba mahakama yako tukufu kuwapa adhabu kali kwani vitendo vya unyang'anyi vimekuwa vinaendelea kushamiri ndani ya mkoa wetu," alidai Gumbo.

Jaji Dk. Laitaika akitoa hukumu kupitia vifungu 195 na 198 kama vilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, alisema amesikiliza maombi ya pande zote, hivyo akawahukumu washtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 15 jela kila mmoja.

Awali, ilidaiwa mahakamani na wanasheria wa serikali, Gumbo na Mramba kwamba washtakiwa wote walifanya kosa hilo Julai 19, 2018, baada ya kumkodi kwa madai ya kuwapeleka machimbo.

Walidai kuwa wakiwa wanaendelea na safari, walipofika eneo la Mto Mbwemkulu, walimsimamisha na ndipo wakamuua na kumnyang'anya pikipiki yake na kuondokana nayo huku mwili wakiutelekeza eneo hilo.

Gumbo alidai mwili wa mwendesha pikipiki huyo ulikutwa Julai 20, 2018 na watu waliokuwa wanapita eneo hilo huku ukiwa na majeraha ikiwa ni pamoja na kukatwa sikio la kulia na kuondolewa jicho la kulia pia.

Washtakiwa hao walikamatwa Mangaka, Wilaya ya Nanyumbu wakiwa wanafungua vifaa vya pikipiki hiyo aina ya SanLG yenye namba za usajili T.657 CXD na kuingiza ndani ya nyumba waliyokuwa wanaishi tayari kwa ajili ya kuuza kimoja kimoja.




Mkuu wa Rasilimali Watu Idara ya Kilimo wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Cleopatra Nasari (wa pili kushoto), akiwa na wafanyakazi wenzake wakishirikia tuzo pamoja na vyeti kikiwamo cha shukrani kwa kampuni hiyo, kudhamini hafla ya Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), baada ya kukabidhiwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (hayupo pichani), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ARU yapokea bil. 67/- kwa upanuzi

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Ardhi (ARU), kimepokea Sh. bilioni 67.7 kupitia mradi wa upanuzi wa vyuo vikuu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ujulikanao kama Higher Education for Economic Transformation (HEET).

Makamu Mkuu wa ARU, Prof. Evaristo Liwa, alisema hayo kwenye mahafali ya 16 ya chuo hicho yaliyofanyika kwenye viwanja vya chuo hicho, Mlimani mkoani Dar es Salaam.

Kwenye mahafali hayo, wahitimu 943 walitunukiwa Shahada, Shahada za Uzamili na Shahada za Uzamivu (Ph.D) na Mkuu wa chuo hicho, Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande.

Miongoni mwao, wanafunzi 883 walitunukiwa shahada za awali, 52 shahada za uzamili, sita shahada za uzamivu (PhD) na wawili stashahada.

Prof. Liwa alisema mradi huo ni mkubwa kuwahi kutokea chuoni hapo kwa kuwa unabadilisha ukubwa wa miundombinu ya kufundishia na zana mbalimbali za kufundishia ikiwamo mitaala mipya.

Prof. Liwa alisema kwenye mradi huo chuo kimejikita kwenye utekelezaji wa maeneo nane ikiwamo ujenzi wa miundombinu mipya ya chuo na ujenzi wa kampasi mpya ya mkoani Mwanza.

Alisema wameshapata hati miliki ya eneo lenye ukubwa wa ekari 378, utayarishaji wa mpango kabambe wa eneo na michoro ya ujenzi na kwa michoro ya kampasi ya Dar es Salaam michoro ya majengo makubwa manne imekamilika na vibali vya ujenzi vimeshapatikana.

Alisema ujenzi wa kampasi ya Dar es Salaam umepangwa kuanza Machi, mwakani baada ya kukamilika kwa taratibu za kupatikana mshauri mwelekezi na mkandarasi.

"Kama kazi hizi zitatekelezwa kulingana na mpango kazi wetu, kazi hii inatarajiwa kukamilika mwaka 2024 kama inavyofahamika chuo chetu ndicho pekee kilichobobea kwenye masuala ya ujenzi, hivyo wataalamu wetu wa ndani wametusaidia katika uandaaji wa nyaraka na michoro ya ujeni," alisema Prof. Liwa.

Alisema kwa mwaka wa masomo 2022/23 chuo kimedahili wanafunzi 2,035 kwa shahada za awali na wanafunzi 86 kwa shahada za uzamili ambao ni ongezeko la asilimia 1.3 kulinganisha na mwaka wa masomo uliopita.

Ongezeko hilo, alisema si kubwa kulinganisha na malengo ya chuo ambalo ni kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,657 wa sasa hadi 11,000 mwaka 2029.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Balozi Salome Sijaona, alisema chuo kimeendelea kutekeleza majukumu yake katika kuleta dhima ya maendeleo si tu kwa chuo hicho bali kwa taifa kwa ujumla.

Alisema kwa kuzingatia sera na miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali baraza la chuo limeendelea kusimamia na kutoa maamuzi ya kuendeleza chuo hicho.

"Napenda nikuhakikishie mkuu wa chuo kuwa ARU imejiwekea misingi bora ya utekelezaji wa majukumu yake ili kuleta mafanikio yanayokusudiwa nampongeza Makamu Mkuu wa chuo kwa kazi kubwa na ni matarajio kuwa miaka michache ijayo ARU itakuwa moja ya vyuo vikuu bora si tu kwa Tanzania bali Afrika Mashariki," alisema.

Balozi Sijaona alisema usimamizi mzuri wa Makamu Mkuu wa chuo hicho umesababisha kiwe na matokeo mazuri na ya haraka ya mipango ya maendeleo na kuongeza kuwa ni matarajio kasi hiyo itaongezeka ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa chuo hicho.

## DC ataka hatua uharibifu vyanzo vya maji

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, ameagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya watu wanaoharibu vyanzo vya maji wilayani hapa kwa kufanya shughuli mbalimbali za kibidamu zikiwamo kilimo na ufugaji.

Kitta alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye chanzo cha maji cha Mbwinji kinachosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea (MANAWASA). Mkuu huyo wa wilaya aliongozana na kamati ya ulinzi na usalama, wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali na zisizo na kiserikali.

Viongozi hao walifika kwenye chanzo hicho kwa ajili ya kufanya shughuli za kijamii ikiwamo kupanda zaidi ya miti 800 ikiwa kuelekea maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru.

Alisema miti hiyo ambayo imepandwa itasaidia kutunza chanzo hicho lakini pia jamii ishirikiane na mamlaka husika katika kutunza kwa kuondoa shughuli za kibinadamu zinazoendeshwa kwenye mto huo ambazo sehemu kubwa ni kilimo.

Kitta alisema kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kutambua umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhudumia wananchi kwa miaka mingi zaidi, hivyo wanapojitokeza baadhi ya watu kuviharibu sababu ya msingi, lazima serikali iwachukulie hatua.

Kwa mujibu wa Kitta, chanzo cha maji cha Mto Mbwinji ni muhimu na inapaswa kitunzwe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu kinahudumia wilaya za Masasi, Nachingwea na Ruangwa.

Alisema serikali ya wilaya ya Masasi inaendelea kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha chanzo cha Mbwinji na vyanzo vingine vyote vinalindwa kwa kudhibiti shughuli za kibinadamu zinazoendelea kufanyika kwenye vyanzo vya maji.

Baadhi ya shughuli za kibinadamu ambazo zimeonekana kushika kasi kwenye maeneo ya hayo ya vyanzo vya maji kikiwamo cha Mwinji ni kilimo cha korosho, mahindi, mboga na uchomaji mkaa. Mkuu huyo wa wilaya aliagiza kwamba kuanzia sasa shughuli hizo zisitishwe mara moja.

Kaimu Meneja wa MANAWASA, Mhandisi Asajile Ngoloke, alisema katika kuhakikisha chanzo hicho kinalindwa, mamlaka inafanya kazi na jumuiya za maji katika kutoa elimu ya kukitunza.

**HABARI KITAIFA**

# Waomba huduma zaidi za kibingwa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WANANCHI wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wameiomba serikali kuangalia mahitaji ya tiba kwa wananchi na kuongeza upatikanaji wa huduma za madaktari bingwa kuwafikia walau mara mbili kwa mwezi.

Wametoa ombi hilo walipojitokeza kupima afya katika kambi ya siku tano ya madaktari bingwa iliyoanza juzi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sekou Toure.

Kambi hiyo imewekwa kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali za kiafya zikiwamo msukumo wa damu, kisukari, saratani, selimundu na huduma za watoto.

"Suala hili lipewe kipaumbele kikubwa maana litawasaidia wananchi ambao wengi wao wamekuwa wakikumbwa na maradhi makubwa kutokana na kukosa fedha za kwenda kupima, hivyo wanajikuta wanakufa. Lakini zikiwapo kambi za mara kwa mara, watu wengi watajitokeza na wataokolewa na magonjwa yanayoweza kutibika," alisema Mushi John.

Daktari bingwa wa magonjwa ya damu, Gloria Mapunda, aliwataka wananchi ambao wanataka kufunga ndoa wapime kwanza ili kuona kama wana vinasaba vya selimundu ili kusaidia kupunguza kuzaa watoto walio na matatizo hayo.

"Ninawaomba wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, wajitokeze kuja kupima afya zao katika kambi hii. Vipimo vipo na ukingundulika una vinasaba vya selimundu tunakupatia matibabu. Dawa za kupunguza makali kwa mgonjwa awe mtoto au mtu mzima zipo," alisema Dk. Mapunda.

Akizungumza katika uzinduzi wa kambi hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, alisema wananchi wa Mwanza na mikoa jirani wajitokeze kutumia fursa hiyo ya kupima na kujua afya zao ili kusaidia kupunguza shida za maradhi katika miili yao.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Sekou Tuore, Dk. Bahati Msaki, ambaye ni daktari bingwa wa mangonjwa ya watoto, alisema madaktari bingwa walioko wanatoka katika hospitali za Bugando na Sekou Toure.

# Gwajima ageuka mbogo madarasa ushoga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorthy Gwajima, amekemea vitendo vya baadhi ya watu kuanzisha madarasa ya ushoga kwa wanafunzi.

Alisema hayo juzi katika ziara yake mkoani Shinyanga wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Town, Manispaa ya Shinyanga, ikiwa sehemu ya kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Dk. Gwajima alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi kusomea na kutimiza ndoto zao na si kuanza kutumika kufundishia masuala ya ushoga kwa wanafunzi na kuwaharibu watoto, huku akikemea vitendo hivyo na kutaka visiendelee kutokea tena nchini.

**Huko mkoani Geita kuna mtu amekamatwa akifundisha watoto ushoga na yeye amekiri yuko hivyo tena amevaa na sidiria.**

"Huko mkoani Geita kuna mtu amekamatwa akifundisha watoto ushoga na yeye amekiri yuko hivyo tena amevaa na sidiria. Huyu naagiza uchunguzi ufanyike haraka sana ili hatua zaidi zichukuliwe na madarasa ya namna hii yafungwe kabisa," alisema Dk. Gwajima.

Aidha, alisema ulinzi kwa watoto hauepukiki, kuwafundisha tabia mbaya haiwezekani, na watoto wana fursa ya kulindwa na kukua katika maadili mema. Aliwataka viongozi wa mkoani Shinyanga wawe pia makini ili mtu huyo kutoka Geita asije akahamishia darasa la ushoga mkoani hapa.

"Tutawalinda watoto wetu sababu wanahaki ya kuishi, kupata elimu, ya kuwa na maadili mema na waje wachague njia yao wenyewe wasije wakatuharibikia mikononi mwetu wakasema hatukuwalinda. Sisi tutawalinda na hayo madarasa ya ushoga yafie huko huko,"aliongeza.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Prof. Siza Tumbo, alisema maagizo yote ambayo yametolewa na waziri watayazingatia pamoja na kudhibiti madarasa ya ushoga ili yasiwapo mkoani hapa kama ilivyotokea Geita.

Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Taifa, Nancy Kasebo, aliishukuru serikali kuendelea kupambana na matukio ya ukatili dhidi ya watoto ili wapate nafasi ya kusoma na kutimiza ndoto zao na kuja kuwa viongozi wa baadaye katika taifa.




Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta (wa tatu kushoto), akikabidhi zawadi ya pikipiki ya mataili matatu kwa mmoja wa wakulima wa korosho, Edwin Jackob, kutoka Chamali Amcos, wilayani humo mwishoni mwa wiki, ambaye ni mmoja wa washindi wa droo ya pili ya kampeni ya Vuna Zaidi na NBC Shambani inayoendeshwa na Benki ya NBC kwa wakulima wa korosho wa mikoa ya Lindi na Mtwara. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Mariamu Chaurembo (kulia), Mkuu wa Kitengo cha Mikakati cha Benki hiyo, Msafiri Shayo (wa pili kushoto) na baadhi ya maofisa wa benki hiyo. . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi wapewa mbinu kukabili ukatili kijinsia

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

WAZAZI na walezi Masasi mkoani Mtwara wamehimizwa kuwa na utaratibu wa kuzungumza kwa ukaribu na kuwakagua watoto kila wanaporudi nyumbani kutoka kucheza au shuleni ili kufahamu kama hawajafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kuingiliwa na watu ambao wamekosa uadilifu dhidi ya watoto.

Wito huo ulitolewa juzi wilayani hapo na Katibu wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Masasi, Pius Amuri, alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi wa watoto wa wanafunzi waliokuwa wakihitimu masomo ya awali katika kituo cha kulelea watoto cha Mamu Day Care Center.

Alisema hivi sasa dunia imejaa mambo ya ajabu na yanayostaajabisha, hivyo ni wakati muhimu kwa wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao hasa katika kuwatunza kwa sababu kumekuwa na kesi au matukio mengi ya watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Amuri alisema matukio ya watoto hasa wa kike kuingiliwa na kuharibiwa sehemu zao za siri yamekuwa yakitokea mara kwa mara na wazazi na walezi wanagundua baadaye wakati mtoto ameshapata madhara makubwa, hivyo kusababisha kuathirika kisaikolojia.

Kutokana na hali hiyo, alisema wazazi na walezi wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kuwakagua au kufanya nao mahojiano ili kujua mienendo yao ya kila siku jambo ambalo itasaidia kufahamu mapema kama wanafanyiwa ukatili wa kijinsia na kuchukua hatua mapema dhidi ya wahusika.

Alisema jumuiya hiyo kwa siku za hivi karibuni imekuwa ikipata taarifa mbalimbali zinazohusu baadhi ya watoto kuanzia umri wa miaka tano hadi 12 kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kuingiliwa na baadhi yao vitendo hivyo ufanyiwa na watu wa karibu kutoka kwenye familia zao.

Kwa mujibu wa Amuri, iwapo mzazi atakuwa mstari wa mbele kupinga vitendo vya kikatili ikiwamo kuviibua kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika ili wahusika wachukuliwa hatua kwa kufikishwa mahakamani, itasaidia kukomesha vitendo hivyo.

Fatuma Bakari, mzazi na mkazi wa Mtaa wa Kisiwani wilayani Masasi, aliiomba serikali iendelee kuweka mkazo katika kutafuta suluhisho la kudumu kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na wahusika kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

# Kampuni yasaidia Muhimbili vifaa mil. 50/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Letshego Holdings imesaidia vifaa tiba kwa kitengo cha wagonjwa watoto wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili vyenye thamani ya Sh. milioni 50.

Vifaa tiba vilivyokabidhiwa kwa kitengo hicho ni vifaa sita vya kusimamia mwenendo wa moyo (cardiatric monitor), mashine 20 za kidigitali za kupima shinikizo la damu, vifaa 18 vya kupima uzito, na vipima joto 10 au 'Ifra-Red thermometer'.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa na Mwenyekiti wa Letshego Holdings Limited, Philip Odera, ambaye alisema sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kushiriki katika masuala ya kijamii.

Odera alisema wanajisikia fahari kubwa kusaidia sekta ya afya na hasa kitengo hicho muhimu cha wagonjwa watoto huku akisisitiza kuwa suala la afya ni jambo muhimu sana kwa jamii kwani ndiyo chanzo cha kufanya shughuli yoyote.

**Ni msaada mkubwa na unahitaji pongezi kubwa pia. Tuna uhitaji wa vifaa hivi kwani ni muhimu kwa tiba nyingi. Naipongeza Letshego Holding kwa kusaidia na tunawaomba waendelee kutusaidia.**

Alisema shughuli zote za taasisi hiyo ni kusaidia kuboresha maisha ya watu, hivyo kusaidia kitengo cha tiba kwa watoto ni moja ya njia ya kutekeleza jukumu lao.

Alifafanua kuwa maana kubwa ya neno Letshego kwa lugha ya Setwana kutoka nchi ya Botswana ni msaada, jambo ambalo limewalazimu kutimiza wajibu wetu kwa jamii kwa kusaidia msaada huo.

"Shughuli zetu kubwa ni kusaidia kuinua maisha ya watu na sekta ya afya ndiyo nguzo kubwa katika ustawi wa jamii. Msaada ni wa kusaidia kizazi kijacho ambacho ndicho kitaendeleza sekta mbalimbali," alisema Odera.

Alisema Letshego inajivunia kuwekeza hapa nchini na katika nchi nyingine barani Afrika na wanafanya vizuri katika sekta ya fedha na hivyo kuinua kipato kwa jamii.

"Msaada huu ni jukumu letu katika jamii ambayo ndiyo wateja wetu katika shughuli zetu za kila siku. Jamii ina hitaji kubwa la matibabu jambo ambalo taasisi yetu imelipa kipaumbele na kwa kuanzia tumeona tusaidie vifaa tiba katika kitengo hiki cha tiba kwa watoto," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alisema msaada huo ni muhimu sana kwa hospitali yao ambayo inatibia takribani wagonjwa 2,000 kwa siku.

Prof. Janabi alisema Muhimbili ni miongoni mwa hospitali kubwa kwa nchi za Afrika Mashariki na imepanua wigo wa tiba kwa sasa.

"Ni msaada mkubwa na unahitaji pongezi kubwa pia. Tuna uhitaji wa vifaa hivi kwani ni muhimu kwa tiba nyingi. Naipongeza Letshego Holding kwa kusaidia na tunawaomba waendelee kutusaidia," alisema Prof. Janabi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Radhid Mfaume, alipongeza kampuni hiyo kwa msaada huo na kuomba waendelee kufanya hivyo kwa kuwa wanawasaidia Watanzania.



Askofu Rose Mgeta wa Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni B, mkoani Dar es Salaam, akizungumza na Askofu Dunstan Maboya (wa pili kulia), wakati wa uzinduzi wa kongamano la SHILO kanisani hapo Jumapili, ambalo hufanyika kila mwaka kama sehemu ya kumuenzi mwanzilishi wa kanisa hilo, Hayati Dk. Getrude Rwakatare. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kongamano la kumuenzi Rwakatare

**Na Joseph Mwendapole**

KANISA la Mlima wa Moto Mikocheni, Dar es Salaam, limezindua kongamano liitwalo SHILO ikiwa sehemu ya kumuenzi mwanzilishi wa kanisa hilo, Hayati Askofu Getrude Rwakatare.

Uzinduzi wa kongamano hilo la siku nane ambalo hufanyika kila mwisho wa mwaka, ulifanyika Jumapili iliyopita baada ya ibada kanisani hapo na Askofu Dunstan Maboya akiambatana na Askofu wa Kanisa hilo, Rose Mgetta.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi wa kongamano hilo, Askofu Mgetta, alisema kongamano hilo liliasisiwa na hayati Askofu Rwakatare na limekuwa likifanyika kila mwaka hata baada ya kifo chake.

"Maombi ya SHILO yalikuwa maono ya askofu wetu mwanzilishi hayati Askofu Dk. Getrude Rwakatare na tumekuwa tukiyaendeleza mwaka hadi mwaka na makanisa yote ya Mlima wa Moto wamekuwa wakifanya maombi haya kila mwaka," alisema.

"SHILO ni majibu ya mwisho ya mtu ambaye amekata tamaa mfano ameshindwa kupata mtoto, ameshindwa kuolewa akija kwenye tamasha hili la siku nane la SHILO lazima jibu lake lipatikane," alisema.

Alisema wataendelea kuombea taifa liendelee kuwa na amani na kuondokana na majanga kama ukame na matatizo mbalimbali yanayotokea kwenye jamii.

"Ili kanisa liwe na amani lazima nchi iwe na amani kwa hiyo umekuwa wajibu wetu kuhakikisha tunaombea amani ya nchi mara kwa mara na tunamwombea Rais wetu Mungu aendelee kumpa afya njema aweze kuendelea kuliongoza vyema taifa letu," alisema.

Naye Dk. Rose Rwakatare alisema kongamano la SHILO lilianza miaka 20 iliyopita katika kanisa hilo lililoko Mikocheni B, Dar es Salaam.

"Hili kongamano tunakuwa nalo kila mwaka na liliangzishwa na marehemu Askofu Dk. Getrude Rwakatare sisi tunaliendeleza kumuenzi na tunaahidi kuendelea kumuenzi si tu kwa kongamano hili bali kwa kazi zote alizokuwa akizifanya," alisema.

Askofu Dunstan Maboya alisema Askofu Rwakatare aliweka misingi mizuri ya kanisa na ndiyo sababu limekuwa likiendelea kutoa huduma ya kiroho hata baada ya kuondoka kwake.

"Namshukuru Rose Mgeta kwa kusimamia maono haya na kuhakikisha kazi ya Mungu inaendelea na nashukuru kwa mzigo mkubwa aliona Rose kuombea taifa lakini Rose na kanisa wamesimama kuombea nchi dhidi ya majanga kama ukame," alisema Askofu Maboya.

# Benki yaja na kampeni ya funga mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA juhudi za kukuza miamala ya papo kwa papo, salama na malipo bila kutumia pesa taslimu nchini, Benki ya NBC imezindua kampeni yake mpya ya kibenki ya kidijitali inayoitwa "Funga Mwaka Kibabe na NBC Bank' ambayo zaidi ya wateja 400 watajinyakulia zawadi.

Kampeni hiyo inalenga kukuza matumizi ya chaneli za kidijitali mtandaoni kwa wateja wa benki hiyo NBC wakati wa msimu wa sikukuu na mapinduzi mapya ya malipo yanayofanyika kupitia viza (Visa) yatawahakikishia usalama wateja na urahisi zaidi wa kufanya malipo.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidijitali wa NBC, Ulrik Tobias, alisema kupitia kampeni hiyo mpya, wateja wanaofanya miamala kupitia njia mbadala za kidijitali za NBC Kiganjani, huduma kupitia mtandao na kupitia kadi ya NBC Debit watapata fursa ya kujishindia zawadi za pesa taslimu, simu za mkononi, runinga na mengine mengi.

Tobias alisema kampeni hiyo mpya inalenga kuhakikisha wateja wanapata pesa zao kwa usalama na kufanya miamala kwa urahisi, kuongeza urahisi zaidi wa huduma na kuboresha uzoefu kwa wateja.

"Tunataka kuwapa wateja wetu muda wa kutosha kwa ajili ya familia na wapendwa wetu katika msimu huu wa sikukuu kwa kuwahakikishia kwamba wanaweza kufanya miamala yote ya benki wakiwa katika hali ya starehe wakiwa majumbani mwao. Tunaelewa kuwa wengi watakuwa likizo na pengine kujiingiza katika matembezi mengi ya matumizi katika wakati huu.

"Benki ya NBC imehakikisha kuwa unaweza kufanya miamala kwa urahisi na kwa ufanisi ukiwa nyumbani huku ukipata nafasi ya kujishindia zawadi," alisema Tobias.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo inalenga kuwazawadia watumiaji na kadri anavyofanya miamala mingi, ndivyo mteja anavyojishindia na kupokea zawadi za kampeni kama vile simu za mkononi, luninga, punguzo la asilimia 40 kwa ununuzi mbalimbali, zawadi za pesa taslimu na vocha za kufanyia ununuzi.

"Wateja wote wanaotumia kadi zetu za benki za visa, ATM, App ya NBC ya simu, na huduma za NBC Kiganjani watakuwa na nafasi sawa za kushinda zawadi hizi. Wanachotakiwa kufanya ni kufanya miamala na kutakuwa na droo za kila wiki, droo za kila mwezi na zawadi za papo hapo zitashindaniwa," alisema.

Alisema kampeni hiyo ilianza Desemba 2 na itadumu hadi Januari 26, 2023 na kwamba benki hiyo imeshirikiana na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ili kuhakikisha ushindi wote ni wa haki na wa wazi na washindi watatangazwa na kutunukiwa hadharani.

HABARI KASKAZINI

## Wapanda Mlima Kilimanjaro kwenda kusimika ujumbe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TIMU ya mabalozi, askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wanahabari na wasanii wameanza safari ya siku sita ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa ajili ya kwenda kusimika ujumbe maalum wa uhuru.

Kazi hiyo inayowahusisha wapanda mlima 200, itawachukua siku sita kupanda mlima huo hadi kufika kilele cha Uhuru, chenye urefu wa mita 5,895 sawa na futi 19,340 kutoka usawa wa bahari.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alizindua safari hiyo jana katika lango la Marangu la Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), kwa kuwakabidhi bendera ya taifa wazalendo hao, kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Tanganyika yatakayofanyika Desemba 9 kila mwaka.

"Kauli mbiu ya mwaka huu ni The Royal Tour, kuimarisha utalii wa ndani na uchumi. Kauli mbiu hii ni mahsusi katika kipindi hiki ambacho wote tumeshuhudia Rais Samia Suluhu Hassan, alivyoshiriki na kuzindua filamu hiyo.

"Mlima Kilimanjaro ni nembo muhimu ya Taifa na umebeba historia kubwa ya nchi yetu. Mlima huu ni mrefu kuliko milima yote barani Afrika na pia ni mlima mrefu zaidi duniani, ambao upo huru ikimaanisha kwamba hakuna safu za milima, umesimama peke yake.

Kabla ya uzinduzi huo Naibu Kamishna wa Uhifadhi, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Asteria Ndaga, alisema kwa mwaka 2021/22, watalii waliopanda mlima huo ni zaidi ya watalii 3,200 ambao waliliingizia taifa Sh. bilioni 39.

Kiongozi wa jopo hilo la wapanda mlima, Brigedia Jenerali, Salum Mnumbe (JWTZ), akizungumza baada ya kukabidhiwa bendera, aliahidi kulifikisha kundi hilo katika kilele cha Uhuru, kwa kuwa ni jukumu lao kama walinzi wa nchi.

**Mlima huu ni mrefu kuliko milima yote barani Afrika na pia ni mlima mrefu zaidi duniani, ambao upo huru ikimaanisha kwamba hakuna safu za milima, umesimama peke yake.**

# Wanawake waanzisha kiwanda kuchakata muhogo

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

WANAWAKE 40 wajasiriamali walioungana ili kutafuta mwarobaini wa kilio cha wakulima wa muhogo nchini, kukosa soko la uhakika la zao hilo, wameanzisha kiwanda cha kuchakata zao hilo ili kuliongezea thamani.

Kiwanda hicho cha Mkinga Food Processing Factory, kilichojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Japan (JIKA), kwa kushirikiana na Shirika la World Vision Tanzania, kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 150.172, kiko eneo la Kasera, Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga.

Jana, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la World Vision Tanzania, Makarios Charles, alisema lengo la mradi huo ni kufungua milango na fursa za kiuchumi, kwa wanawake kuwekeza katika sekta ya viwanda badala ya kudhani jukumu hilo linawahusu wanaume wafanyabiashara pekee.

**Kiwanda hicho ni ufumbuzi wa soko la muhogo lililokuwa likiwakabili wakulima wa Wilaya ya Mkinga na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.**

"Pamoja na mambo mengine, tunataka kuweka ulinzi kwa watoto kupitia wanawake, ambao watakapozalisha kwa wingi kwa kulima muhogo na viazi lishe na kisha kusindikwa, watakuwa wameleta suluhisho la tatizo hilo."

Alisema shirika hilo ambalo hapa nchini lipo katika mikoa 18, kwa Mkoa wa Tanga wako katika Wilaya za Mkinga, Korogwe, Kilindi na Handeni, wamejikita kwenye miradi ya kilimo, kuzikwamua kaya maskini kiuchumi na ulinzi wa watoto.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Elizabeth Malali, akizungumzia uwekezaji huo, alisema kupitia kiwanda hicho serikali inatarajia wanawake wataweza kujikwamua kiuchumi na kuzalisha kwa tija.

Alisema kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, ilitoa Sh. milioni 247 kupitia mapato yake ya ndani, kwa ajili ya kutoa mkopo usio na riba kwa wanawake, vijana na jamii ya watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa kikundi hicho kinachomiliki na kiwanda hicho, Mwanakombo Hussein, alisema kwa kuwa kina uwezo mkubwa wa kusindika muhogo na viazi lishe tatizo litakuwa ni upatikanaji wa malighafi ya kutosheleza kiwanda hicho na soko la bidhaa zitakazosindikwa.

Mbunge wa Mkinga, Danstan Kitandula, alisema kiwanda hicho ni ufumbuzi wa soko la muhogo lililokuwa likiwakabili wakulima wa Wilaya ya Mkinga na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Alisema wakulima waliokuwa wakilalamika mihogo yao kukosa wanunuzi wamepata kimbilio na kwamba Ofisi ya Mbunge, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Halmashauri ya Wilaya hiyo, kazi yao itakuwa ni kuwatafutia masoko ya uhakika na ya kudumu ya bidhaa zitakazosindikwa kupitia kiwanda hicho.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akiwa pamoja na Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (mwenye kofia), Meneja wa kituo cha CCBRT Moshi, Lucy Kavishe (wa tatu kushoto) na wadau wengine wa masuala ya watu wenye ulemavu hapa nchini, wakati wa kuadhimisha siku ya watu wenye ulemavu duniani 2022, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. CCBRT kwa kushirikiana na ofisi ya Mbunge huyo, walikabidhi viti mwendo 100 kwa watu wenye ulemavu na baadhi yao kunufaika na kadi za bima za afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EWURA yatatua kero 1,500 wakazi mikoa ya kaskazini

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imezipatia ufumbuzi kero 1,500 zilizowasilishwa na wananchi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, malalamiko mengi yakihusu kupaa kwa gharama za matumizi ya maji.

Meneja wa EWURA, Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, alisema kero hizo zilipokelewa ofisini kwake na kupatiwa majibu kwa haraka katika mwaka wa fedha 2021 /2022.

Long'idu alikuwa akizungumza jana jijini Arusha, wakati alipokuwa akitoa elimu kwa madiwani na watendaji wa kata, kuhusu wajibu wa kisheria wa utekelezaji wa majukumu ya EWURA.

"Sisi kama mamlaka, tumeona kwa nafasi kubwa tuliyonayo katika jamii, ni vyema kuwashirikisha na ninyi kutambua kazi za mamlaka ili mtusaidie kuelimisha wananchi kuhusu wajibu wa EWURA na namna wanavyoweza kuwasilisha kero au malalamiko yao kuhusu huduma za maji na umeme.

"Tunataka wananchi wanaokutana na tatizo la kupandishiwa gharama za matumizi ya maji au nishati ya umeme, watupe taarifa rasmi kwa kufika ofisini kwetu na kutoa malalamiko ili tufanye uchunguzi na kuchukua hatua."

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda, alielekeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Arusha (AUWSA), kuacha kujificha kwenye kichaka cha miba na kutambua wajibu ni pamoja na kuwapokea wananchi kwa ukarimu na kusikiliza kero zao za huduma ya nishati na maji, na siyo kutupa mzigo huo kwa viongozi wakuu wa serikali.

Kwa mujibu wa Mtanda, kikao hicho kililenga kujadili kero mbalimbali zitokanazo na sekta ya maji na umeme, ambayo ndio matumizi makubwa kwa wananchi ya kila siku.

Alisema kuwa madiwani na watendaji wa kata, wana nafasi kubwa ya kuwafikishia wananchi ujumbe, juu ya huduma wanazozipata kutoka katika mamlaka ya maji na TANESCO.

Meya wa Jiji la Arusha, Maxmalian Iraghe, alisema madiwani wamekuwa chachu ya kutatua kero za wananchi na kwamba kutokana na elimu walioipata, sasa watakuwa mabalozi wazuri wa EWURA kwenye maeneo wanayoongoza.

# RC Kilimanjaro ageuka mbogo ujenzi hospitali ya wilaya

**Na Anjela Mhando,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amegeuka mbogo baada ya kukuta mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Moshi ukisuasua huku serikali ikiwa imeshatoa Sh. milioni 500 za utekelezaji wa mradi huo.

Badala yake amemsihi mkandarasi huyo asisubiri kuiona sura yake baada ya tarehe ya ukomo aliyoitoa kutekeleza mradi huo kumalizika, akitaka aheshimu makubaliano ya mkataba wake alioingia na serikali.

Babu aling'aka, baada ya kutembelea mradi huo jana katika Kijiji cha Mabogini na kutoa siku 30 kwa mkandarasi huyo kukamilisha kazi hiyo kufikia Januari 14 mwakani.

"Wewe fundi mkuu naagiza, mwambie bosi wako kwamba nimesema kazi hii mwisho Januari 14, 2023. Nataka wananchi waanze kupata huduma za matibabu karibu na maeneo yao. Hakuna kisingizio kwa sababu serikali ilishaweka mambo yote sawa.

**Nataka wananchi waanze kupata huduma za matibabu karibu na maeneo yao. Hakuna kisingizio kwa sababu serikali ilishaweka mambo yote sawa.**

"Kwa maana hiyo, mkandarasi unatakiwa kufanya kazi yako usiku na mchana. Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya ya Moshi, andaa mpango kazi wa utekelezaji ambao utaainisha kazi zilizobaki na muda wa ukamilishaji ili kuraхisisha utekelezaji."

Mwezi uliopita, Timu ya Usimamizi Shirikishi kutoka Idara ya Huduma za Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ikiongozwa na Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Dk. Ntuli Kapologwe, iliishauri Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya (CHMT) Halmashauri ya Wilaya Moshi, kuongeza kasi katika ujenzi wa hospitali hiyo ili ujenzi ukamilike kwa wakati na huduma zianze kutolewa kwa wananchi.

Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya ya Moshi, Dk. Damas Mushi, alisema mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo unaotekelezwa katika eneo la Mabogini, Halmashauri ya Wilaya hiyo, ilipokea Sh. milioni 500 za awamu ya kwanza ya ujenzi huo unaohusisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD).

Diwani wa Mabogini, Dk. Bibiana Massawe, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali hiyo kwa kuwa wananchi walikuwa wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa 17 kufuata huduma hiyo Manispaa ya Moshi.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akikabidhi bendera ya Taifa kwa Mkuu wa msafara Brigedia Jenerali Salum Mnumbe, wakati wa uzinduzi wa kupanda Mlima Kilimanjaro, kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara, juzi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Hakimu asababisha kesi ya Ole-Sabaya kupigwa kalenda

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KESI ya uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na rushwa, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya imepigwa kalenda hadi Desemba 12 mwaka huu.

Jana kesi hiyo namba 2 ya mwaka huu, ilishindwa kuendelea, baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Salome Mshasha, anayesikiliza shauri hilo kuwa kwenye majukumu mengine.



Kutokana na udhuru huo Hakimu Mkazi, Erasto Philly, alilazimika kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 12, baada ya upande wa mashtaka kuwasilisha ombi la kutaka kuahirishwa ili kumpa fursa hakimu anayeisikiliza kurejea mahakamani hapo.

Kabla ya kuahirishwa kwa shauri hilo, Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Susan Kimaro, alidai kuwa wanashindwa kuwasilisha vibali vya usikilizaji wa shauri hilo, kwa kuwa hakimu anayesikiliza kesi hiyo, yupo nje ya kituo chake cha kazi kwa ajili ya mafunzo, hivyo wanaomba tarehe ya karibu ili kukamilisha jambo hilo.

Aidha jopo la mawakili wa utetezi, ukiongozwa na Helen Mahuna, ulidai kuwa hauna shida na hoja iliyotolewa mahakamani hapo na upande wa mashtaka na kwamba na wao wanaomba mahakama kupanga tarehe ya karibu itakayowasaidia kukamilisha taratibu hizo.

Makosa anayokabiliwa nayo, Ole Sabaya ni kuongoza genge la uhalifu katika Wilaya ya Hai, Februari 2 mwaka jana na kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, Februari 22 mwaka jana.

Aidha Ole Sabaya, anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai, kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

Pia anakabiliwa na kosa la ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma katika Wilaya ya Hai na shtaka la utakatishaji wa fedha.

# Msekwa akoshwa utendaji kazi TCU, aisifia MoCU

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SPIKA wa zamani wa Bunge, Dk. Pius Msekwa (87), amesema licha ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kupata mafanikio makubwa ya kuongeza udahili wa wanafunzi kila mwaka, 'anakoshwa' na namna Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), inavyojiongeza kwa kufungua dirisha la kwanza, la pili hadi la tatu la udahili wa wanafunzi katika vyuo mbalimbali.

Msekwa alieleza hayo jana akiwa katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, alikokwenda kutunuku astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili, kwa wahitimu 4,356 waliofuzu mitihani ya mwisho inayotolewa chuoni hapo kupitia programu za masomo mbalimbali.

Katika mahafali hayo, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Alfred Sife, alisema idadi ya wanaodahiliwa MoCU, inaongezeka kila mwaka, jumla ya wanafunzi 4,490 wamedahiliwa katika mwaka wa masomo wa 2022/2023 na kufanya idadi ya wanafunzi walioko chuoni hapo kufikia 8,820.

"Kuongezeka wanafunzi hapa chuoni kumesababisha menejimenti ya chuo kuendelea kuboresha miundombinu ya ufundishaji, kufadhili baadhi ya wahadhiri kwenda kuongeza elimu ili kuboresha elimu inayotolewa na chuo hicho.

Akizungumzia mipango ya baadaye kuhusiana na chuo hicho, Prof. Sife alisema pamoja na kuongeza miundombinu ya ufundishaji chuoni hapo tayari kuna miradi ambayo inaendelea kutekelezwa ili kutimiza azma hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini la Chuo Kikuu hicho, Dk. Marina Nsekela, aliipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa chuo kikuu hicho jambo ambalo limekiwezesha kupata mafanikio makubwa ya kitaaluma.

Dk. Nsekela alisema kuwa kuendelea kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na chuo hicho na wale wanaohitimu kila mwaka ni ishara tosha ya kuwa chuo hicho kinatoa mchango mkubwa katika upatikanaji wataalamu wa fani mbalimbali wanafamya shughuli zao ndani na nje ya nchi baada ya kuhitimu kwao.

Ukurasa 14



**Heche awashukia vijana, awakumbusha mabadiliko duniani huletwa na kundi hilo**

Ukurasa 18




Viwanda simu za mkononi vinavyoleta kiama DRC

Ukurasa 19



**Ruto, Gachagua watoa somo sera za kuwafikia vijana**

siasa

JUMATANO DESEMBA 7, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

MIAKA 61 YA UHURU

# Tanzania bado inabanwa utegemezi kiteknolojia, unazidi kufifisha maendeleo

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

TANZANIA imepitia mafanikio na changamoto mbalimbali inapoelekea kuadhimisha miaka 61 ya uhuru wake wiki hii Ijumaa Desemba 9. Mafanikio, matatizo na changamoto hizo zimo kwenye sekta karibu zote ikiwamo teknolojia ambayo ni muhimili na uti wa mgongo wa maendeleo.

Licha ya juhudi kama kuongeza wataalamu kwa kuwasomesha nje na ndani, kukuza ubunifu na ugunduzi pamoja na utafiti ili kuchangia maendeleo ya teknolojia, bado utegemezi kwenye teknolojia umeendelea kulibana taifa na kufifisha kasi ya maendeleo kwa kuwa teknolojia ni muhimu au ndiyo kila kitu.

Utegemezi huo wa kiteknolojia tangu mwaka 1961 umekuwa kwenye maeneo karibu yote ya uzalishaji na huduma, kwa mfano sekta ya nishati uzalishaji wa umeme umekuwa moja ya sehemu ambazo zinaweza kuwa zimeathirika kutokana na utegemezi huo wa wataalamu , vifaa na teknolojia za kigeni.

Licha ya wataalamu hasa kutoka kwa mataifa wahisani au wanaopata zabuni za kiufundi kujenga miundombinu ni wataalamu wao wanaohusika kuweka vifaa mfano jenereta na transfoma. Hata likitokea tatizo taifa linarudi tena kwa wazalishaji (manufacturers) na wataalamu hao ndiyo wanaowafahamu na wanaohusika kutengeneza au kuchonga kipuri na kukileta nchini ili jenereta za kufua umeme na transfoma ziweze kufanyakazi tena.

Wakati mwingine ni masharti ya msaada ya wahisani kuwa wataalamu wa nchi waliotoa msaada wa kujenga miundombinu na kuweka mitambo ndiyo watakaokarabati na kutunza (maintenance and repair) mitambo hiyo kwa miaka kadhaa pengine hata 25. Yote hayo yanaongeza utegemezi na gharama kubwa ya kununua vifaa na vipuri vya ukarabati, kulipa gharama za wataalamu kuja na kukaa nchini kufanyakazi kwa thamani yeyote wanayoitaka.



Teknolojia za kujenga miundombinu ya kisasa inategemea wahandisi wa kigeni ambao ndiyo wanaokarabati na kuisimamia kutokana na kuhodhi ujuzi.**PICHA: IPP.**

Inapotokea jenereta 'linabuma' kwenye kituo cha kuzalisha umeme inabidi mitambo izimwe mawasiliano yafanyike wakati mwingine zabuni zitangazwe na mchakato unaweza kukamilika baada ya miezi kadhaa na ukarabati ukafanyika baada ya mwaka yote hayo yanaweza kusababisha ukosefu wa umeme na mgawo, chanzo kikiwa ni msaada wa kiteknolojia.

Mambo hayaishii hapo hata katika huduma za vifaa vya kisasa vya matibabu kama MRI na CT Scan zinazotumiwa hospitalini kutokana na misaada zinakuja na masharti kwamba ni lazima zitakarabatiwa na kutunzwa au kuangaliwa na watalaamu wa kampuni fulani, yote haya yanawaweka nyuma wataalamu wa Tanzania na pia kulisukuma mbali taifa na masuala ya utaalamu unaohusiana na vifaa hivyo.

Wakati mwingine utegemezi wa wataalamu wa kigeni kwa asilimia kubwa unaweza kulisababishia taifa mambo ambayo hayakutegemewa kwa mfano inaweza kuwa chanzo cha wagonjwa kuumia hospitalini pengine hata kufariki hasa wa familia maskini kutokana na masharti kuwa mashine zinapoharibika ni lazima zikarabatiwe na kampuni fulani na iwapo kuna hitilafu zizimwe mpaka wahusika watakapofika nchini.

Kadhalika ni vyema pia kama taifa kutafakari matumizi ya washauri elekezi. Hawa ni pamoja na kampuni za kigeni zinazopewa jukumu la kufanya tathimini ya uharibifu wa mazingira. Ni suala muhimu lakini linafanyikaje? NI jambo la kuangalia pia,na hata ikibidi eneo hilo lifanywe na wataalamu wa Tanzania wenye elimu , ufahamu na uelewa wa masuala ya Tanzania kuanzia mazingira yake, hali za jamii , maumbile ya kijiografia na hali halisi iliyopo sasa.

Inawezekana taifa halina fedha za kufanya utafiti huo kwa wakati huo, lakini ukweli ni kwamba gharama kubwa zitakazoambatana na msaada wa kiteknolojia zinaweza kuliumiza zaidi kwa miongo mingi , hivyo uwekezaji wa wataalamu wa kufanya uchunguzi wa athari za kimazingira na ushauri elekezi usipuuuzwe.

Ikumbukwe wataalamu wengine wanaweza kutoa ushauri

INAENDELEA UK. 20

# Heche awashukia vijana, awakumbusha mabadiliko duniani huletwa na kundi hilo

## •Asikitika matajiri kuikwepa CHADEMA

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA ni moja ya makundi katika jamii, yenye mchango wa maendeleo kutokana na nguvu walizo nazo, bidii, uthubutu na ukweli kwamba hakuna taifa lolote duniani linaloweza kukua na kuwa imara kiuchumi, kisiasa, kijamii kama litaliweka kundi hilo pembeni.

Vijana wanaweza kupambana na vikwazo vingi katika taifa kama njaa, vita, umaskini, maradhi, elimu duni na ugumu wa maisha, kutokana na kwamba ndiyo wenye nguvu na uthubutu na mara nyingi wana tumaini kuwa wanatakiwa kupambana ili kusonga mbele na kuishi zaidi.

Umuhimu wa vijana kwa taifa, unamwibua Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, John Heche na kuwakumbusha kuwa mabadiliko yoyote duniani hayaletwi na watawala au matajiri bali vijana na watu maskini na kuwataka kubadilika na kufanya juhudi za kufikia mabadiliko.

Anasema maskini hao ni wale wanaopigania maisha na maendeleo katika taifa lao na kwamba kwa pamoja wanaweza kuungana na kuhakikisha wanaleta mabadiliko kwa njia ya sanduku la kura katika uchaguzi na pia kwa kujituma kufanyakazi kwa bidii.

"Labda niwakumbushe kuwa kawaida watawala huwa hawana cha kupoteza, hivyo hawawezi kuleta mabadiliko na pia hayaletwi na matajiri bali ni vijana na watu maskini ambao wanatamani kuwa na maisha au hali bora zaidi,"anasema Heche.

Mjumbe huyo anayaibua hayo wiki iliyopita katika mkutano wa ndani wa chama hicho, unaoihusu Kanda ya Pwani, Kibaha Maili Moja na kufafanua kuwa CHADEMA ikiingia madarakani, kila mwenye uwezo atapata kazi serikalini.

Anasema, watafanya hivyo bila kujali yupo CCM au upinzani, lengo likiwa ni kuwahakikishia Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi serikalini wanaajiriwa na siyo kuchukua wachache na kuacha kundi kubwa nje.



John Heche, kwenye majukwaa ya kisiasa. **PICHA: MAKTABA**

**AWAGUSA MATAJIRI**

"Lakini pia kuna suala ambalo haliko sawa. Ukitaka kujua unafiki wa watu wenye mali, huwezi kuwakuta CHADEMA. Hivi ni kweli wote hawatuelewi? Au sera zetu hazieleweki wala kazi tunazofanya?

Aidha, anagusia mikutano ya hadhara na kusema, kuanzia Desemba wataanza mikutano ya hadhara, ili kuimarisha chama hicho ikiwa ni sehemu ya maandalizi, kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2024/25.

Kwa mara ya kwanza, Heche anatangaza msimamo huo Novemba 16 mwaka huu akiwa katika mkutano mkuu wa chama hicho, jimbo la Sengerema mkoa Mwanza, kwamba ndani ya mwezi mmoja ujao chama kitaanza ratiba hiyo ya mikutano ya hadhara.

Heche aliyewahi kuwa mbunge wa Tarime Viijijini mkoani Mara, anasema mwaka huu hautaisha bila chama hicho kuanza kufanya mikutano ya hadhara ambayo ni haki yake kikatiba na kisheria kwa vyama vyote vya siasa.

Msimamo huo wa CHADEMA unakuja huku kukiwa na vikao mbalimbali vya wadau wa siasa vya kutafuta njia bora ya kuendesha shughuli za kisiasa ikiwamo mikutano ya hadhara iliyozuiwa na serikali mwaka 2016.

Tangu mwaka huo baada ya kuzuiwa na serikali ya awamu ya tano, madiwani na wabunge ndio walioruhusiwa kufanya mikutano katika maeneo yao ya uchaguzi, huku viongozi wakuu wa vyama wakipigwa marufuku.

Sasa CHADEMA inaibuka na kuwataka viongozi na makada wake kujitolea kwa hali na mali kukijenga na kujianda kwa ajili ya chaguzi ili kushika dola, kwa madai kwamba chama hicho kinapendwa na Watanzania wengi.

Anawaambia Watanzania kuwa CCM haiwezi kuleta maendeleo hata ikipewa miaka 100 ya kukaa madarakani, kwa madai kwamba, nchi ina miaka 61 tangu ipate uhuru, lakini inajadili matundu ya vyoo vya vya shimo.

> "Kikosi kazi kinapendekeza mikutano ya hadhara iruhusiwe kufanyika kwa mujibu wa katiba na sheria ya vyama vya siasa. Mikutano ya ndani ya vyama vya siasa iendelee kufanyika bila vikwazo vyovyote.

Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Mwanza, Grayson Wanzagi na Katibu wa Kanda ya Victoria, Zacharia Obadi wanawataka viongozi na wanachama kukijenga kiwe taasisi imara tayari kushinda uchaguzi ujao na kushika dola.

**KIKOSI KAZI**

Moja ya mapendekezo ya kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau kuhusu demokrasia ya vyama vingi, ni kutaka mikutano ya hadhara iruhusiwe sambamba na mabadiliko ya sheria mbalimbali zitakazowezesha mikutano hiyo kufanyika kwa ufanisi.

Hayo yalibainishwa Oktoba 21 mwaka huu, Ikulu jijini Dar es Salaam na mwenyekiti wa kikosi kazi, Profesa Rwekaza Mukandala, wakati akiwasilisha mapendekezo ya kikosi hicho kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Profesa Mukandala akasema kwamba, baada ya kikosi hicho kufanya kazi kwa miezi 10 kikichambua maoni mbalimbali ya wadau, kinapendekeza mikutano ya hadhara iliyozuiliwa mwaka 2016, iruhusiwe kufanyika

"Kikosi kazi kinapendekeza mikutano ya hadhara iruhusiwe kufanyika kwa mujibu wa katiba na sheria ya vyama vya siasa. Mikutano ya ndani ya vyama vya siasa iendelee kufanyika bila vikwazo vyovyote.

"Yafanyike marekebisho ya sheria ili kuhakikisha mikutano ya hadhara inafanyika kwa ufanisi. Sheria hizo ni pamoja na sheria ya vyama vya siasa sura ya 258, sheria ya jeshi la polisi na huduma saidizi, sura ya 3022 na kanuni za maadili ya vyama vya siasa za mwaka 2019," Profesa Mukandala anasema.

Wakati pendekezo hilo na mengine 17 yakiwa yamefikishwa na Rais, kwa ajili ya hatua zaidi za maamuzi, inaonekana CHADEMA uzalendo unawashinda na sasa wametangaza kuanza mikutano hiyo.

# Wanaume waibua sababu kuwa chanzo ukatili kijinsia na jinsi ya kuukabili

**Na Salome Kitomari**

JITIHADA za kupigania haki za wanawake na watoto zimeshika kasi kila kona, kiasi cha kuhofisha wanaume wanaodhani wanaachwa nyuma na siku zijazo kampeni za kutetea haki za kinababa zinaweza kuibuka.

Baadhi ya wanaharakati wakiwamo Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wameliona hilo na kuibua programu ya kuwaleta pamoja wanaume kujadili ukatili wa kijinsia na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili wasije kuwa wahanga.

Ni katika mdahalo wa wanaume, unaofanyika Dar es Salaam, ambako kinababa wanafunguka kuhusu kiini cha ukatili, changamoto wanazopitia na mikakati ya kujikwamua.

WANASEMAJE?

Ni washiriki 30 kutoka sekta mbalimbali wanaoshiriki mjadala huo wakisema vichocheo vya ukatili wa kijinsia ni kuonyesha nguvu walizonazo kinababa baada ya kuachwa nyuma kwenye mipango, sera na mikakati ya kitaifa.

Aidha, wanasema ni muhimu sera, mipango na mikakati ya nchi ikajumuisha wanaume na wanawake, huku wakitaka kuanzishwa kwa majukwaa ya wanaume ngazi za mtaa, vijiji hadi taifa ili waeleze matatizo wanayopitia.

Mwakilishi kutoka Gender Health, Dk. Katanta Simwanzi, anasema wanaume wanaofanya kazi ambazo hazijazoeleka katika jamii mfano kusaidia wake zao, huchukuliwa kama wadaifu wasio na nguvu au waliologwa.

"Wanaume tuliambiwa tusilie, rafiki yangu alifiwa na baba yake akalia alifuatwa na wanaume wakamwambia hatakiwi kulia, kila nikionana naye ananiambia natamani kulia kwa kuwa sikupata nafasi ya kulia siku ya msiba wa baba yangu. Wanaume tumekatazwa kuonyesha hisia zetu tunaambiwa tuvumilie," anasema.

Wakili Severine Allute, anasema Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Wanawake wa mwaka 1995 Beijing China, uliwasahau wanaume na kuja na mikakati ya kumkuza mwanamke kwa nyanja zote, ndiyo maana mipango na mikakati mingi imelenga kinamama na kuwaacha wanaume.

"Nguvu ya kiuchumi ni tatizo kwa wanaume wengi, wanawake wameinuka zaidi kwa sasa, mtu anapokuwa na nguvu kiuchumi anashirikiana na wanaofanana naye. Mwanaume anaona haheshimiki kwenye familia kwa sababu ni mnyonge na mama anajiweza zaidi kiuchumi," anasema.

Anasema ujengaji uwezo ulifanyika upande mmoja na hasira ya wanaume hujitokeza wanapoona wanadharaulika kwa sababu ya kipato, nguvu hazionekani wala heshima ndipo ukatili hutokea kwa sababu ya kutaka tena nafasi yao.

Mtaalamu wa vimbwembwezo- IT, Ikundwila Mwambona, anasema majukumu mazito kama vita na kazi ngumu na kujengwa kisaikolojia kwamba ni wenye nguvu na wanatakiwa kusikilizwa ni mambo yanayoachwa na dunia imebadilika.

"Tupo kwenye utandawazi siku hizi jinsia zote zina nguvu, zamani mama akitaka kukutisha anakwambia nitamwambia baba yako na kweli akirudi anakusema unatandikwa, hivyo unamuona baba ni mbaya na mama mzuri."

Akichangia mjadala huo, mshiriki Juma Rashid anasema; "mifumo ya jamii ilitujenga kwamba sisi ndiyo kila kitu, unadharaulika wakati mwingine unaitwa mwanaume suruali, ukiona hivyo ujue kuna mahali ulikosea, unarudi nyumbani umelewa, unavua nguo mbele ya watu nani atakuheshimu?"

"Kuwa kichwa cha familia sio kumpiga mke, kwa sasa matukio yote mabaya wanatajwa wanaume tujitathmini tunakosea wapi, lazima tuishi kwa kushirikiana badala ya kulipiza kisasi kwa kuwapiga, kuwajeruhi au kuua."

James Maduka, anasema tatizo ni mfumo akitoa mfano wakati wanakua nyumbani kwao walimpa baba yao jina la kikatili na kwamba wakifanya kosa akiambiwa aliwaadhibu hatua iliyozidi kujenga umbali naye.

Joseph Msendo, anasema sera na sheria zinawapa nguvu na kuwalinda wanawake zaidi, kwa mfano wazazi wanapotengana baba haruhusiwi kumlea mwanawe hadi afikishe miaka saba wakati mama anaruhusiwa kuwa naye tangu mdogo.

Wakili wa kujitegemea, Mlowe Pasience, anasema maandiko matakatifu yameelekeza wanaume kuishi kwa upendo na wake zao, wanapokosa kuyatimiza matatizo yanaanza na kuona hawapewi heshima.

"Umeoa, lakini unaendelea kuishi maisha ya ubachela, unahama baa moja kwenda nyingine kama wasio na familia, unarudi asubuhi ukiombwa fedha unasema huna ila unalewa, ukijibiwa vibaya unarusha ngumi na kunyanyasa mke na watoto, huu ni ukatili, lazima turudi kwenye upendo," anafafanua Mlowe.



Wakili wa kujitegemea, Mlowe Pasience ( mwenye kipaza sauti ) akifafanua jambo kwenye mjadala wa ushiriki wa wanaume katika kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

> "Kuwa kichwa cha familia sio kumpiga mke, kwa sasa matukio yote mabaya wanatajwa wanaume tujitathmini tunakosea wapi, lazima tuishi kwa kushirikiana badala ya kulipiza kisasi kwa kuwapiga, kuwajeruhi au kuua."

Anataja umaskini huchochea ukatili kwamba maskini anamuumiza mkewe kwa kipigo kwa sababu kaombwa fedha wakati hana.

Wakili huyo anasema vijana hawaandaliwi kuingia kwenye ndoa bali wanatumia sababu za kwamba amepata mimba, msukumo wa jamii au umri umekwenda, ndiyo maana wanaendelea kuishi maisha ya ujana ikiwamo kuwa na 'michepuko'.

Mshiriki Zenno Ngowi anasema; "Ukitaka watoto wakupende mpende mama yao, muwe na vikao vya mara kwa mara vya familia kuzungumza kwa uwazi, kushirikiana kuendesha maisha, wanaume tuwe wakweli kwa familia zetu kuanzia kipato na tusiishi maisha ya udanganyifu."

Anaungwa mkono na Azam Zahoro, akisema hali ya uchumi ni kikwazo kikubwa kwa wanaume na kwamba wanawake wengi wana vikundi vinavyowawezeshana.

"Anakuomba fedha kila siku huna, hajui mshahara wako ila unalewa, akikuita mwanaume suruali unarusha ngumi, lazima tujijenge kiuchumi."

Mchambuzi wa Uwekezaji, Moshi Elinaja anasema wanaume wengi hawako makini na mfano ni siku ya wababa huoni anayesema lolote kwa kuamini wataonekana ni dhaifu au wanapigania haki, huku siku ya wanawake kuna shamrashamra nyingi wanaweka mikakati ya kujiendeleza kiuchumi.

"Wanawake wana VIKOBA wanapeana mikopo mikubwa, zamani tuliwanyanyasa kiuchumi na kimila ila kwa sasa kiuchumi wako vizuri, ukiambiwa mwanaume suruali unarusha ngumi wakati ni kweli huna fedha. Nimesoma mahali kuwa ikifika 2050 tutaanza kupigania haki za wanaume," anasema.

**UMUHIMU MDAHALO**

Ofisa Habari wa TGNP, Monica John anasema mdahalo huo ni sehemu ya uwepo wa vilinge salama au majukwaa huru kwa wanawake (female safe space).

Anasema wamegundua kuwa majukwaa hayo yameleta chachu kubwa kwa kuwapa uhuru washiriki kufunguka na kuongelea masuala yanayowaathiri wakitaja ukatili wa kijinsia.

"Kwa mara ya pili sasa nimeratibu jukwaa huru na salama kwa wanaume (safe space for men) kwa lengo la kutoa fursa kwa wanaume kuzungumzia kiundani masuala ya kijinsia na nafasi yao katika kutokomeza ukatili,"anasema.

Jukwaa hilo ni muhimu kwa kuwa wanaume wanatuhumiwa na wahanga wa ukatili kwa wanawake na watoto kuanzia kwenye ngazi ya familia hivyo ni muhimu kuwa sehemu ya suluhisho la kutokomeza ukatili wa kijinsia, anaongeza Monica.

"Kuwahusisha katika mijadala kutaleta tija kwenye kubadilisha mitizamo na tabia zao hasi dhidi ya wanawake, kwa kutambua kuwa kuna wanaume ambao huheshimu, kulinda, kuwathamini wanawake na wamekuwa chachu katika harakati za kuleta usawa wa kijinsia ikiwemo kutokomeza ukatili wa kijinsia."

"TGNP inaamini kuwa wanawake na wanaume kwa pamoja wakishiriki katika harakati za kutokomeza ukatili wa kijinsia, tutapiga hatua kwa haraka zaidi, hasa katika kutengeneza mtizamo chanya juu ya jinsia jambo ambalo litasaidia kubadili tamaduni na mila kandamizi zinazochochea ukatili,"anasema Monica.

**KWANINI JUMUISHI?**

Monica anasema ni suala jumuishi: "Inamaanisha kuwa asiache mtu nyuma katika kushughulikia janga hili la ukatili wa kijinsia. TGNP inaamini katika nguvu za pamoja kuleta mabadiliko ya haraka, jumuishi na endelevu. Hivyo, suala hili la ukatili wa kijinsia linapaswa pia kushughulikiwa kwa ujumuishi."

"Ukweli ni kuwa ukatili wa kijinsia haumwathiri tu jirani ambaye utaona anathirika na kuacha kuchukua hatua, unaweza pia kukufikia nyumbani kwako- hivyo ni muhimu kila mtu kusimama na kukemea, kutoa taarifa wanapoona ukatili au dalili zake ili kumlinda mtoto au mwanamke,"anasema MOnica.

Aidha, anasema licha ya kwamba kuna changamoto ya kupatikana kwa takwimu, ni muhimu pia kuangalia aina za ukatili wa kijinsia unaofanywa kwa wanaume pia na kuuzungumzia kwa kuwa lengo ni kuwa na jamii isiyo na ukatili.

# Ndivyo vita vya Urusi, Ukraine vinavyoathiri uchumi Tanzania



Gavana wa BoT, Profesa Florens Luoga, akizungumzia masuala ya sera za fedha na uchumi.**PICHA:MAKTABA**

**Na Salome Kitomari**

TANGU kuanza kwa vita vya Urusi na Ukraine Februari mwaka huu, hali ya maisha kwa nchi za Afrika hayajabaki kama ilivyokuwa kutokana na mataifa hayo kutegemewa kwa bidhaa muhimu za chakula na mafuta.

Ukraine ni mzalishaji mkubwa wa ngano, mahindi na alizeti ndio maana, mafuta ya kula yamezidi kupaa bei, hali inayowafanya wananchi wa hali ya chini kuwa waathirika wa vita hivyo.

Afrika inakabiliwa na tatizo kubwa la athari za mabadiliko ya tabia nchi, ukame umeumiza watu na viumbe wengine, mvua zilizosababisha majanga makubwa na ardhi isiyofaa tena kwa kilimo, hali iliyoathiri usalama wa chakula kwa mataifa mengi.

Pia bara hilo limepigwa na janga la COVID-19 kwa watu wake kupoteza maisha, biashara kuharibika na uchumi wa nchi kuyumba kwa sababu ya maradhi hayo na wakati ikijikwamua kutokana na athari hizo Urusi inaivamia Ukraine na kuongeza mzigo mzito.

Mafuta ni bidhaa mtambuka ambayo inapoathirika inaleta madhara maeneo mengi na kuyumbisha mihimili yote ya uchumi, na sasa bei ya vyakula inazidi kupaa.

Kwa mujibu wa ripoti mbalimbali, Urusi ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mafuta duniani, baada ya Marekani na Saudia Arabia, kati ya mapipa milioni tano ya mafuta ambayo husafirishwa nje kila siku, zaidi ya nusu huenda Ulaya na Marekani inategemea sana takribani asilimia tatu ya mafuta yanayoingizwa kutoka Urusi.

Ndiyo maana, Marekani inaitaka Saudia Arabia kuongeza uzalishaji wa mafuta lakini ilipinga maombi hayo, kwa mujibu wa Shirika la Mafuta Duniani (OPEC), Saudia Arabia ni mzalishaji mkubwa zaidi wa mafuta na shirika hilo huchukua asilimia 60 ya mafuta yote yaliyosafishwa yanayouzwa kimataifa.

Tanzania ni moja ya nchi iliyoathiriwa na vita hiyo na hadi sasa haijaweza kupona kutokana na ukweli kuwa mafuta yanaagizwa kutoka nje, kunapokuwa na vikwazo bidhaa inapungua ndio maana bei ilipaa.

Machi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, anasema: "Baada ya COVID-19 hakukuwa na uzalishaji viwandani kama bidhaa ni chache lazima bei zipande, vita vya Urusi na Ukraine vimepandisha sana bei ya bidhaa nchini. Waambieni wananchi ukweli."

> Kiwango hicho ni cha chini ikilinganishwa na takwa la Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), inayotaka angalau miezi minne na nusu huku Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) inataka ya miezi sita.

Baada ya Rais kusema hivyo, Mei mwaka huu, Waziri wa Nishati, Januari Makamba, anatangaza uamuzi wa serikali kuweka ruzuku ya Shilingi bilioni 100 kila mwezi kwa ajili ya kusaidia kushusha bei ya nishati hiyo.

Taarifa ya bei kikomo iliyotolewa Novemba mwaka huu na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), bei ya bila ruzuku kwa petroli ni Sh. 2,996, dizeli 3,197 na mafuta ya taa 3,111, baada ya ruzuku ni Sh. 2,886 kwa petroli, 3,052 dizeli na 3,111 kwa mafuta ya taa.

Mkazi wa Kondoa ambaye ni mlemavu wa macho, Abeid Abubari, anasema alinunua pikipiki imsaidie mwanaye kupata fedha na kwamba bei ya mafuta imepanda kutoka Sh.2,500 hadi 3,000 kwa lita, abiria wanakataa kupanda na kwamba wamepitia wakati mgumu licha ya kujituma kwenye kazi ili kumudu maisha yao.

Mwanaima Shamshudini anayepika vitafunwa Mwenge-Dar es Salaam, anasema kutokana na kuongezeka bei ya unga wa ngano wanalazimka kupandisha chapati na maandazi.

Oktoba mwaka huu, Kamishna wa Umoja wa Ulaya (EU), Jutta Urpilainen, anatembelea Tanzania na kutangaza kuwa EU itatoa mkopo wa Shilingi bilioni 370 ikiwa ni nyongeza , Februari mwaka huu ilitoa Shilingi bilioni 400.

"Tunatambua Tanzania imepitia kipindi kigumu cha COVID1-19 na sasa vita inayoendelea Ukraine imeendelea kuleta athari, tunatoa fedha hizi kuisaidia nchi kuendelea na mipango yake ya uchumi wa blue na kukuza taasisi za kifedha,"anasema Urpilainen.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaeleza vita hiyo imepunguza akiba ya fedha za kigeni nchini kwa kuwa kiasi kilichopo kinatosheleza kuagiza bidhaa kwa miezi minne na wiki mbili, ikiwa ni muda mfupi kwa zaidi ya miaka mitano iliyopita.

Kiwango hicho ni cha chini ikilinganishwa na takwa la Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), inayotaka angalau miezi minne na nusu huku Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) inataka ya miezi sita.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya BoT ya Sera ya Fedha iliyokutana Novemba 28, mwaka huu, kutathimini hali ya utekelezaji wa sera ya fedha na mwenendo wa uchumi wa taifa, kiwango cha utoshelevu wa fedha za kigeni katika kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kinatarajiwa kuongezeka kutokana na kuendelea kupungua kwa bei za bidhaa kutoka ng'ambo.

Chini ya Mwenyekiti Gavana wa BoT, kamati inabainisha kuwa mara ya mwisho akiba ya fedah za kigeni kupungua hadi miezi 4.2 ilikuwa Februari 2017 wakati akiba ilikuwa Dola bilioni 4.35.

Akiwasilisha bajeti ya mwaka 2022/23, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, anasema vita hivyo vimeathiri nchi kutokana na kupungua mafuta, unga wa ngano na mafuta ya kula.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, anasema Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), imeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola milioni 75 sawa na Sh. bilioni 175.5, kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa pembejeo za kilimo.

"Mradi unalenga kuongeza mifumo ya uzalishaji wa chakula nchini ili kupunguza athari za muda mfupi na mrefu kutokana na mgogoro wa Ukraine, Urusi na mabadiliko ya hali ya hewa,"anasema.

Baadhi ya wataalamu wananukuliwa wakisema vita hivyo vimeiathiri zaidi Afrika kwa kuwa hali ngumu ya uchumi imeongezeka na sasa bei ya bidhaa inazidi kupaa.

Mtaalam wa masuala ya fedha wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Tobias Swai, ananukuliwa akieleza kuwa kuongezeka kwa mzozo wa kijiografia kati ya Urusi na Ukraine, kunaifundisha dunia hususan nchi za Afrika kuwa na uchumi wa kujitegemea hasa kwenye bidhaa muhimu.

Anasema ni muhimu nchi kuacha kutegemea kuagiza nje hata wanavyoweza kuzalisha huku akitolea mfano wa vyakula vinavyoweza kupatikana nchini kwa wingi, jambo ambalo litasaidia kuimarisha akiba iliyopo.

# 'Watanzania kuchezea nembo ya taifa kutawapeleka gerezani'

**Na Thobias Mwanakatwe,SINGIDA**




Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Profesa Elisante Ole Gabriel, akiwasilisha mada wakati wa mafunzo.**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

TANGU Tanganyika na Zanzibar ziungane Aprili 1964 na kuundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maadhimisho na sherehe mbalimbali za kitaifa yamekuwa yakishuhudiwa kila wakati.

Hata hivyo, pamoja na kuandaliwa na kufanikishwa uendeshaji wa masuala ya maadhimisho unaofanywa na watumishi wanaosimamia itifaki umekuwa na upungufu kutokana na kutokujua sheria, kanuni, miongozo na taratibu.

Ili kubadili hali hiyo Kitengo cha Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa Ofisi ya Waziri Mkuu hivi karibuni kinawafunza Wakurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka wizara, idara na taasisi za serikali na makatibu tawala wasaidizi wa mikoa yote ili kufanikisha azma hiyo.

Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Batholomeo Jungu,akizungumza katika mafunzo hayo yanayofanyika mkoani Singida anaeleza kuwapo tatizo eneo la itifaki ya viongozi katika kutambua viongozi, wahusika kujua wajibu wao na hata muonekano akisema ukiwa kiongozi unavaaje, unakulaje kwenye tukio la viongozi wa kitaifa.

Jungu anasema kutokana na hali hiyo , Kitengo cha Maadhimisho na Sherehe za Taifa kimeandaa mafunzo hayo ili wahusika wafahamu itifaki ya viongozi kwenye matukio ya kitaifa.

Aidha, kuhusu washereheshaji ma-MC binafsi kuendesha shughuli za kitaifa, anasema serikali inapaswa kuwa na ma-MC wake wanaojua itifaki za viongozi lakini kumekuwa na tatizo katika kuwapata ambapo mchakato wa mafunzo umeanza kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa ili kuwatengeneza.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Exavier Daudi, anasema mafunzo hayo yanafanyika kukabili upungufu mkubwa kwenye itifaki.

"Watendaji wetu wanapenda kufanya kazi kwa mazoea wakati serikali tunafanya kazi kwa kuzingatia sheria,kanuni, miongozo na taratibu hivyo mafunzo haya yatawafanya wabadilike na kuanza kufanya kazi kwa kufuata maelekezo."

Daudi anasema baada ya mafunzo haya wakurugenzi wa utawala na usimamizi wa rasilimali watu walioshiriki wataanza kupimwa kama wanafanya kazi kwa utofauti au kwa mazoea.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, anasema katika suala la uwekaji wa bendera na matumizi ya alama za taifa kama vile wimbo wa taifa, amegundua kuna ubabaishaji mwingi na kuelekeza viongozi hao kusimamia mabadiliko.

Takribani washiriki 250 kutoka mikoa yote walishirikia mafunzo hayo ambayo mada za ulinzi na uslama kwenye matukio yanayohusu viongozi wa kitaifa, elimu ya majanga, maadili uratibu wa itifaki ziliwasilishwa.

George Lugome, ni Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, akiwa miongoni mwa watoa mada anasema wapo wanaotumia nembo ya taifa kujinufaisha katika biashara zao, akisema wanatenda kosa kwa mujibu wa sheria na hivyo wakibainika wanaweza kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini.

Anawaambia kuwa kuna watu wanachukua nembo ya taifa ambayo ni ngao ya uhuru na umoja , kwenye mtandao ambazo wamezitengeneza bila kufuata vigezo ambavyo sheria ya alama za taifa inasema na sheria inaeleza anayetumia alama za taifa isivyo sahihi anafungwa jela miaka miwili au faini.

Anaongeza kuwa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu ndiyo yenye jukumu la uchapaji wa nyaraka zote za serikali lakini pia inasimamia alama za taifa kama nembo ya taifa, bendera na wimbo wa taifa.

Lugome anasema alama za taifa zinakwenda sambamba na itifaki kwani kwenye itifaki ndiko alama hizo hutumika.

Anaongeza kuwa ofisi yake kabla ya kuanza kuwachukulia hatua watu wanaotumia ovyo alama za taifa imeanza mpango wa kutoa elimu kwanza ili kama kuna walikuwa wakizidandia alama hizo kujinufaisha kibiashara wanafanya kosa ambalo linaweza kuwafikisha jela.

"Hivi sasa kuna tatizo alama za taifa zinatumika isivyo sahihi, na pia unaweza kukuta bendera ya taifa inashushwa lakini watu wanatembea hawajali. Yote hayo tutaanza kuwakumbusha kwenye elimu ya uraia na kuwafikia mitaani pia."

> "Majukumu ya kazi ya ofisa rasilimali watu ni pamoja na kuangalia kama kuna urasimu katika ofisi, pia kama Waziri au Katibu Mkuu anachelewa kutoa maamuzi aelezwe maana ninyi ni wakurugenzi rasilimali watu ni maofisa wakubwa wa mna jukumu la kuwasimamia viongozi," anasema Simbachawene.

Kuhusu suala la kuvuja nyaraka za serikali, anasema limekuwa likijitokeza sana na linasababishwa na kutokufuata utaratibu kwa kuchapa nyaraka sehemu zisizoruhusiwa.

Lugome anasema nyaraka za serikali zina alama za kiusalama na inaendelea kujiimarisha kwenye eneo hilo kwani upo uwezekano wa baadhi ya alama kughushiwa sababu hakuna alama za kiusalama," anasema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, akifunga mafunzo hayo anasema moja ya mambo ambayo yanasababisha sekta ya umma isiwe na ufanisi ni ucheleweshaji kutoa maamuzi na urasimu.

"Majukumu ya kazi ya ofisa rasilimali watu ni pamoja na kuangalia kama kuna urasimu katika ofisi, pia kama Waziri au Katibu Mkuu anachelewa kutoa maamuzi aelezwe maana ninyi ni wakurugenzi rasilimali watu ni maofisa wakubwa mna jukumu la kuwasimamia viongozi," anasema Simbachawene.

Anawaambia washiriki kuwa watumishi lazima watambue kuwa kama mifumo haifanyi kazi vizuri wakurugenzi wa rasilimali watu wahakikishe wanawapima viongozi waliopo chini na juu wanavyofanya kazi na kuchukua hatua ili kuleta ufanisi wa kazi serikalini.

"Ninyi ndiyo wenye nyumba, mnaoweka misingi na mifumo ya kuhakikisha hata viongozi waliopo juu wanafuata utaratibu wa misingi na sheria, mifumo isiposhikiliwa vizuri maana yake serikali inaonekana haifanyi kazi kikamilifu."Anakumbusha.

Simbachawene anasema katika suala la itifaki kumekuwa na mikanganyiko mingi wakati wa maadhimisho, sherehe na matukio ya kitaifa hivyo ni lazima kuwa mkakati ili kuwe na utaratibu.

Anasema mafunzo endelevu kwa mtumishi ni muhimu katika kuwaendeleza kwenye ma eneo ya kiutendaji, kumkumbusha mambo muhimu ambayo wanapaswa kuyatekeleza katika majukumu ya kila siku pamoja na kuwezesha kubadilika kutokana na mabadiliko ya sera, itikadi, sheria na mazingira ya wakati.

"Ni imani yangu kuwa mafunzo haya yameboresha na kuwapatia ufahamu na ujuzi muhimu wa namna ya uandaaji wa maadhimisho yanayohusu idara na taasisi za serikali kwa viongozi wakuu, wa kitaifa na kuzijua kanuni za kiitifaki ambazo mtazitumia katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali kwenye ofisi zenu na maisha binafsi," anasema Waziri.

# Viwanda simu za mkononi vinavyoleta kiama DRC

## •Kwa wazalishaji ‘bora Mkongo’ afe lakini simu ziwepo




Karim Ben Khelife, mwandishi na mpigapicha mtetezi wa Wakongo, akiwa jukwaani kuelezea madhila yao. **PICHA: SEVEN GRAMS.**

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

KINACHOENDELEA nchini DRC kinasikitisha .Watoto, vijana na wazee wanaangamia kisa ni madini yanayotumika kutengeneza vitu muhimu zaidi duniani leo, ni simu za mkononi na kompyuta. Kwa ujumla vifaa vya kielektroniki.

Ni pamoja tungsten’, kobalti, ‘cassiterite’ (madini jamii ya bati) na dhahabu.

Mwandishi wa habari za kivita Karim Ben Khelifa, mwenye asili ya Ubelgiji na Tunisia, ndiye anayeitangazia dunia kuwa simu wanazotumia leo na vifaa vya kielektroniki viwe magari, kompyuta, TV au mitambo ni msiba na mauti kwa raia wa DRC.

Ben Khelifa, ameunda programu kwenye mtandao inayowaonyesha watumiaji wa simu kile kinachoendelea DRC nchi inayozalisha madini yanayounda simu zao na bidhaa za kielektroniki.

DRC yenye umaskini uliokithiri licha ya utajiri mkubwa wa rasilimali lukuki, raia wake wakiwamo watoto wa kiume na vijana wanalazimika kufanya kazi kwa waasi wenye silaha wanaodhibiti migodi ya madini ya thamani yanayotengeneza bidhaa hizo.

Ili kuibua taswira anaita program hiyo ‘Seven Grams’ gramu saba, zinahitajika kutengeneza iPhone na vifaa vingine vya sauti kwenye simu, mwandishi anaonyesha ujumbe huo ambao unakemea kutengeneza simu kwa mali ghafi haramu na udhalimu.

Programu hiyo unapoibonyeza inaleta picha ya simu ya mkononi ukibofya inalipuka vipande vidogo vinavyoonekana kuelea angani kisha dunia inayozunguka inaonekana, ujumbe unakuja karibu kwenye dunia ya ukweli unaodhabitiwa.

Kuanzia hapo, sauti yake inaelezea ‘gramu saba’ , habari ya madini ya thamani yanayotengeneza simu yako na muhimu zaidi anataja yanatoka Congo na jinsi yanavyofika viwandani.

Ben Khelifa amekuwa DRC akiripoti kuhusu mambo tofauti kuanzia 2015 alipopata fursa ya kutembelea migodi ya madini mashariki mwa nchi hiyo na kugundua ilivyo jehenamu kwa Wakongomeni wengi.

Programu ya ‘Gram Saba’, Khelifa anamwonyesha mtoto anayeitwa Chance, ambaye, kama jina lake lilivyo ni mmoja wa waliobahatika kuchukuliwa na kuandikishwa kuwa askari wa waasi wa Mai-Mai, walioko mashariki mwa DRC, lakini Chance alitoroka na kunusurika.

**HAKUNA ULINZI/MSAADA**

Kuna maelfu kama Chance wamenaswa migodini, inayoendeshwa kinyume cha sheria imetapakaa kila mahali, ni ukiwa na umaskini wanaishi kwenye vibanda vya muda vilivyojengwa kando ya mlima.

Watoto wavulana, vijana na wanaume huzama migodini kwa saa 12 kila siku kuchimba miamba kwa mikono ili kupata madini yanayounda simu, TV , betrii zenye nguvu na maelfu ya vifaa vya kielektroniki.Wamefunikwa na vumbi muda wote, mshahara wa kila siku ni kiduchu si zaidi ya bei ya chupa mbili za maji pengine dola moja au Shilingi 2,000.

> “Programu ya ‘Gram Saba’, Khelifa anamwonyesha mtoto anayeitwa Chance, ambaye, kama jina lake lilivyo ni mmoja wa waliobahatika kuchukuliwa na kuandikishwa kuwa askari wa waasi wa Mai-Mai, walioko mashariki mwa DRC, lakini Chance alitoroka na kunusurika.

Kwenye kuta za nyumba zao, anaonyesha buti za mvua zilizopasuka, suruali zilizochakaa ambazo hazijafuliwa kwa miezi kadhaa, mapanga yenye kutu na magunia ya kulalia hakuna vifaa vya kuwalinda wachimba madini hayo dhidi ya vumbi la sumu.

Ndani ya miamba anaonyesha vipande vya madini ya ‘tungsten’, kobalti, ‘cassiterite’ (madini ya bati), lakini pia upo mwamba wenye kipande kidogo cha dhahabu. Vyote makampuni makubwa yanahangaika ili kuvipata na kuzalisha simu na vifaa ghali vya kielektroniki , lakini kwa gharama ya chini mno ikiua Wakongo.

Anaeleza kuwa huko ni kuiba madini ya DRC na kuwaangamiza wananchi wake maskini.

Migodi hiyo inadhibitiwa na vikundi vya waasi vinavyoshindana, ambavyo huuza madini hayo kupitia mtandao ya njia za panya, masoko na mwisho kutinga kwenye viwanda vya makampuni ya kimataifa ya simu na vifaa vya kielektoniki kama Apple, Samsung na Huawei, pamoja na makampuni mengi ya magari.

Katika makala maalumu Ben Khelife anauliza inawezekanaje kwamba DRC, yenye madini yanayokadiriwa kuwa na thamani ya karibu dola trilioni 24 za Marekani, inashikaje nafasi ya 175 kati ya nchi 181 fukara mno kwenye Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu (Human Development Index) ?

Utafiti wa kijiolojia wa Marekani wa mwaka 2019 unaonyesha kuwa DRC inazalisha tani 100,000 za ‘cobalt’ inayotumiwa kuzalisha vifaa vya kielektroniki duniani, ikilinganishwa na tani 6,100 za Urusi, ikifuatiwa na tani 3,000 za Canada.

“Kwa hakika ninataka kufundisha watu, lakini pia nataka kuwapa suluhisho, sio tu kuwaambia kwamba kuna shida na simu na vifaa vya elektroniki kwa ujumla,” anasema Ben Khelifa.

Kwa kufichua mazoea ya biashara, watumiaji wanaweza kuchagua kununua bidhaa zinazotoka kwa watengenezaji ambao hawanunui metali zao kutoka kwenye migodi isiyo halali, na wanaochagua kuchakata badala ya kuzalisha malighafi zaidi.

Ben Khelifa anasisitiza kuwa sasa huwezi kusema hukujua ni wewe na moyo wako.

Makala hiyo ‘Seven Grams’ iliyotayarishwa kwa Kiingereza na Kifaransa ni uzoefu wa uhalisia ulioboreshwa na Karim Ben Khelifa, akifanyakazi kwa pamoja na kampuni za LucidRealities, France TV Lab, POV Spark na Think-Film, inaweza kupakuliwa bila malipo na Google Store na Apple play na mtu akaisoma kufahamu kilio kilichoko DRC.

**CONGO KUFIDIWA**

Katika mwendelezo wa kuibuliwa taarifa za unyama na udhalimu dhidi ya WaDRC na mali zao, kampuni ya Glencore ya Uswizi , Jumatatu wiki hii imetangaza kulipa dola milioni 180 (CHF milioni 168) kwa DRC kama sehemu ya makubaliano yanayohusu madai yote ya sasa na yajayo ya madai ya ufisadi yaliyofanywa na kampuni ya uchimbaji madini nchini humo kati ya 2007 na 2018.

Kikundi cha biashara ya bidhaa na uchimbaji madini kilisema makubaliano hayo yalihusu madai ya rushwa ikiwa ni pamoja na shughuli katika “biashara fulani za vikundi ambazo zimekuwa zikichunguzwa na, miongoni mwa wengine, Idara ya Haki ya Marekani na Kitengo cha Kitaifa cha Ujasusi wa Kifedha cha DRC na Wizara ya Sheria” .

Kampuni hiyo ilituhumiwa kwa madai ya rushwa ikiwa ni pamoja na shughuli katika “biashara za vikundi ambavyo vimekuwa vikichunguzwa na, Idara ya Haki ya Marekani na Kitengo cha Kitaifa cha Ujasusi wa Kifedha cha DRC na Wizara ya Sheria.

Kalidas Madhavpeddi, mwenyekiti wa Glencore, anasema kampuni hiyo yenye makao yake Zug Uswiss inafurahi kufikia makubaliano haya “ambayo yanashughulikia matokeo ya vitendo vyake vya kihalifu vya zamani”.

Glencore, inamiliki migodi ya shaba, nikeli na makaa ya mawe karibu duniani kote na ina kitengo kikubwa cha biashara ya bidhaa, lakini imekabiliwa na tuhuma nyingi na kufanyiwa uchunguzi mara kadhaa kuhusu shughuli zake za kimataifa.


Mwaka wa 2018, Idara ya Haki ya Marekani ilichunguzi kampuni hiyo na kuitaka kukabidhi rekodi zinazohusiana na kufuata sheria za utakatishaji fedha za nchi hiyo na Sheria ya Ufisadi wa Kigeni katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Nigeria na Venezuela.

***REUTERS & Radio France International- rfi***

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ruto, Gachagua watoa somo sera za kuwafikia vijana

•Waunda mfuko serikali kujazia kila kinachowekwa



Rais William Ruto, (kushoto) na Naibu Rigathi Gachagua, wameanza mkakati wa kunusuru vijana. **PICHA: DAILY NATION**

**Na Ani Jozeni**

RAIS William Ruto wa Kenya na Naibu wake Rigathi Gachagua tayari wameanza kuingia katika mipango inayolenga kundi kubwa zaidi la wapiga kura wao, yaani vijana wa mijini na vijijini walioelewa kuwa aliwahi kuwa na maisha kama yao na kwamba aliahidi kuwasaidia.

Anatangaza kuunda mfuko wa vijana kuwekeza akiba zao na serikali kuwaongezea, ili wapate mtaji wa kujiajiri kwani wakati wa kampeni, mgombea alijitambulisha kama 'hustler,' sawa na mmachinga.

Aliwaona aliyekuwa rais Uhuru Kenyatta na mgombea Raila Odinga kama watu waliozaliwa na kukulia katika familia kubwa, wasiowajua wanyonge.

Kukubalika kwa picha hiyo ya Raila ilikuwa ni aina ya kufanya mapinduzi katika utamaduni wa kisiasa nchini humo, kwani baba wa Raila, Jaramogi Odinga, alikuwa ni mwanamapinduzi asilia aliyesimama kijasiri kukataa uhuru wa Kenya hadi Jomo Kenyatta aachiwe huru.

Alikuwa kizuizini Lodwar, kaskazini ya nchi hiyo na hilo ni moja ya sababu zilizoleta umoja kati ya Uhuru na Raila, licha ya Jaramogi kukosana na Mzee Kenyatta kwa masuala ya sera, ya ubepari na ukabaila wa kujigawia mashamba walivyotaka jambo lililokuwa kama kukana harakati za ukombozi.

Upande mwingine wa mabadiliko ya kisiasa ni kuanza kutokomea kisiasa kwa kundi la vijana ambao kimsingi hawana kazi au uhakika wa kujikimu, lakini wanajitambulisha kikabila kama warithi wa harakati ya MauMau, miaka ya 1950, wakiitwa mungiki.

Hawa walitumika katika mapambano ya kuzuia mabadiliko ya utawala kuondoka kwa rais wa awamu ya tatu Mwai Kibaki, kwenda kwa mgombea wa upinzani Raila Odinga, mwaka 2007.

kundi hilo halikufaulu kujizatiti muhula wa pili wa Kibaki na hata wakati wa Uhuru, hivyo wanaungana na mpiganaji, pamoja na 'mungiki' wengine wa kisiasa wakati huo wakiunganishwa na mpiganaji Ruto.

> Bado kutakuwa na mtihani wa uendeshaji wa mfuko huo wa hazina kama vijana wote watafikiwa na fedha za serikali na mfuko unaendeshwa kwa njia ya mitandao.

Viongozi hao wa 'mungiki' tofauti waliunganishwa katika kesi ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) huko The Hague kutokana na watu takribani 1, 000 kuuawa wakati wa machafuko yaliyofuatia uchaguzi mkuu wa 2007.

Kesi hiyo ikakwama wakati mashahidi wakiuawa au kupotea, na si zaidi ya miezi miwili sasa shahidi mmoja aliyekuwa anahitajiwa The Hague naye akauawa.

Kitengo cha polisi kilichohusika na mauaji tofauti maeneo ya pwani, hivyo inadhaniwa walihusika pia kuondoa mashahidi wa kesi za Ulaya.

Kuundwa kwa mfuko huo kunaweza kutafsiriwa kuwa ni jitihada ya kuzuia upinzani kuanza kuwakusanya vijana kuhusu mapungufu ya utawala wa sasa, kwani yako maswali yanayoibuliwa kuhusu hatua tofauti.

Yapo masuala ya kisheria kwa mfano hitaji la kuchunguza kazi za kitengo hicho cha polisi ambayo itakuwa sumu kwa waliokuwa madarakani (akiwapo Ruto kama Naibu Rais).

Kuundwa mfuko huo ni kuopoa vijana kabla 'baba' Raila hajaanza kutoa maelekezo. Somo ambalo linaweza kusaidia Kenya na kwingineko ni 'ongezeko la thamani' katika sera mpya, kwa mfano hapa nchini sera ni kuwakopesha vijana, wanawake na wenye ulemavu asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Vijana na kinamama wanapata asilimia nne kila mmoja wakati wenye ulemavu wanapata asilimia mbili, halafu fedha hizo zinatakiwa zitumike zirudishwe na pale vijana au wanawake na wenye mahitaji maalum, wakichelewesha malipo malalamiko yanaibuka.

Mpango wa Ruto na Gachagua ni tofauti. Wao wanaweka fungu la fedha kuwezesha vijana kuingia katika mfuko na kuweka fedha kama mtaji. Akiingiza shilingi mbili, serikali inaweka moja ni kwa walalahoi pekee wanaruhusiwa wakati wenye fedha au wafanyabiashara wakitakiwa kwende benki.

Bado kutakuwa na mtihani wa uendeshaji wa mfuko huo wa hazina kama vijana wote watafikiwa na fedha za serikali na mfuko unaendeshwa kwa njia ya mitandao.

Ipo hatari ya kupenya majina ya wale wanaotakiwa kutumia benki kwani wanatoka familia zinazojimudu, na hilo litategemea usimamizi wa uendeshaji wa mfuko huo, na kama waendesha mitandao wanaona udhaifu wa dhamira au udhati wake katika hatua za mwanzo. Wakigundua kuna udhaifu ni wazi kuwa wataingiza wasiotakiwa.

Katika ngazi hiyo kuna mvutano ambao utajitokeza kiutendaji, na siyo jambo la kushangaza kama mvutano huo utaonekana hata ndani ya serikali, kuangalia nini wanakifanya.

Wapo watakaoona kuwa suala hapa ni kuwavuta vijana kwa jumla ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kupata kura zao kwa nguvu wakitafuta muhula wa pili, na vurugu za baadaye zikizuka ziwe ni za wanasiasa, ambao hawatafua dafu mbele ya walio madarakani bila kuwavutia vijana vya kutosha.

Ila kuna ambao hawatakuwa na mwamko huo kuanzia mwanzo, watake kuwazawadia wafuasi wao, wajazie walalahoi pesa kwa kuwarubuni, watengeneze ziada haraka.

Jitihada kama hizo zinazonekana maeneo mengi ambako mivutano ya kisiasa ni ya nguvu, kwa mfano jitihada za kutoa boti kwa wavuvi na wakulima wa mwani na maelezo yake hayasemi kuwa wanakopeshwa au watarudisha mikopo kwa njia gani.

Wapowaliopata pikipiki za kujikumu katika mazingira sawia, ambako serikali kuu inawezesha fedha halafu mengine yasimamiwe na serikali za mitaa.

Ila kwa upande wa Bara, yaani serikali ya Muungano, jitihada zinalenga uungwaji mkono wa serikali kwa jumla na siyo hasa makundi maalum, licha ya kuwa mahitaji maalum yanaongezeka.

Kina mifuko na mipango ambayo imeanza na vyuo vikuu ili kuwavuta vijana wahitimu katika kilimo, mifuko ikiwa inalenga kupata vifaa na mbegu bure. Ni mipango tofauti na mikakati sawia.


MIAKA 61 YA UHURU

# Tanzania bado inabanwa utegemezi kiteknolojia, unazidi kufifisha maendeleo

INATOKA UK. 13

unaowanufaisha ili iwe fursa ya kunufaika na pia wanaweza kuandaa taarifa za kufurahisha serikali lakini ambazo huenda zimekuzwa na kupambwa kwa lengo la kufanikisha mipango yao ili kuleta mitambo na mashine na teknlojia ambazo kwenye mataifa yao hazitumiki, yote hayo yanaweza kulisababishia taifa hasara.

Ni vyema taifa kufikiria kuanza kuwatumia wataalamu wa Tanzania ili isiwe tena gharama kubwa na kazi ngumu ya kugharamia zaidi changamoto kama hizo zinapotokea kwa vile zinakwamisha maendeleo na kuongeza gharama.




**KAZI IANZE SASA**

Tanzania inapofurahia miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika ni wakati wa kuwekeza zaidi kwenye teknolojia ya kisasa kwa kufundisha na kutumia wataalamu na mbinu za ndani wapewe fedha, mitaji na fursa ya kugundua teknolojia zao, kuziboresha na kuziendeleza na serikali igharamie kwa namna zote siyo kutegemea wahisani.

Kwa mfano, kwenye umeme ni vyema kuwa na vyanzo vingi vya nishati hasa jadidifu kama upepo na jua na kutengeneza teknolojia ya kuitumia bila kutegemea zaidi wataalamu kutoka nje, ambao wanaweza kuchangia kusuasua kwa mipango.

Mathalani tasnifu (Thesis) ya utafiti ulioangazia kukatika kwa umeme Tanzania iliyoandaliwa katika Chuo Kikuu cha Darmstadt cha Ujerumani mapema mwaka huu, inaeleza kuwa ni vyema kuanzisha vituo vya umeme wa upepo kwa kutumia teknolojia inayogunduliwa na kuzalishwa nchini .

Inasema, hatua hiyo itaondoa adha za kuagiza na kuchonga vipuri nje, wahandisi wa kigeni kukarabati na kusimamia kwa muda wote wa uhai wa mashine hizo, kupoteza mitambo endapo tatizo litatokea bila kujali athari za kijamii na kiuchumi na wakati mwingine kupewa taarifa za kitaalamu za kukanganya na kudanganya kwa vile nchi haiwezi kufanya lolote.

"Kwa mfano inawezekana kuwa na maeneo ya kusambaza umeme wa jua mkoani Dodoma. Ni jiji lenye jua kali zaidi muda wote. Umeme jua unaweza kusambazwa mikoa yote ya kanda ya kati hata mpaka Kagera lakini cha muhimu ni kutumia wataalamu na paneli zinazoundwa nchini." Inaongeza sehemu ya utafiti huo uliofanyika Chuo Kikuu cha Darmstadt.

Pamoja na umeme jua na upepo suala la kutumia vyanzo vingi zaidi vya nishati kwenye gridi ya taifa kama makaa yam awe, gesi asili na nyuklia pia yanatajwa na kupewa kipaumbele.

Teknolojia linabaki kuwa jambo la kipekee na muhimu kwa maendeleo ya sekta zote. Licha ya kwamba juhudi zimefanywa lakini vikwazo na changamoto zinazoambatana na 'siasa' za usambazaji na matumizi ya teknolojia duniani ni kubwa na zinaelekea kufifisha maendeleo hivyo kuwekeza kwenye utafiti wa nishati ni jambo lisilokwepeka.


Kwa miongo sita ya uhuru ni wakati wa kufikiria kuachana na utegemezi wa teknolojia kwa sababu wakati mwingine msaada wa kiteknolojia unaweza kuleta mitambo na vifaa ambavyo havitumiki kwenye mataifa yaliyoizalisha na kuifa Afrika au Tanzania kuwa dampo la kuitupia na yote hayo ni hasara kwa nchi ambayo imetumia fedha nyingi kuinunua na kugharamia utunzaji, ukarabati na uendelezaji wake.

## CHEMSHABONGO NA -00 27 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Upungufu wa kitu
5. Mlima wa pili kwa urefu nchini
7. Kuwa na imani na mtu
8. Mzazi wa kiume wa Baba
9. Lugha ya Pakistani
10.kuwa katika usingizi
12.Maoni ya mtu
14.Mja 15.Thabiti
17.chombo cha kukumbia maji katika mtumbwi
18.kijana wa kwanza kutahiriwa jandoni
19.weza kuonekana madukani


Chini:
1. Taarifa
2. Pengine, labda
3. Kitabu cha Mungu
4. Toa nguo kwenye kamba
5. wingi wa neno ua
6. Utundu
11.Tokwa na machozi
13.Elezwa
14.Jambo linalozungumzwa
16.Pesa ya Omani 17.barabara




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MAKINDA
MKOKOTENI
OMANI
ANGUSHA
WAGANGA
MASAA
KIATU
UWANJA
FUNGU
JANA
GANA
NAWA
NYIKA
TAKA

ADAH
AGUA
BAO
FAA
MDA
EDA
AUA
AU
UA




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P | A | N | I | A | | | H | U | A |
| A | M | A | N | I | S | H | A | | S |
| K | A | N | A | N | A | | I | | K |
| A | L | A | M | I | N | A | | D | A |
| T | I | S | A | | A | | K | A | R |
| A | | I | | S | A | F | A | R | I |
| | S | | | I | | U | T | I | |
| K | H | O | I | K | H | O | I | | U |
| | I | | | I | | N | | | F |
| G | A | N | D | A | M | I | Z | W | A |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | A | B | A | | K | A | B | L | A |
| U | S | A | W | A | | | A | | L |
| N | I | N | I | | S | O | N | Y | A |
| G | A | G | A | Z | I | | G | | M |
| E | | U | | A | M | B | I | W | A |
| | | | U | M | B | A | | I | |
| K | | M | | A | A | L | I | M | U |
| A | | A | | N | | A | | B | |
| W | I | M | B | I | | S | T | O | O |
| I | | B | | | | I | | | V |
| A | G | O | S | T | I | | U | T | U |





# Hospitali yaanzisha kituo kulea watoto

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), imeanzisha kituo cha malezi kwa watoto wa watumishi wa hospitali ili kusaidia watoto kupata uangalizi wa karibu sambamba na kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

**Mpango huo utaongeza ufanisi katika kazi na kwamba itawasaidia wazazi hao kuwahudumia kwa ukaribu watoto wao.**

Akizungumza ofisini kwake jana Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema mpango huo utasaidia kuongeza ufanisi wa kazi kwa mtumishi.

Alisema mpango huo pia utapunguza ruhusa kwa watumishi kwa kigezo cha kutokua na dada wa kazi au kuchelewa kufika kazini kwa wakati kwa madai ya kumhudumia mtoto.

"Kituo hiki kipo eneo la hospitali, kitakua na waangalizi wa watoto wenye taaluma hiyo ikiwamo ya ualimu kwamba watumishi watapata fursa ya kwenda kumuona mtoto kwa ajili ya kumnyonyesha hadi pale utakapofika muda wa kurudi nyumbani," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema matamanio ya mkakati huo ni kumlinda mtoto dhidi ya hatari ambazo zimekuwa zikiripotiwa majumbani lakini pia itaongeza tija ya utendaji wa kazi wa watumishi na watoto watapata fursa ya kufundishwa, kucheza michezo mbalimbali na kupumzika.

Felister Saria alisema mpango huo utaongeza ufanisi katika kazi na kwamba itawasaidia wazazi hao kuwahudumia kwa ukaribu watoto wao.

Alisema usalama wa watoto utakuwa wa uhakika kuliko ilivyo sasa, kwamba huingiwa na hofu ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wakiwa nyumbani.

Daniel Kajane alisema ruhusa zitapungua kwa watumishi waliokuwa wakidai kuwahi kurudi nyumbani kwa kigezo cha kuwahudumia watoto wao ambao kwa kiasi kikubwa wanahudumiwa na wadada wa kazi.

## Wanaopinga ukatili watakiwa kutetea haki za watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU Tawala Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, ametoa wito kwa wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia kuweka juhudi katika kulinda na kutetea haki za watoto wa kiume sawa na ilivyo kwa watoto wa kike.

Akizungumza na Nipashe jana, Mpogolo alisema wadau na wanaharakati wa masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia wamejikita kulinda na kutetea haki za mtoto wa kike pekee huku mtoto wa kiume akisahaulika hali inayosababisha watoto wengi wa kiume kulawitiwa au kufanyiwa vitendo vingine vya ukatili wa kijinsia.

Alisema kuna tatizo kubwa la watoto kufanyiwa vitendo vya ulawiti katika maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni hali inayotishia usalama wao, akashauri kuongeza juhudi katika kutetea na kulinda haki za watoto hao.

"Vitendo vya ukatili wa kijinsia sasa vimeshamiri zaidi kwa watoto wa kiume kulawitiwa, wazazi na jamii tuwekeze nguvu kubwa kumlinda mtoto wa kiume maana juhudi kubwa imewekezwa kwa mtoto wa kike," alisema Mpogolo.

Alisema wadau mbalimbali wanao wajibu wa kushirikiana na serikali kuendeleza mapambano ya dhidi ya ukatili wa kijinsia kwani yanachangia uwapo wa maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi na kupunguza nguvu kazi ya Taifa.

Aliongeza kuwa wazazi na walezi wanao wajibu wa kuwalea watoto wao katika maadili mazuri pamoja na viongozi wa dini na wa mila kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa watoto huku akishauri kupambana na umaskini kama njia ya kuepuka maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Mbeya, Insekta Loveness Mtemi alisema Jeshi la Polisi linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto wa kiume.

Alisema licha ya kutoa elimu pia wanawahamasisha wananchi kuripoti matukio ya ulawiti katika maeneo yao bila kujali undugu au ukaribu wa watu wanaofanya matukio hayo.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization, Prisca Ngweshemi, akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi za kata ya Mipeko, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazalishaji mbolea asili wataka uhamasishaji kilimo ikolojia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZALISHAJI wa mbolea za asili na wakulima katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wameomba serikali kutunga sera itakayohamasisha matumizi ya kilimo Ikolojia.

Wamesema hali hiyo ambayo itahamasisha matumizi ya mbolea hiyo katika uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini na kusaidia kutunza mazingira.

Rai hiyo ilitolewa juzi na wakulima pamoja na wadau wanaohusika na uzalishaji wa mazao mbalimbali wakati wa kikao cha kujadiliana ni kwa namna gani kilimo cha Ikolojia kinaweza kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija na kuongeza rutuba kwenye udongo.

Walisema utungaji wa sera unaweza kuwa msaada kuhamasisha kilimo hicho wakidai utekelezaji wake utakuwa rahisi kwa sababu serikali ndiyo yenye wajibu.

Halfan Bwigane, anayejishughulisha na kilimo cha mpunga katika Kijiji cha Ndobo wilayani Kyela alisema kuwa serikali ikitengeneze mifumo mizuri ya kuboresha kilimo cha ikolojia itamsaidia mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao mchanganyiko na kufufua ardhi iliyokufa kutokana na matumizi ya mbolea zenye sumu.

Alisema kilimo cha ikolojia kupitia mashamba darasa ya mpunga waliyoyaanzisha yameleta matumaini kwa sababu matumizi ya mbolea za asili yanaleta mavuno mengi na yenye ubora ukilinganisha matumizi ya mbolea za viwandani.

Alieleza kuwa kutungwa kwa sera ya kuhamasisha matumizi ya mbolea asilia kwa kuzingatia kilimo ikolojia ili kutunza mazingira kutaleta tija.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Mababu Wilaya ya Kyela, Benjamin Mwaijumba, alisema kuwa uwapo wa kilimo cha ikolojia kimekuwa na tija kwa wakulima kutokana na kuwapo kwa mfumuko wa gharama za pembejeo za kisasa.

"Tulifikiwa na kupatiwa elimu na watafiti wa taasisi mbalimbali za serikali na wakulima walipojaribu kilimo hicho wameona kina tija pia kunachangia kufufua uhai wa ardhi ambayo imeharibiwa na matumizi ya mbolea zenye simu," alisema Mwaijumba.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Mbeya, Adam Mhagama, alisema kuwa maofisa ugani wamekuwa wakihamasisha matumizi ya mbolea za viwandani kuliko mbolea za asili ambazo ni nafuu kwa mkulima.





# Waziri Ndumbaro: Rushwa bado mfupa mgumu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekiri kuwa rushwa bado ni tatizo nchini hali ambayo inaifanya kushindwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuwahudumia wananchi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alibainisha hayo jana jijini hapo, alipokuwa akifungua maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kitaifa 2022.

Alisema: "Nimeeleza hapo juu kwamba Siku ya Maadili na Haki za Binadamu tunayoadhimisha kila mwaka hapa nchini, imetokana na siku mbili tofauti ambazo huadhimishwa kimataifa ambazo ni Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa pamoja na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu."

Aliongeza: "Rushwa ni tatizo katika nchi nyingi duniani hivyo mwaka 2003, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zilikubaliana kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa kila Desemba 9 kuanzia mwaka 2004 ikiwa ni fursa mojawapo kwa kila nchi kutathmini juhudi zake za kudhibiti vitendo vya rushwa."

**Hii ni kwa sababu miradi ya maendeleo hushindwa kufanyika au hufanyika kwa kiwango cha chini kutokana na fedha zinazotengwa kutekeleza miradi hiyo, kuingia katika mikono ya watu wachache.**

Alisema uwapo wa vitendo vya rushwa unaifanya serikali kushindwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuwahudumia wananchi ipasavyo.

"Hii ni kwa sababu miradi ya maendeleo hushindwa kufanyika au hufanyika kwa kiwango cha chini kutokana na fedha zinazotengwa kutekeleza miradi hiyo, kuingia katika mikono ya watu wachache.

"Ndiyo maana serikali yetu imekuwa ikifanya juhudi kubwa, kudhibiti rushwa nchini na ninyi nyote ni mashahidi kwa kuwa mlimsikia Rais Samia Suluhu Hassan, akielekeza TAKUKURU kufanya ufuatiliaji katika miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukabiliana na ubadhirifu ikiwamo rushwa," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema vita ya rushwa bado ni kubwa hivyo wanahabari wanalo jukumu la kutumia vizuri kalamu zao katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kushiriki kwa vitendo katika kuikataa na kufichua vitendo vya rushwa.

"Mtakumbuka kuwa Rais Samia akiwa ziarani Arusha Novemba 23, mwaka huu alizungumzia ahadi ya serikali yake kwa wananchi kwamba ifikapo 2025 nchi nzima itakuwa na umeme kwa asilimia 100 na huduma ya maji kwa asilimia kati ya 95 na 100 mijini na walau asilimia 85 vijijini.

"Lengo hili litafikiwa iwapo kila Mtanzania kwa nafasi yake atatekeleza wajibu wa kikatiba wa kutunza rasilimali za nchi na kuzuia aina zote za rushwa na uvunjivu wa haki za binadamu nchini," alisema.

Alisema unapozungumzia haki za binadamu huwezi kuepuka huduma mbalimbali ambazo mwanadamu huhitaji katika maisha yake ya kila siku.

Kadhalika huduma za afya nchini zimeimarika kutokana na juhudi kubwa ya serikali za kusimamia kwa karibu ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na majengo katika hospitali za wilaya, na za mikoa. Serikali pia, kwa kujali watu wake, imeendelea kutoa elimu bure kuanzia shule za msingi mpaka sekondari kwa lengo la kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye uwezo wa kusoma anapata haki hiyo.

Alisema katika ngazi ya vyuo vya kati na vya elimu ya juu, serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji ili waweze kupata haki ya elimu katika ngazi hiyo.



Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ustawi wa Jamii katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Amina Mfaki (kushoto), akizungumza kwenye kongamano la watu wenye ulemavu, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi. Wengine (kutoka kulia) ni Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) wa mkoa huo, Justuast Ng'wantalima, Makamu Mwenyekiti wa shirikisho mkoa, Hassan Sharifu na Mwenyekiti, Omary Lubuva. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Askofu: Watanzania endeleeni kudumisha amani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Baraza la Makanisa ya Kipentecoste Tanzania, Askofu Dk. Baraka Kihoza, amesema Watanzania wanawajibu wa kudumisha amani iliyoko kwa kuilinda na kuiombea nchi yao ili kuisaidia serikali.

Aliyasema hayo wakati wa ibada maalumu ya maombi ya kuliombea Taifa iliyofanyika kwenye Kanisa la Calvary Assemblies of God Kikuyu Dodoma.

Askofu Kihoza alisema Watanzania wanakila sababu ya kuhakikisha Taifa linakuwa na amani na utulivu badala ya kuachia suala hilo kwa upande wa serikali peke yake.

Askofu huyo alisema hatuwezi kuwa na Taifa linaloendelea bila uwapo wa maombi ya kuiombea nchi hivyo wajibu huo ni wa msingi ili amani iendelee kudumishwa.

Askofu Kihoza alisema Tanzania ina baraka nyingi ikiwamo rasilimali za kutosha ambazo zinazoliingizia mapato makubwa Taifa yakiwamo madini mbalimbali.

Hata hivyo aliwataka waumini wa madhehebu yote ya dini kuendelea kuwaombea viongozi walioko madarakani ili waweze kufanya kazi kwa misingi inayotoka kwa Mungu.

"Waumini kwa kushirikiana na viongozi wa dini wanatakiwa kubeba mzigo huu wa kuwaombea viongozi wetu hao wa serikali, ili waweze kufanya kazi zao kwa hofu na misingi ya kiroho," alisema.

Naye Mtumishi kutoka nchi ya Kenya, Nabii John Sikenga, alipongeza serikali ya Tanzania kwa kudumisha amani na kuiwezesha nchi kuendelea kuwa na utulifu.

Alisema Tanzania inatakiwa kuigwa na kupongezwa kutokana na uhuru na amani iliyopo ambayo watu wake wamekuwa wakifanya shughuli zao za kujiletea mapato na kuinua uchumi wao.

# RC akerwa watu wenye ulemavu kugeuzwa vitega uchumi

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Josephath Maganga, amezitaka jamii zinazoishi na watu wenye ulemavu kuacha kuwatumia kama vitega uchumi kwa kuwaweka barabarani kwa ajili ya kuomba misaada.

Amesema tabia hiyo inawadhalilisha na kuwaondolea utu wao, hivyo jamii inatakiwa kuwajibika kwa kuwasaidia kiuchumi na kimaisha na kuwalinda muda wote.

Alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule, kwenye kilele cha kufunga Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani hapo.

Maganga alisema watu wenye ulemavu wanatakiwa kusaidiwa kiuchumi na kijamii na siyo kuwafanya kitega uchumi kwa kuwaweka barabarani kwa ajili ya kuomba katika maeneo mbalimbali.

"Tabia hiyo kwa kweli inawadhalilisha utu wao kwa kuwafanya kama hawastahili mbele ya jamii, hivyo ninawaagiza tabia hiyo iachwe ya kuwafanya vitege uchumi kwa kuwaweka juani siku nzima ili wapewe misaada kutoka kwa wapita njia," alisema.

Hivyo, aliwataka watu wenye ulemavu wahakikishe wanachangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri zote nchini ili kujisimamia wenyewe kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi wa kila siku.

Vilevile alisema mikopo hiyo ipo kwa ajili yao kinachotakiwa kwao ni kuunda vikundi pamoja na kutimiza vigezo vya kuwawezesha kupata ili wajiendeleza na kutatua kero zao.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Justast Ng'antalima, aliiomba serikali kuwapunguzia makali yaliyoko kwenye mikopo inayotolewa na halmashauri nchini.

Alisema bado kwa upande wao kunaugumu wa kupata mikopo hiyo ya asilimia 10, kutokana na serikali kuwawekea vigezo ambavyo vinavyosababisha kutopata kwa haraka kama ilivyo kwa makundi mengine ya wanawake na vijana.

Alisema: "Kwa wenzetu mikopo hiyo wanaipata kwa urahisi zaidi ila kwetu sisi watu wenye ulemavu bado kuna tatizo ambalo linatukwamisha kuipata mikopo hiyo kwa haraka kama ilivyo kwa wanawake na vijana," alisema.

# Sekta utalii kinara mapato fedha kigeni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SEKTA ya Utalii Zanzibar imekuwa kinara kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni katika uchumi wa visiwa hivyo ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hapsa Hassan Mbamba, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kamisheni hiyo ya Amani visiwani humo.

Alisema kiasi cha asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana na sekta ya utalii na asilimia 29.2 ya uchumi wa Zanzibar unatokana na sekta hiyo.

Alisema wakati wa kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19 hali ya uingiaji wageni ilishuka na kufikia 260,644 kwa sababu wageni walipungua kutokana na maradhi hayo, lakini Zanzibar licha ya kwamba haikufunga mikapa yake.

**Tunataka watalii wenye uwezo wa kifedha kwa ajili ya manunuzi mbalimbali ili serikali kuongeza pato litokanalo na sekta hii ya utalii.**

Alisema kwa mwaka 2021 wageni waliyoingia Zanzibar 364,185, lakini kwa mwaka 2022 hadi Novemba wamefika 322,748.

Alisema malengo ya serikali ifikapo 2025 kuingiza zaidi ya wageni 80,000 na uwezo huo upo na hivi sasa wanajipanga katika kuhakikisha kutangaza utalii katika nchi mbalimbali hasa kupitia wageni wanaofanya mikutano yao Zanzibar.

Aidha, alisema kwa kuwa sekta ya utalii ni mtambuka wamejipanga katika kuhakikisha wanatumia michezo ikiwamo ya baharini ili kuwavuta zaidi wageni.

"Tunataka watalii wenye uwezo wa kifedha kwa ajili ya manunuzi mbalimbali ili serikali kuongeza pato litokanalo na sekta hii ya utalii," alisema.

Hata hivyo, alisema utafiti uliofanywa umeonesha kuwa watalii wengi wanaofika Zanzibar, hutembelea fukwe na sio kufanya utalii wa kutembelea vyanzo vingine vya utalii.

Alisema utafiti huo waliufanya pia umegundua kuwa wageni wengi wanaofika Zanzibar sio wa mara kwa mara wanaotembelea visiwa hivyo kutokana na changamoto mbalimbali hasa kupitia viwanja vya ndege kwa wageni wanaingia na kutoka.

"Changamoto hiyo tayari serikali imeshaifanyia kazi na kwa sasa katika viwanja vyetu vya ndege hakuna usumbufu wowote kwa wageni," alisema.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji na huduma kutoka mamlaka ya vitega uchumi Zanzibar (ZIPA), Shida Makame Kombo, alisema kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kuwapokea wawekezaji wanaofika kuwekeza Zanzibar.

Alisema ZIPA imejipanga kuhakikisha wageni wote wanaofika kuwekeza Zanzibar wanakuwa salama na mali zao na wako tayari kuwapokea wageni mbalimbali.

Alisema katika kuhakikisha maendeleo makubwa kwa upande wao serikali iko katika hatua za kutengeneza bandari kubwa huko maeneo ya Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa wawekezaji wanafika kuwekeza Zanzibar miradi mbalimbali imeshaonesha njia ya visiwa 17 wawekezaji wameonesha nia ya kuwekeza ikiwamo Kisiwa cha Mnemba, Kisiwa cha Misali Pemba na jumla ya Dola milioni 414.50 zitapatikana.

Alisema pia serikali itapata Dola milioni 213.16 kwa ajili ya miradi ya hoteli 30 na Dola milioni 18.26 miradi tisa na miradi hiyo tayari imeshasajiliwa na ZIPA.

## SMZ, Uturuki zasaini mkataba mradi ujenzi wa nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, imetia saini ya makubaliano na Kampuni ya ASER kutoka Uturuki kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa nyumba za maendeleo Zanzibar (Housing Development Projects in Zanzibar).

Hafla hiyo ya utiaji saini wa makubaliano hayo imefanyika mwishoni mwa wiki katika ukumbi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Maisara, Unguja na kusainiwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji na Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Ertan Murat.

Akizungumza baada ya utiaji wa saini, Dk. Mngereza alisema lengo la makubaliano hayo baina ya pande mbili hizo ni kuanzisha mahusiano ya kikazi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za maendeleo na biashara kwa mkopo nafuu.

Alisema, mradi huo unatarajiwa baada ya taratibu zote za makubaliano kukamilika kwa pande zote mbili ikiwamo, mapendekezo ya mradi wa nyumba na gharama zake, taratibu za kisheria, kulipa fidia.

Alisema, Wizara ya Ardhi inatarajia kuwa na mradi mpya wa nyumba za maendeleo Chumbuni utakaojenga nyumba 1,000 kwa awamu.

Awamu ya kwanza zitajengwa nyumba 500 na ya pili nyumba 500 ili kukamilisha idadi hiyo.

Pia alisema mradi huo utajenga nyumba za 50 eneo la Fumba na maeneo ya Mombasa kwa Mchina, mradi utajenga nyumba 48 za ghorofa na nyumba za Mji Mkongwe zitafanyiwa matengenezo.

Naye Naibu Waziri, wizara hiyo, Juma Makungu Juma, alisema Zanzibar kuna mahitaji makubwa ya nyumba na kampuni hiyo imeahidi kujenga nyumba hizo baada ya kukamilisha taratibu zote.

Alisema ujenzi wa nyumba hizo unatarajiwa katika maeneo tofauti Unguja na Pemba na utazingatia kipato cha kila mwananchi ili kuzimudu kwa lengo la kuboresha makazi bora.




Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji (kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya ASER, Ertan Murat (katikati), wakitiliana saini makubaliano ya ujenzi wa mradi wa nyumba za maendeleo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka watumishi kupatiwa mafunzo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, amesema ipo haja kwa watumishi kupatiwa mafunzo ya ulinzi wa mifumo ya kompyuta na kuzuia wizi wa mitandao ili kulinda taarifa za nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya ulinzi wa mifumo ya kompyuta na kuzuia wizi wa mitandao (Cyber Security) yaliyofanyika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST), Mbweni Zanzibar.

Alisema kuna ongezeko kubwa la uwapo wa udukuzi wa taarifa jambo ambalo linaweza kusababisha matatizo mengi katika jamii ikiwamo uvunjifu wa amani.

Alisema endapo watumishi hasa wataalamu wa kompyuta watapata uelewa kuhusu mbinu zinazotumiwa na wahalifu wa mitandao wataisaidia nchi kutunza na kudumisha amani iliyoko.

Aidha, aliwataka washiriki hao kuitumia elimu hiyo katika kuleta maendeleo nchini na kuisaidia jamii kuepuka udhalilishaji unaofanywa mitandaoni.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Utawala na Rasilimali Watu, Dk. Iddy Khatib Iddy, alisema miongoni mwa malengo ya Taasisi ya Karume ni kutoa taaluma ya mambo yanayoendana na wakati ulioko ikiwamo taaluma ya ulinzi wa mifumo na kompyuta.

Alisema, mafunzo hayo yatawawezesha watu binafsi na taasisi mbalimbali hasa za serikali, kupata ulinzi wa taarifa zao.

Aidha, alitumia fursa hiyo kumwomba Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu na taasisi ya Karume hasa katika kufanikisha suala la kutumia Mkonga wa Taifa.





# Watoto 6,000 wafanyiwa ukatili kwa mwaka

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima (pichani), amesema katika kipindi cha mwaka 2021 watoto 6,000 nchini walifanyiwa vitendo vya ukatili vikiwamo vya ubakaji na ulawiti.

Aliyasema hayo juzi katika kikao kwa njia ya mtandao na wananchi wa Mtaa wa Mwatulole mkoani Geita baada ya kutokea tukio la Jabir Hamis (29) Mkazi wa Magogo Mjini kukutwa na idadi kubwa ya watoto akiwafundisha vitendo vya ubakaji na ulawiti.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana watoto 5,899 nchini walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kubakwa huku watoto 1,114 wakifanyiwa ukatili wa kulawitiwa hali inayotishia mstakabali mzima wa maendeleo na kukwamisha ndoto za watoto hao ikiwa ni pamoja na kukatishwa masomo yao kutokana na kupata ujauzito katika umri mdogo.

**Baada ya kupata taarifa niliwasiliana na Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani naye amesikitishwa na tukio hili tuna taka kukomesha ukatili kwa watoto wazazi nendeni kituoni mkatoe maelezo na watoto wakaeleze walicho kuwa wakifanyiwa.**

Dk. Gwajima alisema kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi amepokea tukio hilo na ameahidi kulifuatilia kwa ajili ya kuchukuwa hatua zaidi za kisheria, hivyo kuwataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu.

Kuhusu baadhi ya askari wasio waadilifu waliokuwa wakijaribu kumtorosha mtuhumiwa huyo, Dk. Gwajima alisema tayari wamewachukulia hatua za kinidhamu.

Waziri Gwajima alisema alipokea simu kutoka kwa Diwani wa Kata ya Buhalala akidai kuwa wananchi wanalalamika kuwa mtuhumiwa huyo ameachiwa na Jeshi la Polisi na kisha kuanza kushughulikia jambo hilo.



"Baada ya kupata taarifa niliwasiliana na Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani naye amesikitishwa na tukio hili tuna taka kukomesha ukatili kwa watoto wazazi nendeni kituoni mkatoe maelezo na watoto wakaeleze walicho kuwa wakifanyiwa ni haki yenu," alisema Dk.Gwajima.

Mwenyekiti wa Polisi Jamii eneo la Fadhili Bucha Mtaa wa Mwatulole, Itanga Timothy, alisema mtuhumiwa huyo walimkamata Desemba Mosi mwaka huu lakini cha kusikitisha walipokwenda polisi kwa lengo la kwenda mahakamani walikuta mtuhumiwa huyo ameshaachiliwa.



Katibu Tawala Msaidizi kutoka Sekretarieti ya Utumishi Mkoa wa Mwanza, Daniel Machunda (wa pili kushoto), akikabidhi kifaa saidizi cha usomaji wa ankara za maji kwa mmoja wa wakusanyaji wa takwimu za maji, Mwidini Juma, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji wa takwimu za maji, jijini Mwanza juzi, ulioambatana na mafunzo ya kuwajengea uwezo wasomaji wa ankara za maji kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kushoto ni Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Waomba kujengewa kituo cha polisi kudhibiti uhalifu

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga wameiomba serikali kuweka kituo cha polisi katika eneo hilo ili kuwasaidia kukabiliana na vitendo vya kihalifu ikiwamo ukatili kwa wanawake na watoto vilivyokithiri.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao walieleza kuwa kukosekana kwa kituo cha polisi katika eneo hilo kumekuwa kukiwakosesha haki zao za msingi hususani wapatapo matukio ya kikatili na kuishia kwa viongozi wa vitongoji, vijiji pamoja na kata kutokana na kutokuwa na eneo sahihi la kufikisha malalamiko yao.

Walipaza sauti yao kwa serikali kufuatia utekelezaji wa mradi wa sauti za kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga(SPC) kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mkazi wa kata hiyo, Dorice Lugina alisema kuwapo kwa kituo cha polisi katika eneo hilo kutawasaidia kupambana na vitendo vya wanaume kutelekeza familia zao hasa kipindi cha mavuno kutokana na vituo vya polisi kuwa mbali.

Alisema kata hiyo ingekuwa na kituo cha polisi wangekitumia kuelekeza malalamiko yao katika dawati la jinsia kwa ajili ya msaada zaidi wanapeleka malalamiko yao kwa wenyeviti wa serikali za vijiji na taarifa zinasambaa na wahusika wanakimbia.

Amina Lutubija alisema ili kupeleka malalamiko yao dawati la jinsia Kituo cha Polisi Didia kwa usafiri wa gari ni Sh. 4,000 kwa pikipiki Sh. 10,00, Kituo cha Mwakitolyo kwa gari Sh. 7,000 kwa pikipiki Sh. 30,000 na Solwa kwa gari Sh. 4,000 kwa pikipiki Sh. 15,000, kwamba wale wasiokuwa na uwezo wanashindwa kupeleka malalamiko yao.

Diwani wa kata hiyo, Veronica Nduta alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kwamba pale inapotokea mwananchi kafanyiwa ukatili kitendo cha kwenda Kituo cha Polisi Solwa, Didia au Mwakitolyo mhusika anakimbia.

# Wanawake wadai kufanyiwa ukatili wakati wa mavuno

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAWAKE wa Kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga, wamesema kila ifikapo kipindi cha mavuno wanaume wao hulazimisha kuuza chakula ili wapate pesa za kununulia pombe.

Wamesema pia wanaume wao huwalazimisha kuuza mazao ili wapate fedha kwa ajili ya kuwahonga wanawake wengine ambao hufika kijijini hapo kwa lengo la kujiuza.

Walieleza hayo juzi wakati wakizungumza na Nipashe lilotembelea kijijini hapo lililotaka kujua hali ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mmoja wa wanawake hao, Suzana Ngassa alisema kipindi cha masika familia yote hua inakwenda shambani kulima, lakini kwenye mavuno baba ndiye anakuwa na sauti na kufikia hatua ya kuuza chakula.

"Wanawake wa hapa kijijini tumekuwa tukinyanyaswa sana na waume zetu kipindi cha mavuno, ukimgomea tu baba asiuze chakula unapokea kipigo, na chakula kikiisha ndani anaitelekeza familia,"alisema Suzana.

Naye Tatu Machalale, alisema yeye alimdhibiti mume wake kuuza chakula bali pesa ambazo huwa anazitumia kunywea pombe ni zile ambazo anazitafuta mwenyewe na siyo zitokanazo na kipato cha familia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masengwa, Zacharia Ntemi, alisema licha ya kuendelea kutoa elimu kwa wanaume kuacha matumizi ya ovyo ya chakula, bado baadhi yao wanaendelea lakini tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa, tofauti na miaka ya nyuma hali ilikuwa mbaya.

Mtendaji wa Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, Hussen Majaliwa, alieleza kuwa tatizo ambalo linasababisha ukatili kuendelea dhidi ya wanawake na watoto, ni baadhi ya wanaume kuendekeza suala la mfumo dume.

Alisema kinapofika kipindi cha mavuno hupokea kesi nyingi za vipigo vya wanawake kutoka kwa waume zao, pamoja na wengine kutelekezewa familia huku chanzo chake kikiwa ni kuuza chakula kwamba mwaka huu alipata kesi tatu.

Baadhi ya wanaume kijijini humo akiwamo Juma Masesa, walikiri kufanya vitendo hivyo na kueleza kuwa tabia hiyo hufanywa na baadhi yao kwa kuuza chakula na kwenda kukifanyia anasa.

Aliiomba serikali iendelee kutoa elimu zaidi juu ya utunzaji wa chakula katika kaya ili kukabiliana na baa la njaa ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wanaoendekeza vitendo hivyo.

# TAKUKURU kuwanasa wanaofanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa

**Na Beatrice Moses**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeweka mtego kuwanasa wanaotajwa kuwa sababu ya wafanyabiashara ndogo kuendelea kufanya biashara kwenye maeneo yaliyozuiwa.

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa umma wa TAKUKURU wilayani Ilala, Elly Makalla, alisema hayo wakati alipohojiwa kwenye kongamano la wadau la kujadili haki za binadamu na utawala bora, maadili na mapambano ya rushwa, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku za Kitaifa ya Haki za Binadamu.

Alisema wana taarifa ya kuwapo kwa baadhi ya watendaji wasio waaminifu wanaojinufaisha kwa njia ya ovu, TAKUKURU imeanza kwa kuchukua jukumu la kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara hao kujua viashiria vya rushwa.

"Tuna taarifa baadhi ya watendaji wale wa chini ambao wamepewa jukumu la kusimamia kuhakikisha kwamba wafanyabishara hawakai kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi wamekuwa wakipokea rushwa na kuwaruhusu kufanyabiashara hasa nyakati za jioni," alisema.

Makalla alisema watendaji hao wanapaswa kusimamia utekelezaji wa utaratibu na sheria zilizowekwa, TAKUKURU wanatafuta taarifa zitakazowawezesha kuwakamata na kuwafikisha mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Alisema mapambano dhidi ya rushwa sio ya serikali pekee ni ya jamii nzima kwa kuwa rushwa inatokea huko kwahiyo TAKUKURU inaamini kuwa wanajamii washiriki kikamilifu katika mapambano kulingana na elimu waliyoitoa. Kanda Maalum Dar es Salaam ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imewataka wananchi kutosita kutoa taarifa zenye ushahidi kuhusu viongozi ambao wanakwenda kinyume na maadili yanayowapasa ili hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria zichukuliwe, kuwezesha maadili kuendelea kuzingatiwa hata kwa viongozi.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Kanda Maalum Dar es Salaam wa sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma, George Bakengesa, alitoa wito huo akieleza kuwa kuna taarifa za tuhuma dhidi ya baadhi ya viongozi kukiuka maadili zikipokelewa, lakini watoa taarifa wanapohitajika husita kutoa ushirikiano.

Bakengesa aliwakumbusha viongozi kuwa dirisha la kujaza fomu za maadili tayari limefunguliwa na litafungwa Desemba 31, mwaka huu.




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (katikati), akijadiliana jambo na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori (TAMSTOA), Mgendela Gama (kushoto), wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa tatu wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa TAMSTOA, Chuki Shaban. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SEZ kutoa fursa mabadiliko kilimo ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KUVUTIA uwekezaji kupitia Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) kwa ajili ya kuongeza thamani katika bidhaa za kilimo inatoa fursa kwa nchi katika harakati za kufanya mabadiliko ya kilimo ili kuongeza mchango katika ukuaji wa uchumi.

Ofisa Mkuu Uhamasishaji na Uwezeshaji wa EPZA, Nakadongo Fares, alisema hivi karibuni kuwa kuongeza thamani katika bidhaa za kilimo inawahakikishia wakulima kupata bei kubwa ya soko na kuongeza kipato chao.

"Maeneo maalum ya SEZ yanatoa nafasi kubwa ya kubadilisha kilimo nchini, kuwahakikishia wakulima masoko ya uhakika na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii katika uchumi," alifafanua.

Alisema kwa sasa viwanda vilivyojikita kwa kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo ndio vinavyoongoza katika maeneo ya uwekezaji chini ya Mamlaka ya EPZA na kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta ya kilimo ambayo hutoa ajira kwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania.

"Eneo la kuongeza thamani katika kilimo limechukua nafasi kubwa katika uvutiaji wa wawekezaji chini ya mamlaka," alisema.

Alisema mamlaka hutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji kupitia SEZ ikiwa ni vya kifedha na visivyo vya kifedha kama misamaha ya kikodi, kodi ya ongezeko la thamani, ushuru mbalimbali katika serikali za mitaa.

Wawekezaji katika maeneo maalum ya SEZ wanaruhusiwa kuuza nje ya nchi hadi asilimia 80 ya bidhaa wanazozalisha na asilimia 20 huuzwa katika soko la ndani.

Pia EPZA huwasaidia wawekezaji kupata ardhi na kuwaunganisha wakulima na masoko ya mbalimbali ya kimataifa duniani na kuongeza upana wa masoko yao.

Kutokana na vivutio vinavyotolewa na mamlaka ya EPZA, asilimia 40 kati ya 97 ya viwanda vilivyojikita katika bidhaa za kilimo vipo ndani ya maeneo maalum ya SEZ kwa ajili ya kuchakata na kuongeza thamani bidhaa za kilimo.

Kwa ujumla, viwanda hivyo vinavyochakata na kuongeza thamani katika maeneo ya SEZ vina mtaji ya Sh. trilioni 1.3 na kutoa kazi kwa Watanzania zaidi ya 20,015 katika kipindi cha 2016 hadi 2021.

Alisisitiza EPZA inawahimiza wawekezaji wa ndani na nje kuchangamkia fursa katika uwekezaji kwenye maeneo ya SEZ ili kuchakata na kuongeza thamani bidhaa za kilimo kwa ajili ya masoko ya nje.

# Waziri ataka unafuu bei kemikali

**Na Mary Geofrey**

WAFANYABIASHARA wa kemikali za kuchenjulia dhahabu nchini, wametakiwa kuziuza kwa bei rafiki ili wachimbaji wadogo wamudu gharama.

Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, alitoa rai hiyo jana wakati akipokea maazimio ya mkutano wa wadau wa uingizaji, usambazaji na watumiaji wa kemikali ya kuchenjua madini ya dhahabu ulioandaliwa na Tume ya Madini na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) jijini Dodoma.

"Kuna sababu za ndani ambazo wafanyabiashara wameamua kuzitumia kutengeneza bei tofauti na halisia, kwa hiyo tumeamua kukutana hapa na ninaamini kwamba mtatusaidia kuja na maelekezo mahususi kwa watu wote waliopewa leseni ya kununua dawa za kuchenjua madini ili wauze kwa bei ya soko.

"Kwa bei hii inayouzwa hivi sasa hakuna mchenjuaji ambaye atapata faida kwa sababu kama watanunua kemikali hiyo Sh. milioni 1.2 na bei ya dhahabu inashuka na kupanda maana yake wachimbaji watakufa," alisema.

Alisema kufuatia kupanda kwa bei ya kemikali ya kuchenjulia dhahabu aina ya Sodium Cyanide kutoka Sh. 400,000 kwa dumu moja hadi Sh. milioni 1.2 kumefanya wachimbaji wadogo kupata hasara.

"Asilimia 41.9 ya fedha zote za kigeni zinatokana na sekta ya madini huku madini ya dhahabu yakichangia asilimia 90 ya kiasi hicho na asilimia 50 ya mauzo ya bidhaa zote nje ya nchi yanatokana na madini huku asilimia 90 ya mauzo hayo yakitokea katika madini ya dhahabu," alisema.

Mkutano huo pia uliazimia, serikali kupitia GCLA, kutoa bei elekezi ya kemikali ya kuchenjulia dhahabu aina ya Sodium Cyanide na kuifanyia mapitio kila baada ya miezi mitatu kwa lengo la kulisimamia soko la bidhaa hiyo.

Pia, uliazimia kuwa wafanyabiashara wa kemikali hizo kuunda umoja wao kama ulivyoundwa na wachimbaji wadogo ambao utawasaidia kujadili na kuwa na nguvu ya pamoja na serikali iunde kikosi kazi cha kufuatilia suala la upatikanaji wa kemikali ya Sodium Cyanide nchini.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Yahya Samamba, alisema katika kipindi cha mwaka 2019 hadi Septemba 2022, jumla ya tani 39,564 za kemikali ya Sodium Cyanide, ziliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya kuchenjua madini ya dhahabu kwenye maeneo ya machimbo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ZAITUN MUSLIM TAYABJI KISMAYUWALLA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 160233** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 06 AUG 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/471959/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 62/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ANDREA MAKACHA NGAITI wa DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA... MESHACK PAULO MAKACHA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 05 Mwezi 12 Mwaka 2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DORAH GADI NGELULA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(BMW)** yenye namba za usajili *T312 DLV* Chasis Namba: **WBAAT52030AH66238** Engine Namba: **N42B18A4236702** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **LIN/NAC/RB/143129/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KIM'S HUNTING SAFARIS TANZTIN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 692 AQX – TOYOTA HILUX.** Chassis namba **PN133JV2508003293.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/472405/2022.**

---

**FORM NO. 58**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF BUNDA DISTRICT**
**AT BUNDA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 23 OF 2022 IN THE MATTER OF ESTATE OF THE LATE SOSPERES MANYAMA SULUSI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF ESTATE BY VEDASTUS MANYAMA SULUSI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to above named petitioner.

The matter comes for mention on the 27th day of 12, 2022 before M.p. Kamuntu at 8:00AM
Dated at Bunda this 06 day of 12, 2022

HON. ..................................

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH LAMECK CHOMETE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 863 DFJ.** Chassis namba **MAT38204ZF7R10.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/470894/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEPHEN SIMON RUGAYI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA BREVIS YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 597 DSF**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI KAH /RB/807/2022**

---


OFISI ZA MATANGAZO,
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX
31042,
DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## JULIA AONYESHA MAHABA MAZITO KWA CLOONEY

NYOTA wa kike wa muvi za Hollywood, Julia Roberts, alionyesha mapenzi makubwa ya kumuunga mkono mkali mwingine wa filamu, George Clooney, katika tuzo za kifahari za Kennedy Center kwa kuvalia gauni lililojaa picha za uso wake.



Gauni hilo refu lenye picha za Clooney zilionyesha historia yake kazi yake ya kucheza filamu - kuanzia picha zake za zamani alipocheza nafasi yake kama Doug Ross katika muvi ya ER na picha maarufu aliyopigwa na Jarida la W.

Clooney alikuwa ni miongoni mwa watu waliopata tuzo ya mafanikio ya maisha katika tukio hilo.

Tukio hilo la nyota mbalimbali lilihudhuriwa na watu maarufu na wanasiasa, akiwamo Makamu Rais wa Marekani, Kamala Haris, Matt Damon, Patti LaBelle, Sean Penn, Sheryl Crow, Garth Brooks na Sacha Baron Cohen.

Wengine ni Paul Pelosi, mume wa Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi, ambaye alijitokeza kwa mara ya kwanza hadharani tangu nyumba yake iliposhambuliwa Oktoba mwaka huu.

Pelosi akiwa amevaa kofia nyeusi alificha majeraha aliyoyapata wakati mtu alipomvamia kwa nyundo, alipigiwa makofi kwa muda mrefu na washiriki, walioonyesha kuwa wako pamoja naye baada ya kuvamiwa.



## ZARI AMNUNULIA GARI JIPYA MPENZI WAKE

MWANAMITINDO Zari Hassan, amemnunulia gari jipya mpenzi wake kijana, Shakib Cham wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa, Jumatatu.

Shakib, ambaye ni raia wa Uganda kama Zari, aliweka picha kwenye ukurasa wake wa Instagram akiwa amekaa juu ya gari jipya kabisa la njano aina ya Jeep.

"Siku yako ya kuzaliwa ibadilishe chuki yote kuwa upendo, kutofaulu kuwa mafanikio, adhabu zote kuwa baraka na vizuizi vyote kuwa fursa. Nakutakia siku njema ya kuzaliwa," Shakib Cham alijiandikia ujumbe huo mwenyewe.

Naye Zari aliandika kwenye ukurasa huo wa mpenzi wake na kummwagia sifa huku pia akilitaja gari hilo jipya.

"Heri ya siku ya kuzaliwa mpenzi wangu na pongezi kwa kupata gari jipya. Baraka zaidi babe," aliandika Zari.

Zari na mzazi mwezake, Diamond Platnumz wanatarajiwa kujumuika pamoja msimu huu wa Sikukuu ya Krismas.



# WEMA

## AWACHARUKIA MASHABIKI WAKE

NYOTA wa kike wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, kwa mara nyingine amecharuka baada ya baadhi ya mashabiki wake kumzodoa kuhusu suala la kutopata mtoto.

Mashabiki hao walikuwa wakimtumia jumbe la kumkashifu kwenye ukurasa wake wa Instagram na yeye alikuja juu na kuwajibu kwa hasira.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wema alitupia picha yake kali na kusindikiza na ujumbe huo kueleza masikitiko yake juu watu ambao hupenda kumsemasema kuhusu suala la kutopata mtoto.

"Afu sikieni niwaambie... Msione kwamba basi mkiniambia nimekosa mtoto basi ndio mnaniweeeza...sawa naumia sikatai na mjue nitazoea...sema mnaboa. Mnaudhi. Najiskia vibaya. Sipendi.

# SERIKALI YATAKA MEDALI TAIFA KUOGELEA AUSTRALIA

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, amewataka wachezaji wa Timu ya Taifa ya Kuogelea, kutokwenda kinyonge katika mashindano ya Dunia nchini Australia na badala yake wahakikishe wanakwenda wakiwa na ari ya kuipambania nchi.

Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika Desemba 13-19, mwaka huu, na timu hiyo yenye jumla ya wachezaji wanne itaondoka nchini kesho, Alhamisi kuelekea nchini humo.

Wachezaji hao wanawake wawili ni Sophia Latif, Ria Save na kwa wanaume ni Collins Salibobo na Hilal Hilal, ambaye ataungana moja kwa moja na wenzao nchini Australia.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana katika hafla fupi ya kukabidhi Bendera ya Taifa kwa timu hiyo, Msitha alisema anaimani nayo kwenda kufanya vizuri kwa sababu ya maandalizi waliyofanya.

Alisema kulinga na maandalizi waliyofanya na uwezo wa mchezaji mmoja mmoja, ana sababu ya kujivunia timu hiyo kwenda kufanya vizuri kwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

"Ninachowaomba wachezaji, msiende kinyonge kwa sababu serikali iko nyuma yenu, naomba mutambue hii bendera nawakabidhi kwa niaba ya Watanzania na mnatakiwa kwenda kuipeperusha vema na kutangaza taifa kwa kupata matokeo mazuri," alisema Msitha.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Asma Hilal, alisema wamefanya maandalizi mazuri kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri kuelekea mashindano hayo.

"Tumekamilisha kila kitu kuanzia maandalizi pamoja na taratibu zote za safar na tunatarajia timu kuondoka nchini Alhamisi ikiwa na wachezaji watatu na mmoja ambaye ni Hilal, ataunga na timu hiyo nchini humo," alisema Asma.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi, alisema wamefanya maandalizi mazuri kwa kuandaa timu kuwa imara na tayari kwa ajili ya mashindano hayo.

"Hii bendera kwetu ni dhamana na tunaenda kutunza heshima ya Tanzania katika kuipeperusha vizuri na sasa tunaenda kanyha vizuri kimataifa," alisema Mwaipasi.

# Azam FC kupotezea dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam huenda isisajili mchezaji yeyote kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili kutokana na kuwa na wachezaji wengi wenye uwezo mkubwa na bado mpaka sasa hawajapata nafasi.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kalimangonga Ongala, amesema kwa sasa hafikirii kuongeza mchezaji yeyote kwa sababu ana wachezaji zaidi ya 32 wenye uwezo mkubwa, huku wengi wakiwa hawajapata nafasi ya kucheza mechi za ligi na michuano mingine.

Ongala alisema hayo baada ya kumalizika kwa mechi yao dhidi ya Polisi Tanzania, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Ushirika mkoani Moshi, ikitoka na ushindi wa bao 1-0, ukiwa ni ushindi wa nane mfululizo tangu alipoichukua timu hiyo kutoka kwa aliyekuwa Kocha Mkuu, Denis Lavagne.

"Hayo mambo ya kuongeza wachezaji dirisha dogo sidhani kama yapo kwa sasa, tuna zaidi ya wachezaji 32 na wana uwezo mkubwa, lakini mpaka sasa hawajapata nafasi, sidhani kama tutaangalia hilo. Hata hivyo, kama likitokea la kuongeza hata mmoja mtaona, lakini sidhani," alisema Kally.

Akizungumzia mechi hiyo, aliwasifu vijana wake kwa kuonyesha uwezo mkubwa hasa kwenye viwanja vya mikoani ambavyo amekiri ni vigumu kupata ushindi kilelemama.

"Vijana wameonyesha uwezo, unajua viwanja vya mikoani vinakuwa vigumu kwa sababu ya mazingira, hali ya hewa na viwanja vyenyewe, Polisi Tanzania ni timu nzuri na sidhani kama ikijipanga vema itashuka daraja. Tunawashukuru mashabiki wa Azam kwa kutupa sapoti, wategemee kuendelea kuiona timu ya ushindani kwenye mzunguko wa pili, mengine anajua Mungu, tunafurahia pointi tatu, lakini tuna safari ndefu," alisema kocha huyo.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa kocha wa zamani wa Yanga, Mwinyi Zahera, lakini kocha Msaidizi John Tamba alisema ujio wa kocha huyo umeonekana kuongeza kitu kwenye kikosi.

"Niwapongeze wachezaji, wamepambana kadri walivyoweza, tulikosa umakini tukafungwa bao, lakini walirejea tena kwenye mchezo wakapambana hadi mwisho.

"Zahera ni mwalimu mkubwa na muda mfupi tu ameongeza kitu, tunaamini kwa uwezo wake, mzunguko wa pili tutakuwa bora zaidi na juhudi itafanyika, timu itaimarika kwa sababu dirisha dogo tunaongeza watu," alisema Tamba.

Wakati Azam FC ikimaliza mzunguko wa kwanza ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi zake 35, Polisi Tanzania inaendelea kuburuza mkia, ikiwa na pointi tisa.

**JUU KWA JUU...**




Beki wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda (kushoto) na wa Polisi Tanzania, Juma Kukuti, wakiwania mpira kwa kichwa kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi juzi na kumalizika kwa Azam kushinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Baseball yazindua mfumo wa ligi yao

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Baseball Tanzania (TaBSA), kimezindua mfumo wa ligi yao itakayofanyika April mwakani ambayo itashirikisha klabu nne za Dar es Salaam huku ikichezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Alfred Nchimbi, alisema ligi hiyo itakuwa inashirikisha klabu zote zinazoshiriki mchezo huo kama zinavyofanya nchi za nje.

"Leo tunafuraha kuzindua mfumo wa ligi ya mchezo wa Baseball ambayo itachezwa kwa muda wa miezi sita," alisema Nchimbi.

Katibu huyo alisema vyama vya michezo vimejipanga kufuata nyayo za wanamichezo waliotangulia, na kudai ligi hiyo itawatoa kwenye mfumo wa ridhaa na kuwa mfumo wa kulipwa.

"Hatuwezi kutoka kwenye mfumo wa ridhaa kwenda mfumo wa kulipwa endapo kama hatutakuwa na mfumo wa ligi imara," alisema.

Naye mdhamini mkuu kutoka nchini Japan, Shinya Tomonari, alisema Tanzania kuna wachezaji wengi wazuri isipokuwa hawana uzoefu wakutosha katika mchezo huo.

Kwa upande wa mchezaji kutoka Klabu ya Dragon, Helen Prosper, alikishukuru chama hicho kwa kuzindua mfumo wa ligi hiyo, kwani mara nyingi wamekuwa hawapati nafasi ya kushiriki kutokana na kubanwa na masomo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Giants, Leodgar Leodinas, yeye alisema ligi hiyo itasaidia kuibua vipaji vya vijana huku akifafanua kwamba mtu yeyote anaruhusiwa kujiunga na mchezo huo ili baadaye wapate timu bora ya taifa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAJITOA KWA BELLINGHAM

KLABU ya Manchester United imejiondoa katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kutoka Borussia Dortmund. Liverpool, Manchester City na Real Madrid zinaongoza katika kinyang'anyiro hicho. ***(Sky Sports Germany)***

### MADRID YATOA MSIMAMO

REAL Madrid haitalipa zaidi ya euro milioni 125 kujaribu kumsajili Jude Bellingham kutoka Borussia Dortmund. ***(Defensa Central)***

### INTER YAJIULIZA KWA DUMFRIES

KLABU ya Inter Milan inapata ugumu kukataa ofa ya euro milioni 50 na nyongeza ya thamani ya euro milioni10 ili  kumpata mlinzi wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa akiwindwa na Chelsea na Manchester United. ***(Calciomercato)***

### SOMMER ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United imeanza mazungumzo katika jaribio lao la kumsajili mlinda mlango wa Uswisi, Yann Sommer, mwenye umri wa miaka 33, ambaye mkataba wake na Borussia Monchengladbach unamalizika msimu wa majira ya joto. ***(Bild, via Mirror)***

### OBLACK ALENGWA UNITED

MCHEZAJI wa kimataifa wa Slovenia na Atletico Madrid, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 29, ndiye anayelengwa sana na Manchester United huku wakipania kuleta kipa mpya. ***(Fichajes)***

### LUIZAO HUYOOO WEST HAM

KLABU ya West Ham itamsajili Luizao wa Brazil kwa mkataba wa miaka mitatu na nusu mara tu mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 na Sao Paulo utakapokamilika mwishoni mwa Januari. ***(90 Min)***

### AZPILICUETA ATOA SABABU

MLINZI wa Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 33, amesema aliamua kubaki Chelsea badala ya kuhamia Barcelona msimu wa majira ya joto kwa sababu wamiliki wapya wa klabu hiyo ya Stamford Bridge "walionyesha kwamba wanataka nibaki". ***(90 Min)***

### MADRID WAMUWANIA CESAR

REAL Madrid inavutiwa na Cesar Azpilicueta na wanaweza hata kuipatia Chelsea ofa ya kumnunua beki huyo wakati wa dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa Januari. ***(Fichajes)***

### ROBINSON ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inaangalia uwezekano wa kumnunua mlinzi wa Fulham, Antonee Robinson mwenye umri wa miaka 25, ambaye amevutia sana wakati akiichezea Marekani kwenye Kombe la Dunia la 2022. ***(Teamtalk)***

### WACHEZAJI ENGLAND NA USALAMA

WACHEZAJI wa England wameshauriwa kutathmini upya hatua zao za usalama baada ya nyumba ya winga wa Chelsea, Raheem Sterling kuvamiwa alipokuwa Qatar kwenye Kombe la Dunia. ***(Times)***

### KESSIE AWINDWA NAPOLI

Napoli imejiunga na klabu kadhaa zinazomtaka kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, mwenye umri wa miaka 25, ambaye anapendelea kubaki Barcelona. ***(Relevo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR: NIMEFARIJIKA KUREJEA KUISAIDIA BRAZIL

**Nililia sana, siwezi kuridhika kwa asilimia 100, nimepewa tuzo ya mchezaji bora wa mechi leo (juzi) lakini...**

**DOHA, Qatar**

NEYMAR amesema amefurahia kurejea uwanjani baada ya kupona jeraha na kuchangia katika ushindi wa Brazil wa mabao 4-1 dhidi ya Korea Kusini katika mechi ya Jumatatu ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain alikosa mechi mbili za mwisho za Kundi la Brazil baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu katika mchezo wa kwanza wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Serbia, Novemba 24, mwaka huu.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alionekana kuwa anafaa kucheza dakika 81 za mechi ya upande mmoja dhidi ya Korea Kusini na kufunga bao la pili kwenye Uwanja wa 974.

Neymar amekiri alihofia hali mbaya zaidi alipouguza jeraha kwa siku 11 zilizopita na amefurahi sasa kurejea uwanjani akicheza na kufunga. "Niliogopa sana," alisema katika mahojiano yake baada ya mechi hiyo.

"Nilikuwa naendelea vizuri baada ya kuanza vema msimu huu, kwa hiyo kupata jeraha kama lile nililokuwa nalo ilikuwa ngumu sana.

"Nilipitisha usiku kucha nikilia sana. Lakini kila kitu kilifanikiwa mwishowe, juhudi zilifaa. Mateso yote ni halali.

"Napenda kumshukuru Mungu kwa nguvu niliyopewa kurejea uwanjani, kuweza kufanya mazoezi na kufanya kila nilichohitaji ili niwapo tena uwanjani.

"Shukrani pia kwa madaktari, wafanyakazi wenzangu na wale ambao wamenitia moyo katika siku za mwisho. Nina furaha kurejea uwanjani na kucheza vizuri."

Alipoulizwa kama alihisi maumivu yoyote kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Rodrygo, Neymar alisema: "Hapana, sikuhisi chochote. Niliridhika sana na uchezaji wangu, lakini hiyo ilisema tunaweza kuboresha kila wakati.

"Siwezi kuridhika kwa asilimia 100. Nimepewa tuzo ya mchezaji bora wa mechi leo (juzi) lakini ni ya kila mtu. Nina furaha sana na uchezaji wa wote."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 417,

MECHI KALI
SINGIDA BS FC
VERSUS
COASTAL UNION
1 | 1.79
X | 3.20
2 | 5.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA, UNITED MACHO KWA DUMFRIES



**LONDON, England**

MLINZI wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries, ameripotiwa kuwa atapatikana katika dirisha dogo la usajili la Januari kwa euro milioni 50, huku Chelsea na Manchester United zikitajwa kuwa na nia ya kumsajili.

Dumfries mwenye umri wa miaka 26, alifurahia matokeo mazuri katika mchezo wa kwanza wa mtoano wa Uholanzi nchini Qatar, akichangia bao na kutoa pasi mbili za mabao katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Marekani.

Anaendeleza hali yake nzuri kwa nchi yake, pia akijivunia mabao mawili na asisti katika mechi tano za Ligi ya Mataifa ya Uefa mwaka huu, huku akiongeza pasi tatu za mabao kutokana na mechi 15 za Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu.

Inter wanashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Serie A na klabu ingependa kumbakisha mchezaji anayeanza mara kwa mara katika kikosi chao, lakini kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la Calciomercato inadaiwa kuwa ofa yoyote inayozidi euro milioni 50 haitaweza kukataliwa.

Kwa mujibu wa Calciomercato, kocha Simone Inzaghi, anamwona Dumfries kama muhimu kwa mipango yake msimu huu, lakini suala la kifedha linamlazimu kumuachia.

Dumfries mwenyewe alizungumzia kuhusu tetesi za kutakiwa Chelsea baada ya kuibuka mchezaji bora dhidi ya Marekani, akisema "bila shaka ni furaha kubwa kuhusishwa na Chelsea".

United ndio klabu nyingine iliyotajwa kwenye ripoti hiyo, wakati kocha Erik ten Hag akiwa mawindoni kumtafuta beki mpya wa kulia na wanatajwa pamoja na Mholanzi mwenzake na Dumfries, Jeremie Frimpong wa Bayer Leverkusen.

# Pele: Nipo imara na matumaini mengi

**SAO PAULO, Brazil**

GWIJI wa soka wa Brazil, Pele amesema "nipo imara na mwenye matumaini makubwa" wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Sao Paulo.

Katika taarifa yake, alisema jumbe za kumuunga mkono pamoja na kutazama Brazil kwenye Kombe la Dunia zimempa "nguvu".

Hapo awali hospitali hiyo ilisema "bado anaendelea na matibabu na yuko sawa".

Inafuatia ripoti nchini Brazil kwamba alikuwa anaanza huduma ya mwisho wa maisha baada ya tiba ya kemikali ya 'chemotherapy' kushindwa kufanya kazi.

"Rafiki zangu, ninataka kila mtu kuwa mtulivu na chanya," alisema katika taarifa kwenye Instagram.

"Niko imara, nina matumaini makubwa na ninafuatilia matibabu yangu kama kawaida. Napenda kuwashukuru timu nzima ya madaktari na wauguzi kwa huduma zote nilizopata.

"Nina imani kubwa kwa Mungu na kila ujumbe wa upendo ninaopokea kutoka kwa kila mmoja kote duniani na hunifanya niwe na nguvu nyingi.

Pia mimi natazama Brazil inapocheza kwenye Kombe la Dunia!

"Asante sana kwa kila kitu."

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mara tatu mwenye umri wa miaka 82, amekuwa hospitalini tangu Jumanne.



HABARI MICHEZO


515,870

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 07/12/22 | 21:00 | Huesca vs FC Andorra | 2.57 | 2.87 | 2.92 |
| 2. 07/12/22 | 23:00 | Tenerife vs Alaves | 2.46 | 2.83 | 3.13 |
| 3. 08/12/22 | 16:00 | Burgos vs Eibar | 2.98 | 2.93 | 2.48 |
| 4. 08/12/22 | 17:00 | Modena vs Venezia | 2.34 | 3.12 | 3.02 |
| 5. 08/12/22 | 17:00 | Reggina vs Frosinone | 2.63 | 2.78 | 2.93 |
| 6. 08/12/22 | 17:00 | Cittadella vs Bari | 2.46 | 2.92 | 3.02 |
| 7. 08/12/22 | 18:15 | Lugo vs Sporting Gijon | 2.93 | 3.08 | 2.42 |
| 8. 08/12/22 | 20:30 | UD Ibiza Eivissa vs Racing Santander | 2.62 | 2.97 | 2.77 |
| 9. 09/12/22 | 11:45 | Brisbane Roar vs Adelaide United | 2.45 | 3.48 | 2.63 |
| 10. 09/12/22 | 21:30 | Villefranche Sur Saone vs Chateauroux | 2.39 | 3.15 | 3.00 |
| 11. 09/12/22 | 21:30 | Sedan vs Cholet | 2.34 | 3.15 | 3.10 |
| 12. 09/12/22 | 21:30 | Avranches vs Nancy | 2.30 | 3.10 | 3.05 |
| 13. 09/12/22 | 22:00 | Netherlands vs Argentina | 3.35 | 3.15 | 2.21 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 07/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4900 | Welayta Dicha FC vs Sidama Bunna SC | 2.73 | 2.78 | 2.68 |
| 15:35 | 4710 | Ittihad Kalba vs Al-Thaid | 1.34 | 4.76 | 6.99 |
| 15:45 | 2803 | Farco FC vs El Daklyeh | 1.86 | 3.35 | 4.20 |
| 15:45 | 3990 | Al Wasl Dubai vs Masafi | 1.10 | 7.77 | 16.52 |
| 15:45 | 5628 | Pyramids vs Arab Contractors | 1.54 | 3.73 | 6.36 |
| 16:00 | 1082 | Singida BS FC vs Coastal Union | 1.79 | 3.20 | 5.00 |
| 16:00 | 4123 | Magara Young Boys vs Flambeau DU Centre | 3.46 | 3.46 | 1.91 |
| 16:30 | 3236 | Gokulam Kerala FC vs Sudeva Delhi FC | 1.52 | 3.89 | 5.45 |
| 16:30 | 3722 | Viterbo Calcio vs Vicenza | 3.56 | 3.12 | 2.01 |
| 16:30 | 4402 | Foggia vs Catanzaro | 3.06 | 3.06 | 2.24 |
| 17:00 | 1134 | USM Khenchela vs MC Magra | 1.80 | 3.17 | 4.39 |
| 17:00 | 1664 | Iskra vs Buducnost | 4.18 | 3.35 | 1.78 |
| 17:00 | 2543 | HB Chelghoum Laid vs US Biskra | 5.44 | 3.30 | 1.63 |
| 17:00 | 2629 | Rukh Vinnyky vs Chernomorets Odessa | 2.02 | 3.26 | 3.36 |
| 17:00 | 2724 | CS Constantine vs ASO Chlef | 1.79 | 3.06 | 4.67 |
| 17:00 | 2968 | Paradou AC vs JS Saoura | 3.45 | 2.82 | 2.20 |
| 17:00 | 3594 | El Bayadh vs ES Setif | 3.21 | 2.77 | 2.34 |
| 17:00 | 4374 | Luka Koper vs Tabor Sezana | 1.51 | 3.90 | 5.47 |
| 17:00 | 5147 | USM Alger vs CR Belouizdad | 2.86 | 2.67 | 2.67 |
| 17:30 | 4479 | Al Hidd Club vs Riffa Club | 4.78 | 3.12 | 1.75 |
| 18:00 | 1051 | Argesul Pitesti vs Universitatea Craiova | 3.79 | 3.06 | 1.96 |
| 18:00 | 1916 | Ghazl EL Mahallah vs Al Ahly Cairo | 4.88 | 3.24 | 1.78 |
| 18:00 | 2792 | AD Ceuta B vs FC Sevilla C | 2.31 | 2.85 | 3.50 |
| 18:00 | 4513 | JS Kabylie vs RC Arbaa | 1.65 | 3.45 | 4.86 |
| 18:10 | 3367 | Rustaq Club vs AL Bashair | 1.60 | 3.51 | 5.27 |
| 18:30 | 1794 | Muharraq SC vs AL Badii | 1.48 | 4.10 | 6.60 |
| 18:30 | 4416 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs AL Wahda Scc (UAE) | 2.26 | 3.12 | 2.97 |
| 19:30 | 1110 | Domzale vs NK Celje | 2.83 | 3.46 | 2.18 |
| 20:00 | 3432 | Talaea El Gaish vs Zamalek | 4.77 | 3.13 | 1.83 |
| 20:00 | 3618 | Virtus Entella vs Renate | 2.25 | 3.02 | 3.07 |
| 20:00 | 4124 | MC Oran vs MC Alger | 3.85 | 3.02 | 1.97 |
| 21:00 | 1117 | Racing Ferrol vs CD Linares | 1.73 | 3.46 | 4.28 |
| 21:00 | 1297 | Huesca vs FC Andorra | 2.57 | 2.82 | 2.97 |
| 21:00 | 3255 | FC Cartagena vs Villarreal B | 1.73 | 3.47 | 4.66 |
| 21:00 | 3495 | KF Tirana vs Vllaznia | 2.17 | 2.97 | 3.31 |
| 21:00 | 4366 | Amorebieta vs CD Calahorra | 2.16 | 3.07 | 3.22 |
| 21:00 | 4697 | Farul Constanta vs CFR Cluj | 2.53 | 2.91 | 2.77 |
| 21:00 | 4954 | Universitatea Cluj vs Rapid Bucuresti | 3.16 | 2.87 | 2.30 |
| 21:00 | 5218 | Padova vs Juventus U23 | 2.35 | 3.07 | 2.87 |
| 21:30 | 3763 | Sporting Farense vs Maritimo | 2.35 | 3.26 | 2.96 |
| 22:30 | 5857 | Ternana vs Cagliari | 2.47 | 3.12 | 2.82 |
| 22:45 | 1500 | Stockport vs Charlton | 2.01 | 3.50 | 3.30 |
| 22:45 | 1894 | Kidderminster vs Chester | 1.86 | 3.56 | 3.56 |
| 22:45 | 5347 | Kingstonian vs Lewes | 2.36 | 3.40 | 2.62 |
| 23:00 | 1217 | Tenerife vs Alaves | 2.31 | 2.82 | 3.42 |
| 23:00 | 1569 | Leonesa vs San Fernando CD | 2.07 | 3.20 | 3.30 |
| 23:00 | 2108 | Barcelona B vs CD Eldense | 2.17 | 3.06 | 3.21 |
| 23:00 | 2339 | Cordoba vs Pontevedra | 1.41 | 4.20 | 6.64 |
| 23:00 | 5703 | CD Castellon vs Numancia | 1.97 | 3.21 | 3.55 |
| 23:30 | 4039 | Rio Ave vs Sporting Lisbon | 4.81 | 3.95 | 1.64 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# CHAMA HASHIKIKI KWA 'ASSIST', LOMALISA AANZA KUWA TISHIO

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba raia wa Zambia, Clatous Chama, anaongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao 'assist' kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inamalizia mzunguko wa kwanza.

Wakati Chama akiwa kinara wa 'assist', kiungo mshambuliaji wa Geita Gold, Saido Ntibazonkiza, Ayoub Lyanga wa Azam na Sixtus Sabilo wa Mbeya City wanapo kwenye kasi moja ya kumfukuzia kwa karibu, huku beki wa kushoto wa Yanga, Joyce Lomalisa raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akianza kuwa tishio kwa kutoa pasi za mwisho zilizozaa mabao kwenye ligi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Chama ana 'assist' saba mpaka sasa, lakini anawazidi kwa moja kina Ntibazonkiza, Lyanga na Sabilo ambao wana sita kila mmoja mpaka sasa.

Kutokana na takwimu hizo ni kwamba Chama licha ya kuwa anaongoza kwa wachezaji wote Ligi Kuu, lakini pia anawaongoza viungo wote washambuliaji kwa 'assist', Lyanga akiwa kinara kwa mawinga na Sabilo akiwa na 'assist nyingi kwa mastraika wote wa Ligi Kuu.

Beki wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', anaongoza kwa 'assist' nyingi kwa mabeki akiwa ana pasi za mwisho nne sambamba na Nicolaus Gyan wa Singida Big Stars.

Wenye 'assist' tatu kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ni wachezaji wa Yanga, Jesus Moloko na Lomalisa, Ismail Mhesa wa Mtibwa Sugar na Awadh Juma wa Mbeya City.

Hata hivyo, Lomalisa anakuwa na 'assist' tatu akiwa hajacheza mechi nyingi kwani ameanza kuaminiwa siku za karibuni tu, lakini ameonekana kuonyesha uwezo mkubwa wa kutoa pasi za mwisho na kuwa tishio kwa wachezaji wengine wakali wa 'assist' kwenye Ligi Kuu Bara inayoingia mzunguko wa pili.

## SASA PENALTI...




Shabiki wa Japan na Croatia wakishuhudia hatua ya 'matuta' (penalti), wakati timu zao zikimenyana kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia nchini Qatar jana baada ya dakika 120 kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Croatia ilitinga robo fainali baada ya kupata penalti 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, NAMUNGO PATACHIMBIKA LEO

INATOKA UK. 32

ni timu nzuri na tunacheza ugenini, lakini uzuri tunacheza kwenye kiwanja ambacho kinachezeka," alisema Kaze ambaye atakuwa anakaimu nafasi hiyo kwa mechi ya pili.

Kwa upande wa beki wa timu hiyo, Kibwana Shomari, amesema utakuwa mchezo mgumu, lakini kwao kila mechi ni fainali na watahitaji pointi tatu ili wajiweka salama kwani ligi imeshakuwa ngumu.

"Ukiangalia timu zimelingana pointi hasa juu, na zimepishana pointi chache tu kwa hiyo, sisi tunachofanya ni kushinda na kupata hizo pointi. Nakumbuka mimi binafsi hii itakuwa ni mara ya nne kucheza dhidi ya Namungo, nilicheza mara mbili na Yanga, nikashinda moja Dar es Salaam, Lindi tukatoka sare, halafu nilipokuwa Mtibwa Sugar nilicheza na timu hiyo Lindi tukafungwa," alisema beki huyo.

Namungo, pamoja na kwamba itakuwa nyumbani, lakini icheze kwa tahadhari kwani mechi iliyopita ilipoteza kwa kichapo cha mabao 3-0 ugenini, Uwanja wa Liti, Singida dhidi ya Singida Big Stars Ijumaa iliyopita.

Timu hiyo ambayo msimu huu inaonekana bado haijakaa vizuri, iko kwenye nafasi ya tisa, ikiwa na pointi 18, inahitaji ushindi ifikishe pointi 21 ipande hadi kwenye nafasi ya nane ambayo kimahesabu ndiyo inaweza kufika hapo.

Michezo
Jumatano Desemba 7, 2022
Nipashe



UKURASA 30

**Chelsea, United macho kwa Dumfries**

ULINZI MKALI...



Mshambuliaji wa Brazil, Neymar, akijaribu kuipenya safu ya ulinzi ya Korea Kusini chini ya Jung Woo-young (kushoto), kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia iliyopigwa katika Uwanja wa 974, Qatar jana na Brazil kutinga robo fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, NAMUNGO PATACHIMBIKA LEO

## Mayele, Job ndani, kocha asema ni mechi ngumu lakini...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Mabingwa Watetezi, Yanga, leo wanamalizia mechi ya mzunguko wa kwanza wa ligi kwa kushuka katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi kuvaana na wenyeji, Namungo FC.

Ni mechi ya kiporo iliyokuwa imeahirishwa wakati timu hiyo ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Hiyo itakuwa ni mechi ya kwanza kwa Yanga kucheza ugenini tangu ipoteze kwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu Novemba 29, lakini pia wa kwanza tangu icheze nyumbani na kushinda bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons Jumapili iliyopita.

Yanga ambayo kimahesabu tayari itamaliza mzunguko wa kwanza ikiwa kileleni, itakuwa na kazi moja ya kushinda mechi hiyo kwa ajili ya kuweka pengo kubwa la pointi baina yake na wanaoifukuza.

Ushindi kwenye mechi ya leo utaifanya timu hiyo kuepuka kuwa sawa kwa pointi na Azam FC, badala yake kuweka tofauti ya pointi tatu juu.

Ina pointi 35 sawa na Azam, lakini iko juu kwa sababu imefunga mabao 25 dhidi ya 22 ya wanaoshika nafasi ya pili.

Pointi 38 zitaifanya Yanga kuwa salama zaidi kileleni, huku ikijipanga na mechi za mzunguko wa pili.

Leo itakuwa inacheza mechi ya pili bila kocha wake, Nasreddine Nabi, ambaye amefungiwa kukaa kwenye benchi kwa mechi tatu baada ya kuonyesha utovu wa nidhamu kwenye dhidi ya Ihefu iliyopigwa Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kwenye mechi ya leo kutakuwa na urejeo wa wachezaji wawili, straika Fiston Mayele na beki wa kati, Dickson Job, ambao hawakuonekana katika mchezo dhidi ya Ihefu.

"Mechi ni ngumu kwa sababu Namungo

INAENDELEA UK. 31

## Phiri atoa neno tamu Simba SC

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba na kinara wa mabao Ligi Kuu Bara, Mosses Phiri, ameweka wazi vipaumbele viwili katika msimu huu ndani ya kikosi hicho kinachoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoingia mzunguko wa pili wiki ijayo.

Phiri amefunga mabao 10 katika Ligi Kuu na kutikisa nyavu mara tano katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua za awali na raundi ya kwanza, hivyo kuiwezesha Simba kutinga makundi.

**Akizungumza na gazeti hili jana, kinara huyo wa mabao ndani ya ligi, Phiri ambaye anashika nafasi hiyo sam bamba na Fiston Mayele wa Yanga, alisema anatamani kuwa mfungaji bora lakini hicho ni kipaumbele chake cha pili kwani cha kwanza ni kuipa Simba ubingwa wa Ligi Kuu kwanza.**

Alisema anamwomba Mungu kumpa afya njema ili aweze kuendelea na kasi yake ya kusaidia timu yake kupata matokeo mazuri na kufikia malengo, lakini na yeye kutafuta tuzo ya ufungaji bora kwa msimu huu.

"Nashukuru Mungu ndani ya duru la kwanza licha ya kukosa baadhi ya mechi, kwa ushirikiano na wachezaji wenzangu, nimeweza kufanya lile nililokuwa naamini naenda kulitimiza kwa kusaidia timu kupata matokeo," alisema kinara huyo.

Alisema yupo Simba kwa kazi maalum ikiwa ni kukisaidia kikosi cha timu hiyo kufikia yale yanayotarajiwa na mashabiki na wanachama ikiwamo kusaka ushindi kila mechi.

"Simba kuna wachezaji wengi wazuri kwa kushirikiana na wao katika duru la pili, naweza kufunga zaidi ya haya mabao niliyofunga sasa kwenye ligi na nikaendelea na makali hadi kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika,"alisema Phiri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >